

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Saba - Tarehe 17 Juni, 2004

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

DUA

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 59

Mikakati ya Kuhifadhi Mazingira

MHE. JENISTA J. MHAGAMA aliliza: -

Kwa kuwa tatizo la hifadhi ya mazingira ni endelevu kwa sasa katika nchi yetu na kwa kuwa matokeo yake ni yenye athari kubwa kwa nchi yetu kiafya, kiuchumi na hata kimaendeleo: -

(a) Je, Serikali ina mikakati gani endelevu ya kuhifadhi mazingira ukiondoa ile ya Taifa ya upandaji miti?

(b) Je, ni wadau gani wa ndani wameshirikishwa katika nchi yetu na hasa katika maeneo ya vijiji na miji midogo katika mipango ya kuhifadhi mazingira kwa faida ya Taifa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ili kusimamia na kuhifadhi mazingira ya nchi yetu, Serikali ilipitisha Sera ya Taifa ya Mazingira mwezi Desemba, 1997. Sera hii imeainisha matatizo makubwa sita yanayohitaji suluhisho la haraka. Matatizo hayo ni uharibifu wa ardhi, kutopatikana kwa maji safi kwa wakazi wa mijini na vijijini, uchafuzi wa mazingira, upotevu wa

makazi ya viumbepori na bioanuwai, uharibifu wa viumbe wa majini na uharibifu wa misitu.

Hivyo, Serikali imetambua na kuainisha matatizo haya ya mazingira nchini ambayo ni zaidi ya yale ya uharibifu wa maliasili zetu. Katika kupambana na matatizo haya, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuitisha programu na miradi ya utekelezaji wa sera ya mazingira na kuweka mikakati madhubuti ya kusimamia hifadhi ya mazingira hasa kwa kuzingatia maeneo haya sita niliyoyataja. Baadhi ya mikakati na programu hizo ni pamoja na: -

Programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria. Programu hii ambayo awamu ya kwanza imekamilika, inalenga katika kuhifadhi mazingira ya Ziwa Victoria na inatoa kipaumbele katika kudhibiti magugumaji, kuendeleza uvuvi bora, kudhibiti uchafuzi wa maji na utupaji taka za majumbani na viwandani, pamoja na kuhifadhi ardhi, misitu, vyanzo vya maji na maeneo owevu.

Programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Tanganyika. Programu hii inashirikisha nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia. Programu ina miradi miwili inayohusu Hifadhi ya Bonde la Ziwa Tanganyika na udhibiti wa maji taka katika Halmashauri ya Kigoma/Ujiji.

Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (*Climate Change*). Mpango huu unaandaliwa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha cha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, tunayo pia Miradi ya Hifadhi ya Mazingira ya Pwani ambayo inalenga katika kutayarisha miongozo ya ufugaji endelevu wa samaki na usimamizi bora wa maeneo ya pwani ambayo mingi inatekelezwa kwa Wananchi wenyewe.

Aidha, Programu ya Kudhibiti Kemikali Chakavu inatarajiwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha. Programu hii ina lengo la kusafisha mlundikano wa madawa na sumu mbalimbali chakavu za kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mifano hii michache ni dhahiri kuwa, Serikali inatekeleza shughuli mbalimbali za kusimamia na kuhifadhi mazingira ukiondoa zile za upandaji miti.

(b) Wadau wa ndani katika suala la hifadhi ya mazingira ni pamoja na Serikali na Taasisi zake, Sekta Binafsi, Makampuni mbalimbali, Vyombo vya Habari na wahisani wa ndani. Ili kushirikisha wadau hao katika hifadhi ya mazingira, Sera ya Taifa ya Mazingira inaelekeza uundwaji wa Kamati za Mazingira katika ngazi mbalimbali ikiwemo ngazi ya vijiji na Serikali za Mitaa. Hadi sasa Kamati hizo zimeundwa katika maeneo mengi. Aidha, Serikali imeendesha warsha za kuelimisha na kuhamasisha wadau kutoka Wilaya zote za Tanzania Bara, kuhusu wajibu na majukumu yao katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira. Washiriki wa warsha hizo ni pamoja na Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya. Wadau

mbalimbali pia wameshirikishwa katika mashindano ya usafi wa mazingira katika Halmashauri za Jiji, Manispaa na Miji. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, Wananchi na Halmashauri ya Mji wa Songea, kwa kuwa mshindi na kukabidhiwa tuzo ya kikombe wakati wa sherehe za Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu kule Kasulu, Mkoani Kigoma. (*Makofi*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa malengo ya Kiserikali ya fedha katika nchi yetu ni kuhakikisha kwamba, tunafikia malengo ya kikarne ya kupambana na umaskini na kwa kuwa mazingira bora na yenye kuboreshwa ni hali halisi ya upambanaji wa umaskini katika maisha ya vijijini na ya wanajamii wengi walio chini:-

(a) Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni wakati muafaka sasa wa kuingiza programu maalum ya kuboresha teknolojia mbadala katika maeneo ya vijijini ili kuhifadhi mazingira na misitu ambayo imekuwa ikiharibika kwa wingi katika nchi yetu?

(b) Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa imefikia wakati mwingine muafaka wa kuona umuhimu wa kuingiza programu maalum ya kuhifadhi maeneo ya machimbo ambayo yamekuwa yakiharibiwa sana na kupoteza hifadhi ya mazingira katika nchi yetu ya Tanzania? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA): Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni jambo muhimu na la msingi kiteknolojia kuingiza programu ambazo zinatuwezesha kuondokana na matatizo ya matumizi ya bioanuwai katika kupata nishati na shughuli zetu nyingine zote za maendeleo. Teknolojia ni kitu cha msingi na ni kitu ambacho kinatuhakikishia maendeleo endelevu. Kwa hiyo, katika hilo nakubaliana naye. Nia tunayo na sababu tunayo, tatizo tu ni kwamba, uwezo hatujaupata.

Mheshimiwa Spika, kuhusu programu maalum ya kuhifadhi maeneo ya machimbo, ningependa kujibu kwamba, katika Ofisi ya Makamu wa Rais, mradi wowote unaotarajiwa kutekelezwa, kama tunavyofahamu shughuli yoyote ile itakuwa na athari kwa mazingira, lakini hii haina maana kwamba tusifanye lolote. Tunachotakiwa ni kutambua athari kwa mazingira kwa mradi unaohusika na kumweleza au kumtaka mtekelezaji atekelze kile tunachokiita kwa Kiingereza "*Environmental Impact Assessment*", kutambua athari kwa mazingira kwa kila tunachokifanya ili tusije tukapata hasara zaidi kuliko manufaa tunayoyategemea. (*Makofi*)

Na. 60

Mpango wa Kuondoa Umaskini

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali imeandaa Mpango wa Kuondoa Umaskini ifikapo mwaka 2025: -

(a) Je, ni miradi ipi ambayo Serikali imeanzisha hadi sasa ambayo inalenga kwa makusudi kuondoa umaskini ifikapo mwaka huo wa 2025?

(b) Je, umaskini umepungua kwa asilimia ngapi tangu mpango huo ulipoanza na ni vigezo gani vimetumika kuhakikisha kuwa umaskini umepungua kwa asilimia hiyo?

(c) Je, kwa nini Wananchi wanaonekana kuwa na hali mbaya ya maisha kwa sasa ikilinganishwa na miaka ya nyuma wakati tunasema umaskini utatoweza ifikapo mwaka 2025?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Ni kweli kwamba, Serikali imeandaa mkakati wa kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2025. Mkakati wa Kupunguza Umaskini wa mwaka 2000 ambao kwa sasa unafanyiwa mapitio kwa lengo la kuboresha ili kuleta mafanikio zaidi kwa Wananchi, unalenga kutuwezesha kufikia lengo la kupunguza umaskini uliokithiri kwa nusu ifikapo mwaka 2010 na kuuondoa kabisa ifikapo mwaka 2025. Watekelezaji wakuu wa jitihada za kupambana na umaskini ni Wananchi wenye kwa kushirikiana na Sekta za Serikali, Taasisi za Kijamii, Taasisi za Taaluma mbalimbali na wahisani. Mpaka sasa kuna miradi mingi ya Serikali katika Wizara mbalimbali inayokusudia kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, miradi ambayo Serikali imeanzisha hadi sasa kwa lengo la kuondoa umaskini ni pamoja na: Mradi wa *Tanzania Social Action Fund (TASAF)*, ambao katika awamu yake ya pili utalenga kutoa huduma katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), Mradi wa *Small Entrepreneurs Loan Facility (SELF)*, ambao unatoa huduma katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Dodoma, Morogoro, Singida, Pwani, Pemba na Unguja, Mpango wa kuzuia rushwa unaosimamiwa na Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mkakati wa kuendeleza kilimo (ASDB), Mkakati wa kuendeleza viwanda vidogo vidogo (*SMEs*) na Mpango wa kuboresha huduma unaozingatia sifa na usimamizi unaopima matokeo ya kazi chini ya Idara Kuu ya Utumishi (*Public Service Management*) na kadhalika.

Wakati huo huo, Bajeti za Serikali zilizopitishwa tangu mwaka 2000 hadi sasa zimekuwa zinalenga kutekeleza mkakati wa kuondoa umaskini kwa kuongozwa na vipaumbele tulivyojiwekea kwenye elimu, ujenzi, maji, utawala bora na afya.

(b) Mheshimiwa Spika, idadi ya watu wanaoishi katika umaskini imepungua kutoka asilimia 38.6 mwaka 1991/92 na kufikia asilimia 35.3 mwaka 2000/2001 na idadi ya wanaoishi katika umaskini uliokithiri imepungua kutoka asilimia 21.6 mwaka 1991/92 na kufikia asilimia 17.7 mwaka 2000/2001, kama inavyoonyesha katika Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (*Household Budget Survey 2000/2001*). Upunguaj mdogo huo umejionyesha zaidi kwenye Jiji la Dar es Salaam. Vigezo vinavyotumika kuangalia kama umaskini umepungua ni vile vilivyoainishwa katika mpango wa ufuatiliaji (*Poverty Monitoring Master Plan*) na hasa viashiria vinavyopima umaskini wa kipato kupitia kuboreka kwa huduma za jamii hususan elimu, afya, barabara, nishati, nyumba bora na kadhalika kama nilivyosema hapo juu.

(c) Mheshimiwa Spika, sababu kubwa inayochangia Wananchi kuwa na hali mbaya ni pamoja na kuanguka kwa bei za mazao ya biashara na chakula, suala ambalo kwa sehemu kubwa ni la kidunia. Wananchi wengi na hasa waishio vijijini ambako umaskini unaonekana haujapungua, wanategemea sana kupata fedha kwa kuuza mazao ya kilimo. Kwa mfano, bei ya kahawa, chai na mazao mengine zinaposhuka kwenye soko la dunia, hali ya kipato cha Wananchi huwa inashuka pia na kufanya hali zao kimapato kuwa mbaya. Aidha, ili kupata mafanikio ya jithada za kupambana na umaskini, lazima uchumi ukue kwa asilimia 8 -10 kwa mwaka. Tanzania hajafikia hapo. Changamoto iliyopo ambayo Serikali inaendelea kuzifanyia kazi ni kuhakikisha kuwa kukua kwa uchumi pia kunawanufaisha Wananchi walio wengi na hasa waishio vijijini, ambao wanafanya 80% ya Watanzania. Kama ilivyobainishwa kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka 2004/2005, mkazo zaidi utawekwa kwenye kilimo, viwanda vidogo vidogo na upatikanaji wa mikopo nafuu. (*Makofî*)

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ukitaka kuangalia umaskini umepungua kiasi gani, mara nyingi tunatumia *per capita income*, tunazungumzia pesa. *Per capita income* ya tangu wakati huo mpango ulipoanza *baseline* kwa sababu nina hakika ilifanyika, mpaka sasa imeongezeka kiasi gani?

Ni juzi tu tulikuwa na semina hapa tukaambiwa kwamba hali ya Wananchi vijijini inaendelea kuwa mbaya, sasa inawezekanaje umaskini ukawa umepungua kiasi hiki kwa sababu hao ndiyo wengi kutoka 21 mpaka 17? (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwa kweli ningeweza nikaunganisha yote mawili kwa kusema kwamba, *survey* ambayo imefanyika ya kupima kupungua au kutopungua kwa umaskini, hizo asilimia za kupungua nimesema kwamba, zimejitokeza zaidi kwenye Jiji la Dar es Salaam. Katika vijiji kutokana na maelezo niliyotoa, bado umaskini haujapungua kwa kiwango cha kuridhisha na ndiyo maana nasema kwamba ili kipato cha Wananchi, kile wanayosema *a capital income*, kiweze kuongezeka ndipo tutakapoona matokeo ya kupungua kwa umaskini kwa sababu umaskini tunaousema hapa ni ule wa kipato (*Income Poverty*) ndiyo wanaoona Wananchi kwamba haujapungua. Tukikazia utaratibu wa kilimo na kufuatilia utelekezaji wake tunaweza tukaongeza kipato cha kila mwananchi kwa maana ya *per capita income* pamoja na kuongeza kipato cha mfukoni. Kwa hiyo, ninakubaliana na Waheshimiwa

Wabunge walipokuwa wamechangia kwenye semina kwamba, kuna haja ya kutilia mkazo kilimo. (*Makofi*)

MHE. ESTHERINA KILASI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wakati anajibu swali la msingi ametamka rasmi kwamba, *TASAF* ni mpango mmojawapo ambao umesaidia kupunguza umaskini, lakini wakati anajibu swali lake mwaka 2003 sikumbuki ni mwezi gani aliahidi mwenyewe mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba ifikapo mwaka wa fedha wa 2003/2004, *TASAF* itakuwa imeenea Wilaya zote za Tanzania. Je, anatuahidi nini leo kuhakikisha kwamba *TASAF* itakuwa imeenea Wilayani kote Tanzania? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO): Mheshimiwa Spika, kwa sababu humu Bungeni tunapendana, matatizo yaktitea tunapeana pole, kuitia rafiki yake, nimesikia kwamba, Mheshimiwa Estherina Kilasi, alipata ajali juzi, nampa pole kwanza. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ni kweli mwaka 2003 wakati wa Hotuba ya Makamu wa Rais, tulitegemea na tulisema kwamba, *TASAF* ambayo inatekelezwa kwenye Wilaya 40 kwa hivi sasa kwa mwaka huu wa fedha amba unaishia tarehe 30 Juni, *TASAF* ingekuwa imeenezwa katika maeneo mengine yaliyobaki, lakini hilo halijafanyika na sababu kubwa ni kwamba, sehemu ya mkupuo wa kwanza wa *TASAF* wa hizo Wilaya 40, mkataba wetu na Benki ya Dunia unaisha Desemba, 2004.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana wakati namjibu Mheshimiwa Hassan Chande Kigwallilo, Mbunge wa Liwale, swali la kutaka kuelewa *TASAF* ya awamu ya pili itaanza lini nilisema na ninarudia kusema hapa kwamba, tunategemea itaanza mapema Januari, 2005, baada ya kukamillisha awamu ya kwanza kwa nchi nzima.

Na. 61

Gari la Kituo cha Polisi - Kakesio

MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN aliuliza: -

Kwa kuwa gari la Kituo cha Polisi Kakesio Wilayani Ngorongoro ni bovu na kwa kuwa gari hilo lilipelekwa Arusha Mjini kwa matengenezo na sasa ni zaidi ya miaka mitano imepita bila kurudishwa kituoni: -

- (a) Je, ni lini gari hili litatengenezwa na kurudishwa kituoni?
- (b) Endapo gari hilo limetengenezwa na kupangiwa kituo kingine, je, ni lini Kituo cha Polisi Kakesio kitapewa au kupata gari lingine?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mathew T. Ole-Timan, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, gari liliokuwa la Kituo cha Polisi cha Kakesio lenye namba za usajili *STJ 8652* aina ya *Mercedes Benz* liligawiwa kwenye kituo hicho mwaka 1995 ili litumike katika operesheni dhidi ya majangili na majambazi yenyе asili ya Kisomali. Kutokana na wingi wa kazi za operesheni hizo, gari hili lilipata uharibifu mkubwa na ikalazimu lipelekwe Arusha Mjini kwa matengenezo makubwa mwaka 1997. Baada ya matengenezo, gari hili lilionekana halitaweza tena kumudu mikikimiki ya operesheni na hivyo Uongozi wa Polisi Mkoa wa Arusha ukalipeleka katika Kituo cha Makuyuni, Wilaya ya Monduli. Kutokana na hali hiyo, gari hili halitaweza kurejeshwa tena katika Kituo cha Kakesio baada ya kuonekana halitamudu shughuli za huko.

(b) Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Kakesio pamoja na vituo vingine nchini ambavyo kwa sasa havina magari, Serikali inafanya jitihada kubwa kuvitafutia magari. Kikwazo kikubwa ni gharama. Serikali inatafuta fedha kwa ajili hiyo na pindi zikipatikana vituo hivyo vitapatiwa magari pamoja na Kituo cha Kakesio.

MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ni kweli gari limetengenezwa na badala ya kupelekwa Kakesio likapelekwa Makuyuni. Tukizingatia ukubwa wa eneo la Wilaya ya Ngorongoro, uchache wa maaskari na upungufu wa vitendea kazi kama magari, je, isingkuwa vyema kumwongezea *OCD* wa Wilaya ya Ngorongoro, fungu la mafuta kwa ajili ya kuimarisha doria katika Wilaya nzima ya Ngorongoro pamoja na Kakesio?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Wilaya ya Ngorongoro ni kubwa na wanahitaji vitendea kazi. Kwa kuzingatia hali hiyo mpaka sasa Wilaya ya Ngorongoro ina magari matatu ya Polisi, sasa hivi mawili ni mazima, moja ni bovu. Mazima ni *STJ 3881 Land Rover 110* na *STH 8657* aina ya *Mercedes Benz National Wagon*. Lile ambalo ni bovu ni *STJ 891 Land Rover Defender* na hili limo katika utaratibu wa kulitengeneza ili idadi hiyo ibaki kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongezewa mafuta ili magari haya yaweze kutumika katika Wilaya hiyo, ombi la Mheshimiwa Mbunge litazingatiwa, lakini vile vile itategemea na hali ya bajeti yetu.

Medical Kits

MHE. FRANK M. MUSSATI aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikituma *medical kit* moja yenyé dawa mbalimbali kwenye kila zahanati kote nchini na kwa kuwa yapo maeneo kadhaa ya nchi yetu hususan Mkoo wa Kigoma ambayo yamekuwa na ongezeko kubwa la watu kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002 kiasi kwamba *medical kit* moja kwa mwezi haitoshelezi mahitaji ya dawa, kwani *kit* moja inatumika kwa wiki mbili tu: -

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza *kits* hizo kufikia mbili au tatu kwa mwezi kulingana na kuongezeka kwa watu kwenye baadhi ya maeneo ya nchi yetu?

(b) Je, Serikali imekuwa ikikabiliana vipi kimadawa na ongezeko kubwa la watu katika Mkoo wa Kigoma na hasa Wilaya za Kasulu na Kibondo?

WAZIRI WA AFYA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalí la Mheshimiwa Frank Mussati, Mbunge wa Kasulu Mashariki, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, zahanati imepangiwa kuwahudumia wagonjwa wapatao 10,000 na inapelekewa sanduku moja la dawa kila mwezi kuiwezesha kutoa huduma kwa wagonjwa wapya 1,000. Kituo cha Afya kimepangiwa kuwahudumia watu wapatao 50,000 na kinapewa sanduku moja la dawa kukiwezesha kuhudumia wagonjwa wapya 3,000. Mpango wa masanduku ya dawa (*Kit System*) katika zahanati na vituo vya afya una mapungufu kwani hauzingatii mahitaji halisi ya dawa katika vituo hivyo kutokana na tofauti ya maradhi (*Morbidity Pattern*) hapa nchini. Ili kufanikisha upatikanaji wa dawa katika zahanati na vituo vya afya, Serikali imeanzisha mfumo wa utoaji dawa ujulikanao kama *indent system*. Mfumo huu unaziwezesha zahanati na vituo vya afya kuagiza dawa kulingana na mahitaji kwa kuzingatia fedha zilizotolewa. Mfumo huu unaenezwa katika Mikoa kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa napenda kujibu swalí la Mheshimiwa Frank Mussati, Mbunge wa Kasulu Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kuongeza masanduku ya dawa kwa zahanati kutoka sanduku moja la sasa hadi kufikia mawili au matatu na badala yake Wizara yangu itabadilisha mfumo wa utoaji dawa kutoka ule wa masanduku kwenda *indent system* ili kuziwezesha zahanati na vituo vya afya kuagiza dawa kulingana na mahitaji yao. Utaratibu huu utapunguza kwa kiasi kikubwa matatizo ya upungufu na upotevu wa dawa kwenye vituo hivi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya dawa mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitatu bajeti iliongezeka kama ifuatavyo: Mwaka wa fedha 2001/2002 kilitolewa kiasi cha Sh.11,270,002,200/=, mwaka wa fedha 2002/2003 kilitolewa kiasi cha Sh.12,211,805,800/= na mwaka wa fedha ambao unakwisha wa 2003/2004 Serikali ilitenga kiasi cha Sh.22,901,971,414=/. Aidha, utaratibu wa kutoa fedha kwa ajili ya Sekta ya Afya katika Wilaya (*Resource Allocation Formula*), sasa umebadilishwa kutoka ule wa kutoa fedha kwa kufuata idadi ya watu tu na kuanzisha utaratibu mpya unaohusisha idadi ya watu, mzigo wa magonjwa (*Burden of Disease*) na idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

MHE. FRANK M. MUSATI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Serikali inajiridhishaje kwamba hizo *kits* zinatumika kwa walengwa na wala haziuzwi? (*Makofî*)

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, Serikali inajihakikishia kwamba, dawa ambazo zinapaswa kwenda katika vituo vya afya, zahanati na hospitali zinatumika vizuri. Tumeanzisha utaratibu wa kuhakikisha kwamba, kila kituo cha afya kinakuwa na Kamati ya Wananchi wa maeneo yale kuhakikisha kwamba, *kit* imefika, wanakagua *register* ya matumizi na kuhakikisha kwamba, kweli dawa zinatumika. Pale ambapo Wananchi hawasimamii matumizi ya dawa hizi ndipo wizi unatokea. Kwa hiyo, naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali imetoa utaratibu wa usimamizi pale pale kituo kilipo na ndiyo maana tunataka kubadilisha utaratibu wa kugawa *kits* kwa sababu inawezekana hata dawa zinazobaki mwisho wa mwezi ule hazijulikani zinapokwenda. Yote haya yanaelewaka. Kwa hiyo, tunaomba usimamizi ufanywe pale zahanati ilipo.

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mafanikio ya waziwazi ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kuhusu kueneza huduma za afya yameonekana waziwazi na kwa kuwa vile vile mpango wa uchangiaji wa huduma hizi ulioamuliwa na Serikali ni mzuri, lakini yapo matatizo katika utekelezaji hasa kwa maana ya kufika vijiji. Je, Wizara haioni ingekuwa vizuri mpango huu ukatekelezwa awamu kwa awamu mpaka tuone mafanikio yake badala ya kufanya kwa nchi nzima? (*Makofî*)

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mfuko wa Afya ya Jamii ulianza kwa majoribio katika Wilaya ya Igunga na ulifanikiwa sana, ukasambazwa kwenye Halmashauri 10, umeonyesha mafanikio. Waheshimiwa Wabunge baada ya kuona mafanikio hayo, wanadai kwamba badala ya kwenda pole pole tuueneze katika nchi nzima.

Kwa kutambua kwamba nayo ni kazi kubwa sana, mwaka huu wa fedha tumekwenda zaidi katika Wilaya 88 na ni mategemeo yetu kwamba, tutahamasisha katika Wilaya zote zilizobaki katika mwaka ujao wa fedha. Lakini naomba nitoe wito kwamba, hakuna kitu kinachowasaidia Wananchi wetu zaidi kwa matibabu kama Mfuko wa Huduma ya Afya kwa Jamii. (*Makofî*)

Barabara ya Mtwara - Songea - Mbamba Bay

MHE. IRENEUS N. NGWATURA aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Wilaya za Mbinga, Namtumbo na Tunduru hawajawahi kuona barabara ya lami na kwa kuwa wananchi hao walifurahi na kushangilia sana walipomsikia Mheshimiwa Rais akisema katika hotuba yake ya tarehe 12 Februari, 2004 kwamba, upembuzi yakinifu kwa barabara ya *Mbamba Bay* umekamilika na kwa kuwa Marais wa nchi mbili zinazopakana na nchi yetu yaani Rais wa Malawi, Rais wa Msumbiji na Rais wa Tanzania yenyewe wanakaribia kustaafu kwa mujibu wa Katiba za nchi zao:-

(a) Je, barabara ya Mtwara - Songea - *Mbamba Bay* itagharimu fedha kiasi gani?

(b) Je, ni maandalizi gani ambayo mpaka sasa yamefanywa ili barabara hiyo ianze kujengwa kabla Marais wa nchi hizo hawastaafu?

(c) Kwa kuwa yapo maeneo korofi katika barabara hiyo hasa *Mbamba Bay* - Mbinga na Kilimasera - Matemanga, je, Serikali itakuwa tayari kuanza kujenga kwa kiwango cha lami sehemu korofi za barabara hiyo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus Ndunguru Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, gharama halisi ya ujenzi wa barabara ya Mtwara - Songea - *Mbamba Bay* itajulikana rasmi baada ya kupokea na kutathmini zabuni za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, barabara hii yenyewe urefu wa km. 854 katika Bajeti ya 2003/2004 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni moja. Serikali ya Kuwait kuititia mfuko wake wa *Kuwait Fund* ilitoa msaada wa shilingi bilioni moja kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu ambao ulikamili Desemba, 2003. Sehemu ya msaada huo itatumika mwaka wa fedha 2004/2005 kufanya usanifu wa kina wa kilomita 200 kati ya Songea na Matemanga kwa kiwango cha lami. Serikali inaendelea kuwasiliana na wafadhili mbalimbali ikiwemo Serikali ya Kuwait, kwa nia ya kupata fedha za ujenzi ikiwezekana kabla Rais wa sasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hajastaafu. Aidha, maeneo korofi katika barabara hasa *Mbamba Bay* - Mbinga na Kilimasera - Matemanga, yataendelea kufanyiwa matengenezo ya kawaida ili barabara iweze kuitika wakati wote hadi fedha za ujenzi kufikia kiwango cha lami zitakapopatikana. (*Makofî*)

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, napenda Serikali ipokee shukurani za wananchi wa Mbinga kwa kukubali kujenga barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa km 4 Mjini Mbinga. Vile vile ningependa niombe na ninaombea kweli na nina imani kwamba, Mheshimiwa Rais wa Malawi ameshastaifu, ni matumaini yangu kwamba, aliyechukua nafasi yake atakuwa na moto ule ule ili kuhakikisha kwamba, mradi huu unaendelea kwa kasi. Baada ya kusema hayo naomba niulize maswali kama ifuatavyo:-. (*Makofii*)

(a) Ningependa nifahamu kama barabara hii itatumia madaraja ambayo yamejengwa katikati ya Songea na Mbinga, madaraja ambayo yalijengwa kwa ajili ya lami. Je, barabara ya sasa itatumia madaraja hasa ya Mto Ruvuma?

(b) Kwa kuwa eneo hili tayari madaraja yapo, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuanza kuweka lami kutoka Peramiho mpaka Mbinga hasa ikizingatiwa kwamba eneo hilo linalima kahawa nyingi sana?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ili tuweze kujua kama barabara itatumia madaraja ambayo yako kati ya Mbinga na Songea itabidi tungoje usanifu ambaa ndiyo hasa utaamua kama ni vizuri kutumia madaraja hayo ama sivyo, kwa sababu usanifu unaweza ukaepuka madaraja hayo. Kwa hiyo, maamuzi sasa hivi ya kuyafanya hayapo isipokuwa tungoje usanifu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa madaraja ya lami yapo tayari kati ya Peramiho na Mbinga kwa hiyo, ni vizuri kutia lami, bado nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wastahimili tungoje matokeo kwa sababu tuktitia lami sasa hivi hapo kama tulivyotia lami Mjini Mbinga km. 4 kwa sababu tunajua Mji pale Mbinga hauwezi kuhama. Lakini maamuzi ya kati ya Peramiho na Mbinga kutia lami bado tunangojea tuone kama barabara itatakiwa ipite hapo. Si vizuri kutia lami barabara vipande vipande kama unashona viraka vya nguo, ni vizuri ukangoja usanifu na ukapata fedha ukatengeneza barabara hatua kwa hatua inavyostahili. (*Makofii*)

Na. 64

Barabara ya Ulinzi Kando Kando ya Mto Ruvuma

MHE. ARIDI M. ULEDI aliuliza:-

Kwa kuwa kulikuwa na mpango wa kufufua barabara ya ulinzi kando kando mwa Mto Ruvuma na kwa kuwa kufufuliwa kwa barabara hiyo kungesaidia sana kiuchumi na kijamii kwa wananchi waishio kwenye vijiji vilivyomo kando kando ya Mto Ruvuma:-

(a) Je, barabara hiyo ina urefu gani ndani ya Mkoa wa Mtwara?

(b) Je, gharama ya kuifufua ni kiasi gani na itajengwa kwa kiwango gani?

(c) Je, barabara hiyo itaanza kujengwa lini na kumalizika lini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Aridi M. Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, ninapenda kwanza kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuifufua barabara ya Ulinzi kando kando ya Mto Ruvuma, ni utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alilotoa wakati wa ziara ya kikazi Mkoani Mtwara mwezi Septemba, 2002.

Barabara hii ya ulinzi kando kando ya Mto Ruvuma inatoka Kijiji cha Mangamba Wilaya ya Mtwara Mjini hadi Mitema Upinde katika Wilaya ya Masasi. Awali sehemu ya barabara hii, kati ya Mangamba na Kitaya (km. 81) ilikuwa ni ya mkoa na kuhudumiwa na Wakala wa Barabara Mkoa wa Mtwara na kilomita 216.5 zilikuwa zinahudumiwa na Halmashauri za Wilaya ya Mtwara, Newala na Masasi. Baada ya agizo la Mheshimiwa Rais, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*), imeanza kufufua barabara hii ya Ulinzi.

Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara yangu ilitenga shilingi 125 milioni kwa ajili ya kugharamia ukarabati wa kilomita 10 za barabara hiyo. Kazi imefanyika kati ya Vijiji vya Mnongodi na Kilimahewa ambazo zilikuwa hazipitiki. Hadi kufikia Aprili 2004, tayari kilomita 6 zilikuwa zimekamilika kutengenezwa kwa kiwango cha changarawe na barabara inapitika vizuri baada ya ukarabati huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninapenda sasa kujibu swal la Mheshimiwa Aridi Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Barabara ya Ulinzi ndani ya Mkoa wa Mtwara ina urefu wa kilomita 297.5 inayoanzia Mangamba (Mtwara) hadi Mitema Upinde (Mto Ruvuma) mpakani mwa Mkoa wa Mtwara na Ruvuma.

(b) Gharama ya kuifufua na kuijenga kwa kiwango cha changarawe barabara hiyo inakadiriwa kuwa kiasi kisichopungua shilingi bilioni 3.9. Gharama hizo hazihusishi ujenzi wa madaraja matano yenye jumla ya urefu wa mita 200 ambayo yanakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 2.0. Kwa hiyo, kuijenga barabara hiyo kikamilifu kwa kiwango cha changarawe zinahitajika shilingi bilioni 5.9.

(c) Barabara hiyo imekwishaanza kufufuliwa tangu mwaka 2003/2004. Aidha, kwa kuzingatia uwezo mdogo wa Serikali na ufinyu wa bajeti, kazi ya kuifufua barabara za ulinzi itafanywa kwa awamu mwaka hadi mwaka. Mkakati wa Serikali kwa sasa ni kujenga kwa kiwango cha changarawe sehemu za barabara hiyo ambazo hazipitiki ili hatimaye barabara yote ya Ulinzi ndani ya Mkoa wa Mtwara iweze kuitika. Tayari

sehemu ya barabara hiyo ambayo ilikuwa haipitiki kati ya Mnongodi na Kilimahewa imejengwa kwa kiwango cha changarawe na sasa inapitika bila matatizo. (*Makofi*)

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa barabara hiyo, inaunganisha vijiji kadhaa vyenye wakazi wengi na kwa kuwa kazi kubwa katika barabara hiyo ni ukataji wa miti na ulimaji wa nyasi. Je, kwa nini Serikali isiwatumie wananchi wanaoishi katika vijiji hivyo kwa kazi hiyo ya barabara na hasa kwa kuzingatia mafanikio ya miradi ya aina hiyo, ambayo imefadhiliwa na *TASAF* ambayo yameonyesha mafanikio makubwa sana? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa kazi nyingine kubwa katika barabara hiyo ni ujenzi wa madaraja ambayo yalizolewa na mafuriko na mengine kung'olewa baada ya zoezi la ulinzi kumalizika. Je, kwa nini Serikali sasa isiharakishe ujenzi wa madaraja hayo na hasa baada ya kuelezwu hapa Bungeni kuwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madaraja zipo za kutosha, kwa nini madaraja hayo na hasa Daraja la Mto Lukwamba ambalo lilizolewa na mafuriko miaka miwili iliyopita mpaka sasa hivi halijengwi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, mara nyingine tunatumia wananchi kutengeneza barabara, lakini kwa maelekezo ya Rais, juu ya barabara hii, ilikuwa itengenezwe kwa kiwango cha changarawe. Kwa hiyo, ni dhahiri hapa inahitajika mitambo na barabara iliyotengenezwa kwa usahihi kabisa badala ya kutumia wananchi kukata miti na majani tu na hatutakuwa tumetekeleza ahadi yake. Lakini vile vile kutumia wananchi kukata miti na majani hii inawezekana tukishamaliza sisi kutengeneza hiyo barabara. Hiyo ni *tender* ya Mkoa ndiyo inayotumia vikundi mbalimbali vya akina mama na wananchi wengine kukata majani na miti.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi namwomba Mheshimiwa Mbunge, astahimili twende kwa hatua tunayokwenda ili tutimiza ahadi ya Rais kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha changarawe. (*Makofi*)

Ujenzi wa madaraja nilisema katika jibu langu la awali, ujenzi wa madaraja unahitaji shilingi bilioni mbili katika bajeti na tunajitahidi pole pole ili tuone tunaweza kupata kiasi gani cha fedha kujaribu kumaliza matatizo haya ya madaraja. Nilisema hapa tunahitaji shilingi bilioni 5.9 kwa barabara hii, ni kiasi kikubwa sana cha fedha na Mheshimiwa Mbunge, bila shaka atakubaliana nasi kwamba, kwa jinsi bajeti yetu ilivyokuwa finyu, hatuwezi kupata fedha hizi mara moja kwa barabara moja. (*Makofi*)

Na. 65

Utoaji wa Nakala za Kudumu za Kesi Mahakama za Mwanzo

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Kwa kuwa katika kutoa haki, uamuza wa Mahakama hapana budi uonekane katika kumbukumbu rasmi zilizothibitishwa na Hakimu:-

- (a) Je, kwa wastani inachukua siku ngapi kutoa nakala ya hukumu ya kesi?
- (b) Je, anayehitaji kupewa nakala ya hukumu anatakiwa kulipa fedha kiasi gani?
- (c) Je, ni kesi ngapi zimefunguliwa katika Mahakama za Mwanzo mbili zilizoko Bumbuli na Soni katika Jimbo la Bumbuli na ngapi zimefungwa tangu mwaka 1996 hadi Desemba, 2002?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa utaratibu wa Kimahakama upatikanaji wa nakala ya hukumu unaweza ukachukua muda mfupi au mrefu kutegemea na hali halisi ya utendaji kazi wa Mahakama inayohusika. Kama Mahakama ya Mwanzo inayo Mpiga Taipu na mashine ya Taipu ipo kwenye hali nzuri, nakala ya hukumu inaweza kutolewa mapema iwezekanavyo kutegemea na ukubwa wa hukumu na uwingi wa kazi alizonazo Mpiga Taipu huyo. Aidha, kama Mahakama hiyo haina Mpiga Taipu wala mashine ya Taipu, jalada linapelekwa Mahakama ya Wilaya kwa ajili ya kuchapa hukumu, kazi ambayo itachukua muda mrefu zaidi, kukamilifu. Hata hivyo, kulingana na Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa Mahakama, nakala ya hukumu inapaswa kutolewa ndani ya kipindi cha miezi mitatu.

(b) Nakala za kudumu hutolewa kwa utaratibu ufuatao: Katika kesi za jinai nakala za hukumu hutolewa bure na nakala za hukumu za kesi za madai pamoja na mirathi hutolewa kwa kulipia ada. Kwa mujibu wa kifungu cha 65 cha Tangazo la Serikali Na. 233/2001 (*The Courts fees (Amendment Rules 2001)*), kwa kila maneno 100 au pungufu yake ikilipiwa ada ya Sh. 50 lakini ada hiyo haitazidi kiwango cha shilingi 1,000/= kwa nakala nzima ya hukumu;

(c) Kati ya mwaka 1996 na 2002 idadi ya mashauri ya mirathi, madai na jinai kwa pamoja yaliyofunguliwa na kushughulikiwa katika Mahakama za Mwanzo Bumbuli na Soni ni kama ifuatavyo: Katika Mahakama ya Mwanzo Bumbuli yaliyofunguliwa mashauri 1,452, yaliyofungwa yalikuwa 1,392, yalibaki mashauri 60 na katika Mahakama ya Mwanzo Soni yaliyofunguliwa mashauri 1,836, yaliyofungwa yalikuwa 1,765, yalibaki mashauri 71.

Mheshimiwa Spika, iwapo Mheshimiwa William Shellukindo, atataka mchanganuo wa mashauri hayo kuhusu mashauri ya jinai, madai na mirathi wa Mahakama hizi za Mwanzo mbili, nipo tayari kumpatia muda wowote kuanzia sasa.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kwa majibu yake mazuri sana isipokuwa nina swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Bumbuli amesimamishwa kazi na sasa kesi za Bumbuli zinakwenda kufanyika Soni umbali wa km. 44 kwenda na kurudi na kwamba ni usumbufu mkubwa sana kwa sababu wananchi wengine hawana nauli kwa hiyo inabidi watembee kwa miguu.

Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba ni vyema Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Soni apange ratiba ya siku maalum za kwenda Bumbuli kushughulikia kesi huko badala ya kuwafanya wananchi watembee mwendo huo? (*Makofi*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, hakuna tatizo lolote ni suala la kuwasiliana na kuweza kupanga kwamba, Hakimu huyu wa Soni aende kutembelea Mahakama ya Mwanzo ya Bumbuli. Kwa hiyo, agizo hilo nimelipokea na nitalifanya kazi. (*Makofi*)

Na. 66

Sheria 40 za Tume ya Jaji Nyalali

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA aliuliza:-

Kwa kuwa Tume ya Jaji Nyalali ilipendekeza Sheria 40 zifanyiwe marekebisho au zifutwe.

- (a) Je, mpaka sasa wakati swali hili likiulizwa ni sheria ngapi ambazo zimeshafanyiwa marekebisho zikitajwa kwa majina?
- (b) Je, ni sheria ngapi ambazo tayari zimefutwa kabisa?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, mwaka 1998 katika Mkutano wa Bunge la Bajeti, Serikali ilitoa kauli yake kuhusu Sheria 40 ambazo Tume ya Nyalali ilizishughulikia na kupendekeza zifutwe au zifanyiwe marekebisho yanayofaa. Kati ya Sheria hizo 40, Sheria 29 zipo katika Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambazo zimekwisha shughulikiwa. Sheria nyingine 11 zipo chini ya Mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Aidha, Serikali imechapisha kijitabu kinachoorodhesha sheria zote 40 zilizoainishwa na Tume ya Nyalali. Katika kijitabu hicho, Serikali imeelezea hatua zote

zilizochukuliwa na Serikali kuhusu kila sheria iliyoinishwa na Tume ya Nyalali. Kijitabu hicho kimegawiwa kwa kila Mheshimiwa Mbunge na kuchapishwa katika magazeti mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ili kuokoa muda wa Bunge lako Tukufu kwa kuzitaja sheria hizo moja baada ya nyine na kwa kuzingatia Kanuni Namba 34(2)(x) ya Kanuni za Bunge la Tanzania, Toleo la 2004, ninamwomba Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, akirejee kitabu hicho ambacho kina kumbukumbu zote anazozihitaji. (*Makofii*)

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo: Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, je, hakuna sheria nyine tofauti na hizi zilizoainishwa na Tume ya Jaji Nyalali ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho na ikiwa zipo ni lini zitafanyiwa marekebisho au kufutwa kabisa?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, Sheria hizi 40 zilitokana na Tume Maalum ambayo ilikuwa inatazama mfumo wa kuendelea na chama kimoja ama mfumo wa vyama vingi, kwa hiyo, wakatoa mapendekezo hayo. Kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, sheria hizi mbalimbali zimefanyiwa kazi. Pia niseme tu kwamba, zipo sheria ambazo tunazifanyia kazi kwa maana ya kuzifanyia marekebisho na wakati muafaka ukifika basi tutaziwasilisha Bungeni. Pia naomba Waheshimiwa Wabunge, kama wanaona kwamba, kuna sheria ambazo zimepitwa na wakati basi waweze kuwasiliana na Wizara ili tuweze kufanya marekebisho yanayohusika. (*Makofii*)

Na. 67

Maombi ya Ujenzi wa Soko la Samaki Zanzibar

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipojibu swali langu Na. 81 katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge kuhusu ujenzi wa soko la kisasa kule Kilimani Kikwajuni, ilieleza kuwa maombi ya ujenzi wa soko hilo yaliwasilishwa kwa Serikali ya Japan na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitaendelea kufuutilia matokeo ya maombi hayo kupitia Wizara husika:-

- (a) Je, Wizara husika zinafuutilia vipi suala hilo na imefikia hatua gani hadi sasa?
- (b) Kwa kuwa jambo hilo ni la muda mrefu, je, ni sababu gani zinazofanya suala hilo lisipatiwe ufumbuzi kwa wakati huu?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, naomba nitoe maelezo mafupi ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyooleza wakati nikijibu swal la Bunge Na. 81 ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Japan inaendelea kuisaidia nchi yetu katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo inayohusu sekta ya uvuvi. Moja ya miradi inayoendelea sasa hivi chini ya ufadhili wa Serikali ya Japan ni ule wa ujenzi wa soko la samaki la Kirumba, Mwanza. Mradi huu ni moja ya maeneo kumi na 15 yaliyoainishwa na kupewa kipaumbele kwenye mradi wa Mpango Kamambe wa Kuendeleza Sekta ya Uvvi uliokamilika Juni, 2002.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ninaomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, kufuatia maombi ya ujenzi wa soko la samaki la Kirumba Mwanza na lile la Kilimani, Kikwajuni Zanzibar, yaliyowasilishwa kwa Serikali ya Japan, Serikali ya Japan imeridhia kufadhili ujenzi wa soko la samaki la Kirumba Mwanza. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Japan zimeweka saini Mkataba wa kuanza ujenzi wa soko la samaki Kirumba Jijini Mwanza. Ujenzi wa soko hilo unatarajiwa kukamilika ifikapo Machi, 2005.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu zinazofanya suala la ujenzi wa soko la samaki la kisasa la Kilimani, Kikwajuni lisipatiwe ufumbuzi wakati huu ziko mikononi mwa Serikali ya Japan ambayo hadi sasa hajatoa jibu lolote kuhusu ombi la kujenga soko hilo. Aidha, kama nilivyooleza kwenye kipengele (a) hapo juu, tukumbuke kuwa ni Mei, 2004 ambapo Serikali ya Japan imekabidhiwa eneo la ujenzi wa soko la samaki la Kirumba, Mwanza. Kwa hali hiyo, ni vigumu sasa hivi kwa Serikali ya Tanzania kuweka shinikizo kwa Serikali ya Japan kuhusu majibu ya maombi ya kusaidiwa katika ujenzi wa soko la Kilimani, Kikwajuni. Ninashauri Mheshimiwa Mbunge awe na subira kuhusu majibu ya maombi hayo.

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN: Mheshimiwa Spika, pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swal kama ifuatavyo:-

Je, isingekuwa vema kwa Serikali yetu kulifutilia kwa juhud zaidi suala hili, kwani suala hili la Kilimani ni la zamani zaidi kuliko la Kirumba? (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Serikali inafutilia na labda nieleze hapa kwa bahati nzuri wiki iliyopita nilionana na Balozi wa Japan ofisini kwangu na nilimwuliza suala hilo na nikamwomba kwa kweli atusaidie kwa upande wa Serikali yake. (*Makofi*)

Utunzaji wa Miti ya Asili

MHE. RUTH B. MSAFIRI aliuliza:-

Kwa kuwa miti ya asili inazidi kupungua kutokana na ukataji na ufyekaji unaofanywa na wauza kuni na wachoma mkaa na kwa kuwa kasi hiyo inatokana na soko kubwa la watumiaji wa kuni na mkaa vijiji na mijini na kwa kuwa kasi hiyo inatishia kumaliza miti ya asili ambayo ni adimu na huchukua muda mrefu kukua:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutunza miti ya asili ya Tanzania?
- (b) Je, Serikali imefanya tathmini kuona kiasi gani cha miti kinakatwa katika pori la Dodoma - Morogoro na hatua zipi zinachukuliwa kunusuru pori hilo?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuzingatia kuwa kasi ya ukataji miti ya asili kwa ajili ya mkaa na kuni inatishia kumaliza miti ya asili ambayo ni adimu na huchukua muda mrefu kukua, Serikali imetekeleza mikakati ifuatayo:-

(i) Tangu miaka ya 1960 hadi sasa mashamba 16 ya miti yameanzishwa ambapo miti ya kigeni imayokomaa haraka imepandwa kwa lengo la kutoa malighafi ya miti kwa viwanda vya mbaa kwa matumizi ya ndani na nje ya nchi, nguzo, kuni na kupunguza kasi ya kutegemea misitu ya asili kama chanzo cha malighafi ya miti;

(ii) Mheshimiwa Spika, Serikali inahamasisha wananchi waanzishe misitu yao wenyewe na kushiriki katika usimamizi wa misitu ya Serikali. Kwa mfano, hadi Juni, 2003 jumla ya misitu ya vijiji na ya jamii 957 ilikuwa imeanzishwa katika Mikoa ya Arusha, Iringa, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Morogoro, Mwanza, Pwani, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga. Aidha, wananchi katika vijiji 525 katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Mbeya, Mtwara, Morogoro, Mwanza, Pwani, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga, wanashirikishwa katika usimamizi wa misitu 37 ya Serikali. Juhudi za uhamasishaji zinaendelea; na

(iii) Mheshimiwa Spika, Serikali imewaondoa wavamizi katika misitu ya *Ilomero Hill, Igombe River* (Nzega), Mwakalundi, Goweko na *Igombe River* huko Nzega katika Mkoa wa Tabora, Biharamulo katika Mkoa wa Kagera, Uyovu na Runzewe katika Mkoa wa Shinyanga, *Livingstone* na Irenga katika Mkoa wa Mbeya na katika misitu ya Kazimzumbwi na Masanganya katika Mkoa wa Pwani. Sambamba na zoezi la

kuwaondoa wavamizi, Serikali imeimarisha doria katika misitu yake kwa kuipatia vyombo vyta usafiri Wilaya za Kilwa, Kigoma, Singida na Kilosa na mashamba ya miti ya Rondo, Mtibwa na Ukaguru. Aidha, mipaka ya misitu 13 ilipimwa upya mwaka 2002/2003 katika Wilaya za Muheza, Kilwa, Morogoro na Kisarawe kwa lengo la kuimarisha ulinzi.

(b) Mheshimiwa Spika, Pori la Dodoma - Morogoro ni eneo huria ambalo halijafanyiwa tathmini yoyote kujua miti inayokatwa. Eneo hilo halijafanyiwa tathmini kwa sababu matumizi yake ni mengi na yanabadilika wakati wowote. Matumizi hayo ni pamoja na kilimo, mkaa, kuni, nguzo za ujenzi na kuanzisha makazi ya watu. Ili kupunguza kasi ya uharibifu wa misitu katika eneo hilo, sera ya misitu inahimiza sekta binafsi, jumuiya za wananchi, Serikali za vijiji na Halmashauri za Wilaya kutenga, kuhifadhi, kumiliki na kusimamia raslimali ya misitu iliyoko kwenye eneo hilo kwa ajili ya kuinua uchumi na kuhifadhi mazingira. Serikali pia inatilia mkazo elimu na kuhifadhi mazingira na kuwashirikisha wananchi katika usimamizi na matumizi endelevu ya misitu hiyo.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini napenda kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa juhudhi inaendelezwa na Serikali ya kupanda miti ya kigeni ambayo hukomaa haraka kwa matumizi ya ndani na nje ya nchi, kwa matumizi kama ya nguzo, kuni na kadhalika.

Je, Serikali inazingatia vipi suala zima la miti ya asili ambayo hutumika katika kuponya magonjwa kama ya kisukari, pumu, malaria na magonjwa mengine ambayo miti ya kigeni haina sifa hiyo, je, miti hiyo ya asili imepewa umuhimu gani kutunzwa ili isiweze kuteketea katika kipindi kinachokuja? (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwamba kuna mashamba ya Serikali Kuu, kwa hiyo, hapa ndipo ambapo kwa kweli miti ya asili inapandwa kwa utaratibu maalum. Lakini pia kuna sehemu zile ambazo zinahifadhiwa na Halmashauri pamoja na Wilaya, nazo pia tunatilia mkazo.

Sheria ya Misitu ambayo ilipitishwa hapa Bungeni, inatoa nafasi kubwa sana kwa wananchi, vikundi, pamoja na vijiji na Serikali za Halmashauri kuweza kuhifadhi maeneo yao. Kwa hiyo, ningependa kwa kweli kutoa wito kwamba, wafanye hivyo na napenda kuwapongeza Wananchi wa Wilaya ya Kongwa kwamba tayari wameiomba Serikali itenye eneo hilo ili kuweza kuhifadhi maeneo ya miti.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamejibowi yote. Sasa matangazo ya vikao vyta siku ya leo. Kwanza ni kwa Kambi ya Upinzani, *Chief Whip* wa Kambi hiyo anawatangazia Wabunge wa Upinzani wote kwamba, leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi walitengewa, kutakuwa na kikao cha Kambi hiyo ya Upinzani. Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Dr. William Shija, anawatangazia Wajumbe kwamba, leo saa 5.00 asubuhi

kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi Na. 231, Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje.

Kamati nyingine, ni Kamati ya Hesabu za Serikali, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, mara baada ya maswali basi Kamati ikutane chumba Na. 227 ghorofa ya pili. Kamati ya tatu na ya mwisho ni Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, anawaomba Wajumbe wake wakutane saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi Na. 231.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo ningependa kutoa taarifa juu ya ratiba ya kesho, kwa sababu kesho ndiyo siku ya mwisho ya mjadala wa Bajeti, tumepanga kama ifuatavyo:-

Wamebaki Waheshimiwa Wabunge wachache sana kati ya 91 walioomba kuchangia ambao watamalizia kesho asubuhi. Baada ya hapo Naibu Waziri wa Fedha, atapewa nafasi kuanza kujibu, halafu atafuata Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, naye atatoa majibu yake. Watakapomaliza hao tutasitisha shughuli za Bunge kwa sababu tulipanga kwamba upigaji kura uwe kipindi cha jioni. Kwa hiyo, tutarejea saa 11.00 jioni kumsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa muda wa saa moja hivi. Mnamo saa 12.00 ndiyo tutaanza kazi ya kupiga kura ile ya kuita majina. Ninaona niwafahamishe mapema ili sote tuwepo katika muda unaotakiwa. Mwisho wa matangazo, tuendelee na *Order Paper*, Katibu.

KAULI ZA MAWAZIRI

Hali ya Utawala Bora na Vita Dhidi ya Rushwa Nchini Tanzania

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha Kauli ya Serikali, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumwombea Mheshimiwa Rais wetu apone haraka na kurejea nchini aendelee kusimamia majukumu yake ya Utawala Bora. (*Makofî*)

Pili, napenda kuchukua nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa ajali ambayo wameipata. Naomba na wao wapate subira na kupona haraka sana. Mwingine ni Mheshimiwa Estherina Kilasi, ambaye pia amepata ajali, tunamwombea apone haraka, nimeongea naye amenieleza kuwa ana maumivu. Pia napenda kumpa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na mzazi wao mpendwa na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na binti yake.

Mwisho, nampa pongezi Mheshimiwa Danhi Makanga na wananchi wa Bariadi Mashariki, kwa ushindi wa kishindo katika uchaguzi wa Bunge na Viti vya Madiwani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa niaba ya Serikali, nawasilisha Kauli ya Serikali juu ya Hali ya Utawala Bora na Vita Dhidi ya Rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika mjadala unaoendelea, Mkutano huu wa Kumi na Sita, juu ya hoja za Serikali zilizowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wameeleza kutoridhishwa kwao jinsi Serikali inavyosimamia maeneo kadhaa na dhamira ya Serikali kupiga vita rushwa. Kwa kutambua na kuheshimu nafasi na wajibu wa Kikatiba wa Bunge letu Tukufu, ikiwa ni pamoja na kuishauri na kuisimamia Serikali na vyombo vyake vyote, Serikali imeona ni vyema na wajibu kutoa maelezo mapema ili kuondoa mashaka juu ya uwajibikaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu ya Chama Cha Mapinduzi imekuwa ikitekeleza mikakati ya kuboresha utawala bora na vita dhidi ya rushwa kwa mafanikio. Serikali ya Tanzania inajitahidi sana kuendesha mambo yake na mambo ya umma kwa kuzingatia Sheria, uwazi na uwajibikaji wa hali ya juu. Serikali yetu imewekwa madarakani kidemokrasia kupitia uchaguzi ulio huru na haki. Tunaheshimu uhuru wa kusema na uhuru wa vyombo vyakoe habari.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha demokrasia, uhuru wa kusema unalindwa na Katiba yetu. Serikali yetu imekuwa ikishirikiana na vyombo vyakoe habari. Maafisa wa Habari wameajiriwa kila Wizara ili kurahisisha upatikanaji wa habari na kuhakikisha mahusiano mema kati ya Idara za Serikali na vyombo vyakoe habari. Sera ya Serikali ni kujibu mapema maswali ya vyombo vyakoe habari juu ya mambo yenye maslahi ya umma. Zaidi ya magazeti 400 yamesajiliwa katika nchi yetu. Vituo vyakoe Redio 30 vimesajiliwa na kuanzishwa. Vituo vyakoe *Television* 12 vimesajiliwa na orodha haijafungwa. Hii inaaminika ni rekodi katika Afrika. Aidha, Idara ya Mawasiliano imeanzhishwa Ikulu kurahisisha mawasiliano kati ya Ikulu na Umma.

Mheshimiwa Spika, madai ya rafiki yangu na mtani wangu Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, siyo ya kweli kwamba, tangu Tume ya Warioba hakuna kilichofanyika na kwamba taarifa yenye mapendekezo ya Tume ya Rais ya kuchunguza tatizo la rushwa katika nchi yetu imepuuzwa na kuwekwa pembeni. Tume ya Rais ya Kuchunguza Tatizo la Rushwa (*Presidential Commission of Inquiry Against Corruption*), ambayo inajulikana zaidi kama Tume ya Warioba, iliteuliwa tarehe 17 Januari, 1996 na kukamilisha kazi yake tarehe 7 Desemba, 1996. Tume ya Warioba ilibaini mianya ya rushwa iliyopelekea rushwa kuongezeka.

Aidha, Tume ya Warioba ilitoa mapendekezo juu ya namna bora ya kupambana na rushwa katika Wizara zote na Idara huru za Serikali. Katika mapendekezo hayo, juhudhi za kujenga uchumi imara zilitiliwa mkazo kama mbinu mojawapo ya kukabiliana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu, imeweka nguvu zaidi katika kujenga uchumi imara tukizingatia misingi ya uchumi wa soko huru. Mageuzi makubwa ya kiuchumi yamefanyika pamoja na kurekebisha na kubinafsisha mashirika ya umma ili

kujenga uchumi imara na endelevu. Mageuzi haya yamefanyika kwa ushirikiano mkubwa kati ya Serikali na Bunge letu hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Taifa wa kupambana na rushwa uliidhinishwa na Baraza la Mawaziri, Novemba, 1999 na ukasambazwa Wizara zote pamoja na mapendekezo ya Tume ya Warioba kwa utekelezaji. Aidha, mkakati huo ambao uliandaliwa kwa ushirikiano na wadau wote, umesambazwa Wilaya zote za nchi yetu kwa lugha ya Kiswahili. Katika Mkutano huu wa Kumi na Sita tutawagawia Waheshimiwa Wabunge kwa mara nyingine mkakati huo, taarifa za utekelezaji, mafanikio na matatizo katika vita dhidi ya rushwa kwa kipindi cha 1995 - 2001.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Taifa kupambana na rushwa na mpango wake, unatilia mkazouzuiaji wa vitendo vya rushwa kwa kuziba mianya ya rushwa. Kwa hiyo, mageuzi ya mfumo wa uendeshaji asasi za umma na msisitizo wa elimu kwa umma katika kupambana na rushwa vimepewa kipaumbele kwa kuzingatia kwamba, masuala ya Utawala Bora ni mtambuka (*Cross Cutting*). Mkazo umewekwa pia katika ushirikishwaji na vitendo sio maneno matupu.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Uratibu wa Programu ya Utawala Bora kimeanzishwa Ikulu. Kitengo hiki tunakisimamia tukisaidiwa na Katibu Mkuu Kiongozi, ambaye pia ndiye Mkuu wa Utumishi wa Umma. Katika ngazi ya Wizara imeundwa Kamati ambayo inasimamia utekelezaji wa mpango dhidi ya rushwa (*Inter Ministerial Committee*). Asasi za Serikali zinazoshirikana na Taasisi ya Kuzuia Rushwa kwa karibu sana ni Idara ya Usalama wa Taifa, Jeshi la Polisi, Mkemia Mkuu wa Serikali, Idara ya Uhamiaji, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Kitengo cha Ukaguzi wa Maadili katika Idara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Taasisi hii ya Kuzuia Rushwa inaendelea kuimarishwa kwa sababu vita dhidi ya rushwa ni ya kudumu. Watumishi wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa wameongezwa kutoka 142, mwaka 1995 Serikali ya Awamu ya Tatu ilipoingia madarakani na kufikia 714 sasa. Watumishi hawa kwa ajili ya upeletezi wamehitimu katika fani za Sheria, Uhandisi, Uchumi, Uhasibu, Elimu yaani Waalimu, Waandishi wa Habari na Utawala, katika viwango vya digri moja hadi tatu na *Diploma* za juu.

Mwaka 1995 zilikuwepo Ofisi saba tu zilizoko Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Tabora, Mwanza, Dodoma na Makao Makuu Dar es Salaam zikisimamia wastani wa mikoa mitatu hadi minne katika Kanda hizo. Tangu mwaka 1999 Taasisi ya Kuzuia Rushwa imefungua Ofisi katika Mikoa yote 21 Tanzania Bara na imefungua Ofisi katika Wilaya zote nchini isipokuwa Wilaya sita tu ambazo nazo Ofisi zitafunguliwa hivi karibuni. Bajeti ya Taasisi ya Kuzuia Rushwa imekuwa ikiongezwa tangu 1995 toka shilingi 191.7 milioni katika mwaka wa fedha 1995/96 kufikia shilingi bilioni 6.2 mwaka wa fedha 2003/2004. Mwaka wa fedha ujao tumeomba shilingi bilioni 8.642 na wafadhili kwa kutambua jitihada ambazo Serikali yetu imeweka katika kukabiliana na

tatizo la rushwa, wameahidi kutoa shilingi bilioni 29.625 kwa kutambua juhudhi za Serikali. Waliahidi watatoa mchango huo.

Mheshimiwa Spika, rafiki yangu, mtani wangu Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, jana alisema kuongezeka kwa bajeti ni ushahidi wa kuongezeka kwa rushwa. Mheshimiwa Mbunge alishauri fedha zihamishiwe kwingine kama rushwa imepungua. Waheshimiwa Wabunge, kuongezeka kwa bajeti ya Taasisi ya Kuzuia Rushwa ni ushahidi wa dhamira thabiti ya Serikali kupambana na rushwa na wananchi wanafurahia Taasisi ya Kuzuia Rushwa kusogezwa Vijijini. Wafadhili wanahestimu hili na kuahidi mabilioni ya shilingi zaidi. Mkakati wa dunia ni kuongeza nguvu katika vita dhidi ya rushwa. Hakuna nchi duniani isiyokuwa na tatizo la rushwa, hata Marekani bado wanapambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, tangu Januari, 2003 hadi sasa kuna kesi 125 zinaendelea Mahakamani, kesi mpya zikiwa 51. Katika kipindi hiki kesi 9 zimekwisha na Watuhumiwa wamewekwa hatiani kwa kufungwa. Kesi 28 ziliondolewa na rufaa 18 zikafunguliwa. Katika kipindi hicho Taasisi imepokea malalamiko 2,285 nchi nzima. Wananchi wana imani na *PCB* na wanatoa ushirikiano kwa sababu *PCB* iko karibu na wananchi. Mwaka wa fedha ujao Wilaya zote zitakuwa na Ofisi za Taasisi za Kuzuia Rushwa na hii inatarajiwa itasaidia kukabiliana na rushwa ya kisiasa ambayo imeanza kulalamikiwa kabla hata uchaguzi haujafikiwa, ikiwa ni pamoja na Uchaguzi Mkuu mwaka kesho. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Utumishi iliyopitishwa na Bunge hili imewevesha kuongeza ufanisi kwa kuwa na Tume moja ya Utumishi wa Umma. Kanuni za Utumishi zimetungwa chini ya Sheria mpya na kusambazwa Mikoa yote. Ajira na kupandishwa vyeo ni lazima kufanyika kwa ushindani na uwazi. Nafasi zilizo wazi lazima zitangazwe na kujazwa kwa sifa, sio kujuana. Utekelezaji wa Kanuni hizi unaendelea vizuri na malalamiko kama yapo kuna utaratibu wa kuyapokea na kuyashughulikia.

Mheshimiwa Spika, eneo la usimamizi wa fedha za umma kwa kiwango kikubwa limeboreshwa na Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001. Chini ya Sheria hiyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali amepewa madaraka makubwa kutekeleza majukumu yake. Aidha, chini ya Sheria hii, Serikali imefanikiwa kudhibiti rushwa na matumizi mabaya ya fedha za umma. Maafisa Wahasibu lazima waheshimu bajeti ili kuepusha madeni yasiyo ya lazima. Mtandao wa kompyuta unatumika ili kudhibiti malipo hewa na kucheleta kwa malipo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sheria za Fedha za Umma vitabu vya mwongozo wa uhasibu na ukaguzi (*Accounting and Auditing Manual*), zimeandaliwa na kusambazwa katika Ofisi za Serikali. Wadau 2,100 wamepewa mafunzo kuilewa Sheria hiyo ya fedha za umma ya mwaka 2001. Wizara inagharamia mafunzo ya vijana 1,700 katika Vyuo vya Elimu ya Juu ili kuhakikisha uendelevu wa maadali ya udhibiti na ukaguzi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Manunuzi ya Mali za Umma ya mwaka 2001 imeanza kutekelezwa Julai, 2001 baada ya kuidhinishwa kwa Kanuni za utekelezaji wake Juni, 2002. Bodi ya Taifa ya Zabuni ilisambaza mwongozo juu ya utoaji wa tenda za ujenzi, ununuzi wa bidhaa na huduma. Wizara na Mashirika ya Umma walianza kuzitumia mwaka 2002. Mabadiliko makubwa yamefanyika kuiboresha Bodi ya Zabuni ya Taifa. Katibu Mtendaji mpya aliteuliwa Agosti, 2003. Wajumbe waliteuliwa Septemba, 2003 na Mwenyekiti aliteuliwa na Mheshimiwa Rais Februari, 2004. Mamlaka ya Rufaa juu ya Maamuzi ya Mali ya Umma (*Public Procurement Appeals Authority*), imeundwa na elimu kwa Maafisa wa Umma inaendelea ili kufanikisha utekelezaji bora wa Sheria hii muhimu. Ndani ya Serikali tunaamini kwa kushirikiana na Bunge tutafanikiwa kuwadhibiti watumishi ambao wanatumia mianya ambayo bado ipo kuleta ubadhirifu na rushwa.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali kupambana na rushwa ni dhahiri kutokana na mifano michache nilioitoa kuonyesha juhudzi za Serikali kudhibiti rushwa kubwa na ndogo kisayansi na kwa kuzingatia Sheria na Haki za Binadamu. Kwa kuwa vita dhidi ya rushwa inahusisha kila Wizara na kila mwananchi, Waheshimiwa Mawaziri watatoa taarifa ya mapambano dhidi ya rushwa katika maeneo yao kuitia hotuba zao za bajeti.

Mheshimiwa Spika, tatizo la rushwa ni la dunia nzima, lakini nashangaa sana ninaposikia kwamba, rushwa inaongezeka kuliko ilivyokuwa 1995. Tume ya Warioba ilibainisha rushwa pamoja na maeneo mengine katika kuandikisha watoto shule ya msingi. Tumefuta karo na michango yote ya shule za msingi. Tumefuta kodi ya maendeleo na ushuru wa kero. Sasa Waziri wa Fedha katika hotuba yake anapendekeza kufuta ada ya leseni za biashara zenyenye mauzo yasiyozidi shilingi milioni 20 kwa mwaka. Kweli hatua zote hizi hazipunguzi rushwa? (*Makofî*)

Biashara zenyenye mauzo yanayozidi shilingi milioni 20 kwa mwaka, ada ya leseni ni shilingi 20,000/= tu na leseni itolewe mara moja tu wakati biashara inapoanzishwa. Hapa nafasi ya mizengwe iko wapi? Mapato ya Serikali yamekuwa yakiongezeka na Mamlaka ya Mapato inasifiwa na wengi hata ndani ya Bunge hili. Idara ya Mahakama na Jeshi la Polisi wanadhibitiana, wachache wao ndani ya Mahakama na ndani ya Polisi wanawachafua wenzao.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mionganini mwa nchi ya kwanza zinazoongoza katika kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji katika Afrika. Wawekezaji wengi wamevutiwa kuja kuwekeza hapa kwetu kwa sababu kuna Utawala Bora na uchumi unakua. Uchumi ni vigumu kukua katika mazingira ya nchi ambayo rushwa imekithiri. Wengi tunakumbuka wosia wa Baba wa Taifa kwamba, rushwa ikikithiri mapato ya Serikali hayakusanywi. Mamlaka ya Mapato (*TRA*) imetekeleza mkakati wa kupambana na rushwa kwa nguvu zote na matunda tunayaona. (*Makofî*)

Kwa mfano, malengo ya *TRA* mwaka 2000/2001 yalikuwa shilingi bilioni 779,494. Lakini makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 843,763.9, ongezeko la asilimia 8.3. Mwaka wa fedha 2001/2002, lengo lilikuwa shilingi bilioni 930,545.4 lakini

makusanyo halisi yakawa shilingi bilioni 941,995.4. Mwaka wa fedha 2002/2003, lengo lilikuwa kukusanya shilingi trilioni 1 bilioni 71.6. Makusanyo halisi yakawa shilingi trilioni 1 bilioni 108,781.1. (*Makofi*)

Ikumbukwe Mamlaka ya Mapato ilikuwa inakusanya wastani wa shilingi bilioni 25 hadi bilioni 28 kwa mwezi mwaka 1995 wakati tulipoingia madarakani. Sasa inakusanya wastani wa shilingi bilioni 100 kwa mwezi. Huu ni ushahidi wa kuongezeka kwa uadilifu na uwajibikaji ambao ndiyo misingi ya Utawala Bora. Uboreshaji wa elimu, barabara na afya ni ushahidi kwamba tupo kwenye njia sahihi. Siyo kukuza uchumi tu bali pia kuendeleza nchi yetu na kuongeza fursa kwa wananchi kupambana na umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, napenda kulitaarifu Bunge letu Tukufu kwamba, wananchi wengi na Taasisi sizizokuwa za Kiserikali ndani na nje ya nchi, zinasifia juhudzi za kupambana na rushwa za Serikali ya Awamu ya Tatu ya CCM, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa. Utafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Mambo ya Uchumi na Kijamii (*Economic and Social Research Foundation*) na (*Front Against Corrupt Elements in Tanzania*) uliofanyika hivi karibuni, umeonyesha mafanikio katika mapambano dhidi ya rushwa na ripoti zimeshawasilishwa.

Taasisi ya Kimataifa (*Transparency International*), ambayo sisi mara nyingi tunasema vigezo vyake hatuafikiani navyo kwamba tunanyimwa *marks* inasema rushwa inashuka Tanzania. (*Makofi*)

Kwa hiyo, waliomwambia mtani wangu Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga kwamba, Tanzania ni nchi ya nne kwa rushwa katika Afrika, walimdaganya. Kwa mujibu wa Taarifa ya *Transparency International* ya mwaka 2003, Tanzania ni mionganini mwa nchi 20 za Afrika ambazo zinasemekana kwamba zinasimamia mambo yake kwa kuzingatia Utawala Bora. Tanzania imepewa nafasi ya 17 ikifuatiwa na Zambia, Sudan na Zimbabwe. Uganda inashika nafasi ya 23, Kenya nafasi ya 27. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika orodha ya nchi za dunia nzima tumepewa nafasi ya 92. Nchi ya Nigeria ni ya 132 na ya mwisho ni Bangladesh ambayo imepewa nafasi ya 133. Tunaamini tunastahili nafasi nzuri zaidi kuliko takwimu za *Transparency International*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa 2004 imetolewa taarifa ya dunia kwa ajili ya Mkutano wa Uchumi wa Dunia (*World Economic Forum*), uliofanyika Geneva Switzerland mwaka huu wa 2004, juu ya hali ya ushindani wa kiuchumi katika dunia na katika Afrika na tatizo la rushwa kuelezwaa katika taarifa hiyo ambayo iko hapa. Ninazungumza kwa ushahidi,taarifa juu ya hali ya ushindani wa kiuchumi katika Afrika na tatizo la rushwa, *Corruption Sub-Index Rank* kati ya nchi 25 bora za Afrika, Tanzania ni ya 10. (*Makofi*)

Kati ya nchi 102 za dunia, Tanzania ni ya 73. Imani ya umma kwa wanasiwa Tanzania imepewa nafasi ya nne kati ya nchi 25 za Afrika. Uhuru wa Mahakama,

Tanzania imepewa nafasi ya sita kati ya 25 bora za Afrika. Upendeleo wa watumishi wa Serikali yaani kuvuruga Kanuni, Tanzania imepewa *marks* kwamba si zaidi kama nchi nyingine, kwa hiyo ni ya saba kati ya 25 bora za Afrika. Uwezo wa Serikali kupambana na umaskini tumepewa nafasi ya nne kati ya 25 na ni ya 28 kati ya nchi 102 za dunia. Hii ni kwa mujibu wa *Global Competitiveness Report*, ambayo nimeitoa hapa. Jambo lingine la kuvutia katika ushindani wa ukuaji wa uchumi (*Growth Competitiveness Index Rank*) kati ya nchi 25 za Afrika, Tanzania ni ya 9. Katika ya nchi 102 bora za dunia Tanzania ni ya 69. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, majirani na ndugu zetu wa Kenya na Uganda wanaweza kujifunza mengi kwetu. Kenya imepewa nafasi ya 21 kati ya nchi 25 za Afrika na nafasi ya 95 kati ya nchi 102 za dunia kuhusu rushwa. Uganda imepewa nafasi ya 19 sisi wa 10 kati ya nchi 25 za Afrika na nafasi ya 93 kati ya nchi 102 kuhusu rushwa. Taarifa ya mkutano mkuu wa dunia na utafiti huu umefanywa na wataalam nje ya Afrika. Kwa hiyo, katika ulimwengu wa sasa wa ushindani mkali na utandawazi, kuvutia wawekezaji na kulinda heshima ya nchi ni muhimu kutetea na kuenzi mafanikio ya nchi yako badala ya kuyabeza. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mlikuwa mnajiuliza kulikoni juu ya malalamiko katika magazeti na Mikutano ya Kimataifa juu ya kero ya rushwa, ukweli ndiyo huo, kuna ushindani. Ukikutana na wenzako kwenye Mkutano wa Kimataifa, tetea nchi yako, wao wanakuchafua, wakudidimize ili wawekezaji waende kwao. Takwimu zinaonyesha tuna uwezo wa kutembea kifua mbele. Ni haki kujivunia mafaniko yetu na kuongeza nguvu zaidi kukabiliana na tatizo la rushwa kwa sababu bado lipo na ndiyo maana tunaongeza bajeti na kuimarisha taasisi zetu na kuomba Bunge liendelee kutoa ushirikiano. Bado tunahitaji uvezeshwaji kifedha, teknolojia na nguvu watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika taarifa iliyoadaliwa na Wataalam wa Kimataifa, ambayo nimeieleza hapa, Senegal imewekwa nafasi ya 12 kati ya nchi 25 bora za Afrika na nafasi ya 78 kati ya nchi 102, lakini Marekani imeteua kwa msaada wa *Millenium Challenge Account* dunia ya sasa. Katika mazingira ya ushindani na ukuaji wa uchumi, fikiria katika uamuzi wa nchi ya Marekani kutoa msaada kupitia *Millenium Challenge Account*, Mozambique ambayo imewekwa nafasi ya 15 kati ya nchi 25 bora na nafasi ya 83 kati ya nchi 102 za dunia kuhusu rushwa, Madagasca nafasi ya 20 kati ya nchi 25 za Afrika na nchi ya 94 kati ya nchi 102 za dunia kuhusu rushwa pia na Ghana ambayo imepewa nafasi ya 13 kati ya nchi 25 za Afrika bora na nafasi ya 79 kati ya nchi 102 kuhusu rushwa. Hizi nchi ndizo ambazo Amerika imeziteua kuwa zinastahili kunufaika na *Millenium Challenge Account* na kuiacha Tanzania. Katika vigezo vyote vya Utawala Bora na mapambano dhidi ya rushwa tunazipita kwa mbali sana. (*Makofi*)

Lakini Tanzania tumeachwa na Wwapinzani wameanza kutumia uamuzi wa Marekani kutushambulia kwamba, utawala wetu una walakini katika kupambana na rushwa. Tunajua kwa nini Wamarekani wametunyima msaada huo na Serikali yetu imeshawaambia Serikali ya Marekani na mshangao wa dunia kwa nini Tanzania imeachwa. Hatutatoa sababu sasa hivi, mazungumzo bado yanaendelea. Lakini napenda kuwashakikishieni katika Siasa za Kimataifa za sasa hivi wanaofatilia siasa za Kimataifa

watajua sababu yake ni nini. Ni heshima yetu ya Tanzania kulinda uhuru wa nchi yetu.
(*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inashirikiana na nchi nyingine ndani na nje ya Bara la Afrika katika kupambana na rushwa. Tarehe 9 Desemba, 2003 nilipewa heshima na Serikali yetu kuweka sahihi kwa niaba ya nchi yetu, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Rushwa Mjini Merida Mexico. Aidha, Tanzania tumeweka saini Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kupambana na Rushwa wa mwaka 2003. Tunatarajia mwezi Octoba, Serikali itawasilisha maombi Bunge liweze kuridhia.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, kutokana na ushindani mkali wa kiuchumi, kuna mikakati ya kuchafuana kati ya nchi na nchi, vyama vya siasa na hata ya viongozi wa kisiasa, ndiyo sababu kwa kuzingatia sheria na haki za binadamu, tunaendelea kudai ushahidi. Watu wanaochafua jina la nchi yetu bila sababu hawatutendei haki.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kujali na kukemea rushwa. Ni wajibu wetu sote. Lengo la maelezo ninayoyatoa ni kuimarisha vita dhidi ya rushwa sio kufunga mjadala wa rushwa ndani na nje ya Bunge. Lakini tusiwape nafasi wenyewe lengo baya kutuchafua kwa sababu zao binafsi na kudai kwamba, Tanzania hakuna Utawala Bora. Matatizo ya rushwa tuliyonayo na mengineyo, tuna uwezo wa kuyatatua kwa heshima na haki. Bunge letu Tukufu kuititia Kamati zake linafanya kazi nzuri kuisimamia na kuishauri Serikali na hatutarajii mtu wa nje aingie hapa kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu ailinde Tanzania, naomba kuwasilisha.
(*Makofî*)

SPIKA: Tunaendelea. Orodha ya Waheshimiwa Wabunge watakaochangia leo kwenye hotuba zile mbili imeshawekwa kwenye ubao wa matangazo, lakini wanenye wa mwanzo ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba na Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga.

Tunaendelea, na *Order Paper*, Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2003, Mpango wa Maendeleo
wa Mwaka 2004/2005 na Makadirio ya Mapato na
Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005**

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. STEPHEN M. KAHUMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza asubuhi hii ili nami nichangie machache yaliyoachwa na wenzangu. Ninafurahi zaidi kuchangia mara baada ya taarifa ya Serikali,

iliyotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, kwa sababu katika mchango wangu vile vile nitazungumzia Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema mambo mengi, napenda niseme wazi kwamba, naunga mkono hoja zote mbili kwa sababu zimenyooka, nzuri na zinaelekea kutupeleka tunakotaka kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa ndugu zangu Wabunge, napenda kusema kwamba, unapokuwa umepanda chombo kikubwa cha safari kama meli au treni unashindwa kuelewa kama unakimbia, utadhani umekaa tu mpaka utazame *speed meter* utashangaa alalah kumbe tuko 120 hata gari unaliona kama linaserereka tu mmeCAA mnazungumza. Hiyo ndiyo hali ya maendeleo ya nchi. Tunaokuwa humu tunadhani hatuendi lakini kwa kweli tunakwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Waziri aliyekaa sasa hivi kwamba, mambo mazuri yapo, tusiogope na kero ndogo ikitokea tukadhani basi tumekufa, hapana. Tunakwenda vizuri tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapa pole ndugu zangu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na dada yake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na Mzee wetu, Mzee Omar Kigoda, Mungu awazidishie nguvu ya kuyakabili machungu haya. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, vile vile nimpe pongezi ndugu yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuliongoza jeshi lake la Madiwani ambalo alitoka nalo *UDP* na amelivusha. Tunamkaribisha Mheshimiwa Danhi Makanga katika jeshi tulivu la CCM. (*Makofi*)

Nimesema naziunga mkono hoja zote kwa sababu zifuatazo: Kwanza, ni kweli zinalenga kwenye shabaha ya Ilani ya Uchaguzi kama alivyobainisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Pili, zinalenga kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo. Tatu, zinalenga kwenye Mkakati wa Kupunguza Umaskini ingawa kwa uchumi wa kienyeji niliosoma nitajaribu kushauri kwa sababu unaweza kudhani unapunguza umaskini lakini kumbe unabeba bomu.

Labda nianeze moja kwa moja, kufuta leseni za biashara ndogo inaonekana wazi wazi kwamba, tunajaribu kufukuza umaskini lakini tusipoweka vizingiti tutakuwa tunazidisha umaskini kwa sababu vijana watakimbia vijiji na kwenda mijini kufanya biashara bila leseni, biashara anayofanya ni ya kuuza vibiriti. Mheshimiwa Waziri kama Mchumi anafahamu kwamba biashara ni *service industry*, haizalishi mali ila inatoa mfuko wa kulia kupeleka mfuko wa kushoto. Kama wazalishaji watahama kule vijiji kukiimbilia kuja kutembeza vibiriti kwa sababu hakuna leseni, basi tunakaribisha umaskini badala ya kuondoa umaskini. Vile vile marekebisho mapya katika kodi mbalimbali aliyorekebisha, nayakubali kwamba ni sahihi ingawa kitu kinachotia dosari kimesemwa sana na Wabunge hapa ni Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa. Tumekuwa

tukilalamika na kuishauri Serikali kwamba, Halmashauri zenyenye migodi zingepata mrabaha kutoka kwenye mgodi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimekuwa hapa tangu mwaka 1985 hata ndugu yangu, Msukuma mwenzangu, Mheshimiwa William Shija, aliwahi kushika Wizara hii ya Nishati na Madini, tulipokuwa tukisema tupate mrabaha naye alikuwa anakimbia. Sababu tunayoambiwa ni moja kwa sababu tuko wengi, balaa sana kuwa wengi. Mkisema mnaambiwa wameanza ukabila Wasukuma, ukabila kuomba mrabaha? (*Makofi/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Waambie bwana!

MHE. STEPHEN M. KAHUMBI: Mheshimiwa William Shija, aliogopa kuungana na sisi Wasukuma wenzake kwa sababu asije kuonekana anaongoza jeshi la ukabila, sasa leo tunaye. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu, Mheshimiwa Basil Mramba unaposema kwamba Jasi itolewe mrabaha, juzi Mbunge wa Kahama alisema hapa kwamba, mlisema kwa kupewa mrabaha italigawa Taifa, hii Jasi hailigawi Taifa? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa sijui Jasi inatoka wapi nilipoambiwa kuna Jasi, kuna nini nikauliza hivi inatoka wapi? Nikaambiwa inatoka Kilimanjaro na Tanga, ndio chokaa. Alaah kumbe huko? Sasa mimi nimeanza kuona tunagawiwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nilisema sana kuhusu mrabaha nikaambiwa kwamba, ardhi ya juu ndio mali yenu kule chini ni mali ya Taifa. Alaah! Sasa labda kwa sababu chokaa hii inatoka tu kwenye matumbawe ndio maana wanapewa watu wa Tanga! Nafikiri iko haja kwa ile Tume inayochunguza sheria hii kuangalia vizuri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Waziri amesema na nimesema nashukuru niseme baada ya ye ye kusema, amesema yanatengenezwa mazingira mazuri ya wawekezaji. Haya ndio mazingira mazuri ya wawekezaji kutunyima sisi mrabaha? Mazingira mazuri ya kuwapa likizo ya miaka mitano wawekezaji wasilipe chochote kwa nchi hii, ndio mazingira mazuri? Mazingira mazuri wanayopewa hawa watu ni ya kupata ardhi bure wakati mimi nikijenga kibanda changu Mjini Tabora nalipa kodi ya kiwanja wao ardhi eka kwa eka bure, ndio mazingira mazuri? Jamani hivi haya mazingira bora yakoje? Labda Waziri wa Utawala Bora atatueleza tena mazingira bora kwa msingi huo ni nini? (*Kicheko/Makofi*)

MBUNGE FULANI: Waambie bwana!

MHE. STEPHEN M. KAHUMBI: Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kama ningekuwa na uwezo wa kuagiza ningeagiza kwamba, mrabaha uwekwe kwenye madini yote pamoja na gesi ya Songsongo kwa sababu ni kitu walichopewa na Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilipewa majibu hapa kwamba, ooh kama wanavyoingiza wangepata hela nyingi sana Dar es Salaam. Niliwajibu nikawaambia Dar es Salaam bandari ile tumejenga wote hawakuijenga Wazaramo wa Dar es Salaam lakini dhahabu

ya Nzega hakuna aliyeiweka pale, Mungu tu alitupa sisi zawadi sasa hii zawadi tunaachiwa mavumbi ambayo hamkumruhusu Mheshimiwa Emmanuel Kipole, aimwage jana, mngemruhusu aimwage, ndio tunayopata sisi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hakuna sababu ya msingi ya kuhalalisha mrabaha kwa chokaa ukatunyima sisi wa dhahabu, hakuna sababu. Msitoke hapa mwende mkamjaze maneno Rais kwamba, wameanza ukabila wao, hatuna ukabila sisi tunataka haki tu. (*Kicheko/Makofi*)

MBUNGE FULANI: Sema baba.

MHE. STEPHEN M. KAHUMBI: Mheshimiwa Spika, kuhusu ufutwaji wa kodi, kodi zilizofutwa nafikiri zinafa lajini nafikiri rafiki yangu Mheshimiwa Basil Mramba alisahau tu au mimi sikuona kwenye kitabu, kuna bidhaa ambayo ni ya muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa hili. Katika Taifa hili tunasema elimu ni kitu cha msingi lakini tuna Taasisi ya Elimu, Baraza la Mitihani, Baraza la Elimu ya Juu na Baraza la Elimu ya Ufundu, hawa wanachapa *documents* nyingi sana kwa mfano, mitihani lakini wanatozwa kodi ya karatasi. Kama unamwachia mkulima apate mbolea bila kodi, kwa nini hawa watoto wetu walipe kodi ya karatasi zinazochapishiwa mitihani? Naomba Mheshimiwa Mramba, Baraza la Mitihani lisitozwe kodi ya karatasi, Taasisi ya Elimu inayoandaa mitaala na vitabu vya ziada na kiada pale Dar es Salaam, wapewe karatasi bila kodi. Baraza la Elimu ya Juu pale Dar es Salaam wanaandika *documents* nyingi sana kuhusu Elimu ya Juu, Baraza la Elimu ya Ufundu wana *documents* nyingi sana lakini wanaumia kwa kodi. Nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, tumewatembelea shida yao moja kubwa ni hiyo wanalamika kwamba tunatozwa kodi sana. (*Makofi*)

Katika ukurasa wa 25 umezungumzia matatizo ya kilimo na mpaka leo bado tunawaita wakulima wadogo wadogo. Mheshimiwa Basil Mramba ulikuwa Mkurugenzi wangu kule *SIDO*. Tulikaa pale Chuo cha Ufundu tukaondoa neno "vidogo", mimi na wewe na wenzetu tukasema tunaposema Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo tunaweka katika vichwa vya watu koroboi. Tukaligeuza jina tukasema ni Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo, hawa wakulima wadogo wadogo wataendelea kuwa wakulima wadogo wadogo kwa sababu tunapofikiria pembejeo tunafikiria mbolea, majembe ya mkono kama walivyosema wengine. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, juzi Waziri Mkuu alikuwa Tabora aliulizwa na mama mmoja mzee tu anashangaa tangu tumepata uhuru anaona magari tu yanaingia mbona matrektu hayaji? Mheshimiwa Sumaye hakujibu swali hilo. Leo mlajib. Mmi nilikuwepo wala sikumwambia yule mama aliyemwuliza Waziri Mkuu matrektu mbona hayaji? Mwingine amesema kwamba, ye ye angekuwa na uwezo angeyachoma Mashangingi kwa sababu yanakuja na yanabadilishwa kila mwaka lakini trektu haziji ingawa mnasema yataingia bila kodi, yako wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kumkumbusha Mheshimiwa Basil Mramba, tulipokuwa *SIDO* tuliisisitizia Serikali ipitishe Azimio la Kupendelea Mali ya Viwanda Vidogo. Leo ukifika kwenye maofisi yenu ninyi mnaagiza *furniture* kutoka Ulaya halafu

mnasema kuna *VETA* hapa, nani ameagiza viti kutoka *VETA*? Baba wa Taifa alituunga mkono *SIDO* kwa kusema kwamba, Serikali inunue vitu kutoka kwenye viwanda vidogo? Viwanda hivi vitakwenda wapi kama hatuviungi mkono, vitakuwa tu hata stuli ya kunywea chai unaagiza Ulaya! Ndugu zangu hebu turudi huko watu wanunue vifaa kutoka kwenye viwanda vidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza watu wa Ilala, akina Mheshimiwa Iddi Simba na Mstahiki Meya wa Ilala, wametoa barabara ya Lumumba wamewapa watu wanafanya biashara bila leseni. Waziri wa Fedha, unipeleke Uingereza kusomea *management* ya *small enterprises*, hiyo ndio njia yenyewe sio ile ya kufukuzana nao. Meya ya Ilala amefanya kazi nzuri, amewapa muda wanauza barabarani bila malipo. Kama inawezekana basi Serikali nyingine za Mitaa zingefuata mfano wa Ilala. Mimi nilifika pale nikawatazama nikawauliza mnasemaje wakasema oyeee! Kwa sababu badala ya kufukuzwa wamepewa barabara. Tunaacha barabara nusu wapite wenyewe magari nusu wafanyabiashara, siku mbili kwa wiki tunawapa fursa ya kuijendezea, fursa sawa kwa wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo labda ningezungumzia kidogo kwa sababu muda unakwenda ni kuhusu maghala kwa Waziri wa Ubinafsishaji. Kamati yetu ilitembelea Bohari za Madawa, jirani yake tu kuna Bohari Kuu ambayo sasa hivi hayafanyi kazi kutokana na sera yetu ya ununuzi. Sasa maghala yale yanakaa bure, kwa nini maghala haya wasipewe Bohari ya Madawa kwa sababu wanakodi maghala mbali wakati mengine yako tupu tu pale. Mheshimiwa wa Waziri wa Nchi, Offisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, anaweza siku moja kukurupuka akayabinafsisha wakati madawa pale yanakwenda kupangishwa nje. Tunaomba ikiwezekana maghala yale wapewe Bohari ya Madawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wenzangu wamesema sana na sio vizuri kurudiarudia, naomba tena niseme kwamba, Utawala Bora ni huo Waziri wa Fedha anasema atawapa nafasi *TRA*, nawapongeza sana wanafanya kazi. Jana niliongea na Mkuu wa *TRA* kuhusu Utawala Bora. Nakubali tulizungumza vizuri lakini napenda kuliweka katika rekodi, Mheshimiwa Basil Mramba, ndugu yangu, uwasaide wenzetu kwa mfano, watu wa Bima hawalipi Bima zilizoiva. Nimeletewa barua ya mteja wao ambaye Bima zake tatu zimeiva analalamika halipwi, nasikia na za Walimu ni nyingi tu, hiyo ni hatari pia nitakuletea shida zenyewe hapa kwa *record purposes*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. YUSSUF KOMBO JUMA: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa mawazo yangu kuhusiana na bajeti hizi mbili zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kusema lolote, napenda kutoa pongezi kwa Wizara zote mbili, kwa bajeti nzuri ambayo inaonyesha matumaini ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pole kwa wale wote waliopata misiba na pia napenda kuwapa pongezi waliopata mafanikio kwa shughuli moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja naomba nianze na suala la UKIMWI. Katika hotuba zetu mbili hizi nimezipitia vizuri nimeona sehemu ambayo imezungumzia suala hili la UKIMWI, lakini limezungumzwa kwa kiasi kidogo sana. Nilitegemea labda lingechukua nafasi kubwa kutokana na kwamba ndio tatizo ambalo linaweza kutufikisha sehemu tusiyoitarajia.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu siku hizi ukipita njiani katika safari zetu, inatisha sana kwa sababu utakuta ndugu zetu na hapa niwe mkweli zaidi, wanawake nguo wanazovaa zinatisha. Nasema ukweli hata kama wenyewe wanaweza kuliteea lakini huo ndio ukweli, nguo wanazovaa kwa kweli zinatisha. Hili linaweza kupelekea zile juhudhi zetu za kupunguza UKIMWI na mambo mengine yanayohusiana, zisifanikiwe kwa sababu macho hayana pazia. Utamkuta mtu amevaa kiasi kwamba, huwezi kuamini kama ni binadamu wa kawaida amevaa vitu vya ajabu na tuseme ukweli hivi ni vyanzo vinavyosababisha UKIMWI kuongezeka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuna baadhi ya vitu pale ameviongezea bei ili labda visitumike sana au viongeze uchumi wa Taifa. Lakini kwa mawazo yangu, nadhani kuna kitu kimoja amekiacha na kukiacha kwake ndio kinahamasisha hili tendo la ngono, nazo ni *condom*, kwa sababu *condom* zinauzwa Sh.100 na zimo tatu.

MBUNGE FULANI: Umejuaje?

MHE. YUSSUF KOMBO JUMA: Najua kwa sababu si tunaletewa mpaka hapa Bungeni, sisi sote tumeziona? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa kuuza *condom* kwa bei poa kabisa ina maana gani? Ni kuongeza au kuhamasisha tendo hili lifanyike. Nashauri kwamba, tungeangalia na hili tungeweka bei kiasi kwamba wale watoto wetu wa shule wa miaka 13, 14 washindwe kuhimili bei kama si hivyo basi tutabaki tunapiga kelele hapa UKIMWI, UKIMWI, lakini utazidi na hatujui tutafika wapi.

Mheshimiwa Spika, niende katika sehemu nyingine ambayo ni sehemu ya maendeleo ya jamii. Nimeangalia vile vitabu vikubwa, Kitabu cha Nne, *Vote 53*, ukurasa wa 75 na kile kingine katika sehemu inayoshughulikia vijana wetu yaani watoto, katika bajeti iliyopangwa nimepata wasiwasi sana kwa sababu sikuona fedha za ndani pale. Kuna shilingi milioni 30 katika maendeleo ya watoto tena za nje za ndani hakuna. Hili linanipa wasiwasi. Watoto hawa ndio tunaowategemea wawe viongozi wetu baadaye wajenge nchi hii. Kuwepo hapa sisi kupanga mambo yetu tunategemea kupanga lakini ni watoto hao ndio tunaowapangia ili waweze kuwa na hali nzuri ya maisha ili kupata viongozi wazuri hapo baadaye. Lakini inashangaza kuona kwamba, sisi wenyewe hatukuwajali watoto hao na tunategemea zaidi misaada kutoka nje. Hii haionyeshi ukweli au udhati wa sisi kutaka maendeleo au kupanga mambo yetu kwa usfanisi katika nchi hii.

Inaonekana kama bado tunafanya mambo ya mchezo, mchezo tu hasa kwa kuzingatia kwamba watoto ndio Taifa ambalo tunalitegemea baadaye.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna hii Wizara ya Maendeleo ya Vijana na Michezo, katika bajeti ya safari hii kuna fedha nyingi zimewekwa kuhusiana na ujenzi wa uwanja wa kisasa. Mimi kidogo nina wasiwasi tunapoweka fedha nyingi sana kwenye uwanja lakini hatukuweka hata shilingi kwa ajili ya vijana, sasa huu uwanja tumewakusudia akina nani? Kwa sababu tunapojenga uwanja wa kisasa kwa kutegemea watu wa Mataifa ya nje waje wafanye michezo hapa, sasa watakapokuja wakacheza peke yao sisi tutakuwa tumenufaika nini?

Mheshimiwa Spika, ninachoshauri na namwambia Waziri wa Fedha hapa kwanza ili tuwe na matumaini ya huo ujenzi wa uwanja wa kisasa basi kwanza tuwe na maandalizi mazuri na tuweke bajeti ya kutosha kuwaandaa vijana wetu ili hao watakapokuja waje kushindana na sio tunakuja kuwaangalia wao tu. Kama hatutafanya hivyo sijui tunachokifanya hapa kwa sababu utakuwa unafanya jambo kwa kumfurahisha mtu wa nje wakati mwenyewe hapa ndani umejisahau na hukujipangia mipango mizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo ya ujumla, naomba niende katika mambo ya muungano. Nimeangalia vizuri katika vitabu hivi nilivyovitaja mwanzo, nimeona hapa katika ukurasa wa 16, Kitabu cha Nne, Makadirio ya Fedha za Serikali kuna shilingi 421 milioni mwaka huu wa 2004/2005 na shilingi 454 milioni na shilingi 600 milioni na kuendelea hapo za mwaka 2003/2004. Hapa nina mashaka kidogo na naomba Waziri mhusika atueleze vizuri, mwaka 2003 fedha zilikuwa nyingi kuliko mwaka huu na wanasema fedha hizi ziliwekwa kwa ajili ya kujenga Ofisi na nyumba ya Makamu wa Rais kule Zanzibar. Kuna sehemu tumeona wameanza kujenga lakini mpaka sasa hivi umejengwa ukuta tu. Sina ushahidi wa Kipolisi lakini taarifa nilizonazo ni kwamba, huenda nyumba ile isijengwe kwa sababu ya kiusalama, inasemekana hivyo.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kuzungumza hapa kipindi kilichopita kwamba huwa tunapanga vitu halafu baadaye baada ya kupata gharama na kuwekeza kwa kiasi fulani tunasema ile sehemu haifai kwa sababu za kiusalama na mambo mengine. Mimi huwa najiuliza sana, hivi tunapofanya utafiti huwa hatuzingatii kwanza yale mambo muhimu ambayo baadaye tunakuja kusema ile sehemu haifai kwa sababu ya usalama. Sasa na hili atakapokuja Waziri kutujibu naomba anihakikishie kwamba kwanza hii nyumba pale pamoja na ofisi itajengwa na kama haitojengwa kwa nini zikatumika fedha nyingi za Serikali kwa sehemu ambayo haifai. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuongezea hapa inaonekana kwamba kuna kipindi fulani katika mchango wangu nilisema ile miradi ambayo inahusu Zanzibar huwa inakuwa migumu kutekelezwa na huu nao ni mfano mwingine. Labda naweza kubadilisha mawazo hayo atakapokuja Waziri anayehusika na hili na kunieleza kwamba labda ule ujenzi utajengwa na siyo kama vile ninavyofikiria mimi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea napenda kuchangia hapa kwamba kuhusiana na huu mchango wa Serikali wa 4.5. Nimesoma katika hotuba ya Waziri wa Fedha napo

pia nimepata matatizo kidogo kwa ile lugha aliyoitumia pale na naomba kunukuu ukurasa wa 39 wa kitabu cha Mheshimiwa Mramba katika mambo ya kipaumbele, kuna nane na tisa pale anasema: “Bajeti inaendelea kutenga asilimia 4.5 ya mapato yatokanayo na misaada (*grants*) isiyo ya miradi kwa ajili ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Utaratibu huu utaendelea hadi hapo mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha (*Joint Finance Commission*) yatakapopatikana”.

Mheshimiwa Spika, sasa hayo mapendekezo ya hiyo Tume yatakapopatikana kutoka wapi. Kwanza, ninavyoamini Tume iko hapa Tanzania na ina karibu ya mwaka na zaidi au miaka miwili sasa, lakini bado tunaambiwa hajakamilisha shughuli zake na Serikali ya Tanzania itaendelea kukusanya hizo fedha kwa mtindo ule ule wa zamani hadi hayo mawazo yatakapopatikana. Sasa mimi nina wasiwasi hapa hili jambo tunalifanya kama sio muhimu na ndiyo maana kila mara tunasema mpaka Tume itakapomaliza. Mimi nataka kuwaauliza hawa wahusika wa hili kwamba wapo *serious* na hili jambo au wanafanya mchezo? Nasema hivi kwa sababu haiwezekani, Watanzania wote tupo hapa, hakuna hata mmoja labda anayehitaji ndege ya kwenda kwenye Kamati au anayehitaji nauli sijui ya shilingi ngapi ya kufanya hili suala, ni kiasi cha kupanga, kukaa na kumaliza haya matatizo, lakini mpaka leo inaelezwa tu kwamba mpaka Tume itakapomaliza na itakapofanya shughuli zake. Sasa hili mimi linanipa wasiwasi na kuona kwamba niwe na hofu labda na yale mambo yaliyokubaliwa au tuliyokubaliana katika kulitekeleza hili.

Mheshimiwa Spika, sasa naiomba Wizara itueleze hasa hivi hii Kamati itamaliza lini shughuli zake na ipeleke ripoti inapotakiwa kwa sababu tukubali tu kwamba sasa tuna miaka arobaini ya Muungano, tunaendelea mbele, sasa haya mambo ambayo tunayaweka yanaweza kutufikisha mahali tusipopatarajia. Sasa naishauri Serikali kwa yale yote ambayo yamekuwa yanasemwa semwa si kwa kauli nzuri basi yazingatiwe na yatafutiwe jawabu muafaka kabla hajatokea ile sitafahamu ambayo hatuitarajii na wala hatupendi iwe hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme kwamba mimi nimeifurahia sana Bajeti hii. Kwanza inazingatia mambo yale yote ambayo kwa Mtanzania wa sasa aliyatarajia. Lakini hizi kasoro ndogo ndogo, ambazo nadhani tukiziachia au tukizifanyia mchezo zinaweza kutufikisha mahali ambapo siyo pazuri ziondolewe na Waziri achukulie uthabiti mambo haya ili hii nafasi kwa sababu nafasi ni dhamana na dhamana unatakiwa uitumikie kadri inavyotakiwa, sasa utakapokuwa unakwenda kinyume basi utakuwa hutimizi majukumu yako vizuri. Kwa hiyo, nawaomba Mawaziri wote wafanye shughuli zao kama inavyotakiwa ili tuondokane na yale matatizo madogo madogo ambayo tumekuwa tunayazungumza kila siku.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme tu naziunga mkono hoja hizi zote mbili na nashukuru sana. (*Makofi*)

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba hizi mbili

ambazo tumefikishiwa hapa za Bajeti. Kabla sijaendelea naomba niseme kwamba naunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nichukue nafasi hii kuwapongeza watoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Basil Mramba na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji Dr. Abdallah Kigoda na watendaji wao kwa ujumla kwa kuandaa hotuba nzuri ambazo kwa ukweli zina mwelekeo mzuri kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza pia Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi wake mkubwa na wa kishindo wa kulitetea Jimbo lake la Bariadi Mashariki hususan kwa kupitia Chama maarufu, Chama cha CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kuwapa pole Waheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Makongoro Nyerere kwa ajali walizopata,. Mwenyezi Mungu atawapa ahueni na waliopata majeraha basi nawaombea wapone haraka.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kutoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, uongozi wa Bunge, uongozi wa Chama na Serikali, ndugu, jamaa na marafiki na wapiga kura na wananchi kwa ujumla wao kwa jinsi walivyoshirikiana nasi na kutufariji kwa hali na mali katika msiba mkubwa wa mpendwa baba yetu, Mzee Omar Kigoda , ambaye alifariki na hatimaye kumpumzisha kule Handeni. Kwa niaba ya familia, nachukua nafasi hii kuwashukuru sana na tumwombee Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu baba yetu mpenzi, mahali pema peponi. *Amina*.

Mheshimiwa Spika, baada ya muhtasari huo, naomba sasa nichangie machache kuhusu hotuba hizi mbili. Kwanza, napongeza kabisa kama nilivyo sema hotuba zote mbili kwanza Bajeti hii inaonyesha kabisa kwamba inamsaidia mwananchi hasa yule wa kawaida na inaonyesha dira na mwelekezo mzuri lakini kuna maeneo machache tu, naomba na mimi niyagusie ili kuweza kuboresha na kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitazungumzia kuhusu suala la UKIMWI. Tunatambua wote, Serikali kwa kushirikiana na wananchi na asasi mbalimbali jinsi inavyojitahidi sana kupambana na janga hili la UKIMWI na ni ukweli usiopingika kwamba wengi sana wameathirika na tatizo hili si hapa Tanzania tu lakini dunia nzima.

Lakini napenda vile vile niipongeze Serikali kwa kuweza kutenga shilingi bilioni mbili ikisaidiana pamoja na program nyingine ili kuweza kuwapatia waathirika dawa za kurefusha maisha na hatimaye ziweze kupatikana bure.

Mheshimiwa Spika, lakini labda mimi ningeomba kitu kimoja. Hizi dawa zitakapopatikana kuwe na utaratibu mzuri ili ziweze kuwafikia walengwa hususan wananchi wengi ambao wako kule Vijijini na uwezo wao ni mdogo. Nasema hivi kwa sababu sasa hivi ukienda katika Miji mikubwa unakuta dawa hizi zinapatikana na wale

wenye uwezo wanaweza angalau kutoa ile shilingi arobaini elfu na kuwasaidia wale wachache ambao wameathirika. Lakini wengi walioko Vijiji bado hawana uwezo huo. Lakini si hilo tu kama tunavyofahamu nadhani Mawaziri na Serikali kwa ujumla labda pia tuangalie dawa hizi zikitolewa bure tusishau kuangalia madhara ya dawa hizi kwa sababu usugu unaweza kutokana kwa utumiaji holela wa dawa hizi.

Sasa ni vizuri basi kuwepo na maelezo mazuri ili zitakapofika kule Vijiji hawa wananchi watakaokuwa wanazitumia basi waweze kuzitumia ili kupunguza usugu. Vile vile ningeomba pia uwepo uwezekano wa kupatikana vipimo vikubwa basi *at least* katika kila Zone au katika kila Mkoa ambavyo vinaweza kumpima yule mwathirika atambulike kwamba kweli anaweza kutumia dawa au la, kwa sababu siyo wote wenye virusi wanahitaji kutumia dawa kwa wakati ule.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo naomba kugusia ni sehemu ya kilimo. Wote tunafahamu kwamba kilimo ni suala la msingi na Serikali iliahidi katika Bajeti iliyopita kwamba itasimamia kila Wilaya iwe na mazao mawili ya biashara. Lakini ...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Enhee, hiyo kengele ya kwangu!

MBUNGE FULANI: Muda unakwenda haraka?

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Enhe!

Mheshimiwa Spika, naona kana kwamba muda wangu haujamalizika!

SPIKA: Nadhani muda wako haujamalizika, Katibu alikosea.

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Mimi nafikiri hivyo hivyo.

SPIKA: Hazijakwisha dakika zako kumi, endelea. (*Makofî*)

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba sasa niende upande wa kilimo. Serikali kama ilivyosema kwamba ingesimamia kila Wilaya iweze kuwa na mazao mawili ya kibiashara lakini hili suala halikuweza kutekelezeka. Sababu zimetolewa lakini nasema kwamba kilimo bado ni sekta kiongozi. Kwa hiyo, sasa tunaiomba Serikali iendelee na ijitahidi sasa iweze kutimiza ahadi hii kwa sababu sasa inaonekana bila kutimiza ahadi hii bado Serikali yetu itakuwa omba omba na matatizo ya majanga ya njaa yanaweza kutufikia.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo naona kugusia ni muhimu ni kuhusu suala la uvuvi. Nchi yetu sehemu kubwa kabisa imepakana na bahari, lakini inaonyesha uvuvi katika maziwa hasa Ziwa Victoria ndio umetiliwa msisitizo sana na kusahau uvuvi bora katika bahari au maziwa mengine kama Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ushahidi mzuri ni kuwepo viwanda vya minofu kule Mwanza, kuwepo na ndege maalum ambayo inachukua ile minofu na vile vile sasa hivi kama tulivyosikia tu katika vyombo vya habari kwamba imefunguliwa maabara ya kisasa kabisa ambayo inaweza kufanya utafiti wa mazao ya samaki na utafiti wa *soil* na kadhalika.

Hapa mimi naipongeza sana Serikali lakini nilikuwa naomba kuwa uliza hawa Mawaziri ni mikakati gani sasa imewekwa ili uvuvi wa kisasa wa bahari kuu hii *deep sea* na majimafu katika mwambao wa Tanga, kwa mfano Pemba, Lindi, Mtwara, Mafia na kadhalika na sisi basi tuone ndege zinatua ili kuchukua minofu ya samaki toka katika viwanja vyetu vya ndege kule Tanga au Mtwara au Mafia na lini basi tutaona maabara za kisasa kwa ajili ya samaki wa maji chumvi ambao wanapatikana kwa wingi sana na viumbe vingine kutoka kule baharini. Kwa hiyo, pamoja na ile maabara nzuri basi tunaomba kwa upande wa uvuvi wa maji chumvi na hili nalo liangaliwe.

Suala lingine naomba nizungumzie kuhusu suala la kufutwa kwa leseni kwa wale wafanyabiashara ndogo ndogo. Nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali. Hii imesaidia sana ili wengi hasa waliopo Vijijini hasa akinamama ambao wengi wanajishirikisha katika biashara ndogo ndogo waweze kufanya biashara zao bila kupata hii bughudha. Lakini kitu ambacho nataka kusema ni kwamba ni vema katika hali hii tuwe waangalifu kwani isiwe sababu kubwa kwamba vijana wengi wakajipeleka katika biashara ndogo hizi na wakasahau masuala ya kilimo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, vile vile sasa hii isiwe sababu kwamba badala ya kuwa na vijana wanaofanya shughuli kubwa basi wakawa wanafanya biashara ndogo hivyo tutazalisha wachuuzi badala ya kuzalisha vijana ambao ni wazalishaji mali. Lakini katika hili pia nilikuwa naomba tuwape *support* kubwa sana shirika la pekee la Serikali la *SIDO* ambalo kwa asilimia kubwa lina mtandao mkubwa sana unaowafikia kule Vijijini ili waweze kuwasaidia vijana au wananchi ambao wana biashara hizi ndogo ndogo waweze kupata ufahamu mzuri wa kuweza kuendesha hizi biashara zao na vile vile iweze kuwasaidia kutoa elimu ya ujasiriamali kwani *SIDO* kama ilivyo na mtando mkubwa na wataalam, Serikali iweze kutoa *support* kubwa kwani hawa wanayo mafunzo ya jinsi gani ya kuanza biashara, kuweka biashara yao na jinsi gani ya kuboresha biashara na hivyo kuingia katika ushindani wa soko.

Mheshimiwa Spika, suala lingine labda ningezungumzia malipo ya wastaafu. Nazipongeza sana Serikali kwa sababu sasa hatimaye imeamua kuanza kuwalipa wale *pensioners pension* zao, wale ambao walipata kwa mikupuo. Lakini sijui kuna mantiki gani au sijui kuna sababu zipi kubwa sana ambazo zimesababisha kwamba hawa wastaafu wasubiri mpaka Januari mwakani kama ilivyotolewa taarifa.

Mheshimiwa Spika, wastaafu hawa walipokuwa wamelipwa mwanzo walikuwa wametegemea katika kipindi cha miaka kumi baada ya kustaafu kwao wawe labda wameshatoweka, wengi wawe wameshakufa. Lakini sasa ni kwamba watu huwa hatuna Mikataba na Mwenyezi Mungu na hawa watu wameendelea kuishi hata wengine zaidi ya miaka ishirini na ni vizuri kwamba Serikali wameliona hili. Lakini sasa kwa vile

wameamua kwamba wawalipe basi angalau katika maandalizi haya badala ya kungojea mpaka Januari wapunguze basi hajjambo hata kwa miezi mitatu wawe wameshaanza kulipwa ili sasa hata kama wale ambao wangekufa kipindi hicho japo waanze kupata pesa kidogo. Kwa hiyo, ningeishauri Serikali labda wangebunguza muda huu wa kuwasubirisha kwa sababu kama tunavyosema kwamba huwezi kujua lini binadamu anaweza kufariki.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ya mwisho ambayo naomba kuzungumzia ni kuhusu suala la kuondoa umaskini. Bajeti nzima imelenga katika kupunguza umaskini, mimi naipongeza sana kwa sababu kweli kabisa wananchi wetu kwa asilimia kubwa ni maskini wakiwemo wa Mijini na Vijiji. Sasa katika kupunguza umaskini kigezo kimojawapo ni kuwa na miundombinu. Kuna tatizo ambalo mimi bado linanizonga na nafikiri hapa sasa ni budi pia nilizungumzie. Kinachonishangaza ni kwamba Mkoa wa Tanga, kwa mfano, tuna shida ya barabara katika Wilaya zetu lakini ukiangalia Mkoa wa Tanga kuna barabara kubwa hii inayopita kutoka Dar es Salaam inayounganisha Mkoa wa Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha kwenda Nairobi na Tanga kwenda kwenda Mombasa. Hii ni barabara nzuri na Serikali inaihudumia, kwa kweli ina faida kubwa sana kwa sababu ya pato la Serikali na vile vile katika kutoa huduma lakini ukweli ni kwamba Mkoa wa Tanga bado Wilaya zake haziwezi kupitika hasa wakati wa mvua na kwa muda mrefu mimi nimeshaona kwamba bado kabisa zile Wilaya hazipitiki.

Lakini vilevile tukiangalia Tanga kwa mfano bado kuna Wilaya ambazo *potentially* zinatoa uchumi mkubwa sana. Kwa mfano, tukiangalia Wilaya ya Pangani, Wilaya hii ipo katika ukanda wa utalii kule Saadan lakini barabara ya kutoka Tanga Mjini kwenda Pangani wakati wa mvua kwa kweli lazima usome dua zote ndiyo uende kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Wilaya ya Handeni na Wilaya ya Kilindi ambayo ni Wilaya mpya *potentially* ardhi ina rutuba nzuri na sasa hivi kuna madini yamepatikana kule, kwa hiyo watu wengi tu wanakwenda kule kufanya biashara za kujipatia kipato lakini barabara zake kwa kweli ni mbovu, ni mbovu sana huwezi kwenda kule wakati wa mvua unajikuta kabisa wote mmekwama kule.

Sasa ningeomba Serikali basi pamoja na juhudu kubwa ambazo barabara nyingine zinatengenezwa lakini na hiyo waitupie macho angalau tupate barabara zinazowenza kupitika kwa wakati wote ili basi tuweze kuinua uchumi na hawa wananchi waliopo katika sehemu hizi waweze kushiriki katika sehemu za kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache nafikiri naomba nikomee hapo nikirudia tena kwamba nawapongeza sana Mawaziri wote wawili, napongeza Bajeti, napongeza Serikali kwa juhudu zake ambazo inachukua ili kuweza kuwasaidia wananchi kujikwamua katika masuala ya umaskini. Lakini vile vile basi haya matatizo mengine basi tushirikiane tuyaondoe ili isiwe kero na iweze kuipa sifa Serikali yetu ambayo inaongozwa chini ya Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Spika, narudia kusema kwamba naunga mkono hoja zote mbili na nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. (*Makofî*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kukushukuru wewe kwa njia ya kipekee kwa kunipa heshima hii kuwa mchangiaji mmojawapo kwa asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuitumia nafasi hii kumpungeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyothamini mchango wa wanawake katika Serikali yao kwa sababu juzi ameteua akinamama wawili kuwa Makatibu Tawala wa Mikoa. Hii anaonyesha ni jinsi gani anavyotekeleza uamuza wake kwa vitendo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile niendelee kumpungeza Mheshimiwa Rais pamoja na jeshi lake la Miavuli jinsi wanavyosimamia Ilani ya Uchaguzi kwa kutekeleza kwa vitendo, nadhani Bunge hili Tukufu wanafahamu kwa vitendo kabisa jinsi miradi ya maendeleo inavyoteklezwa katika maeneo yetu tulikotoka. Mimi binafsi nimetoka Mkoa wa Singida, nina mifano halisi, barabara sasa hivi zinamimiwa kwa kiwango cha lami, mawasiliano sasa hivi mpaka Kijiji, mpaka mama yangu sasa hivi anataka nimpelekee simu. Haya yote ni maendeleo ya Serikali ya CCM. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi hii nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella kwa heshima kubwa aliopata kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika. Hapa ametupa heshima kubwa Wabunge wa Bunge la Tanzania na wanawake wa Afrika kwa ujumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile niitumie nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi mkubwa alioupata wa kurudi nyumbani pamoja na Waheshimiwa Madiwani wote kwa kura walizopata za kishindo. Karibuni sana katika Serikali yenu ya CCM. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo naomba niitumie pia nafasi hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Waziri Dr. Kigoda na dada yake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba wa baba yao walioupati. Vile vile nitoe pole kwa Waheshimiwa Wabunge waliopata ajali nikianzia na Mheshimiwa Mama Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Makongoro Nyerere. Tunashukuru Mwenyezi Mungu ameponya nafsi zao wanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa nitumie nafasi hii kuzipungeza hoja zote mbili zilizo mbele yetu nikianzia na Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mramba pamoja na Mheshimiwa Dr. Kigoda, Makatibu Wakuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hoja zote mbili zilizo mbele yetu bila kumsahau mwanamke mwenzangu, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mama Blandina Nyoni, kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuandaa Bajeti zote mbili vizuri sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia naomba nitumie nafasi hii kabla sijasahau kuunga mkono kwa asilimia mia moja Bajeti hii iliyo mbele yetu kwani

imetuonyesha bayana jinsi inavyowajali wananchi walio chini ama wananchi wa kawaida kwa sababu mambo mengi yamewaletea unafuu wa maisha. Kwa kweli hali hii imetutia moyo sana sisi Waheshimiwa Wabunge lakini kwa kuwa tuna wajibu pia wa kuainisha yale maeneo machache ambayo labda yana mapungufu tunalazimika kuchangia lakini kwa ujumla Bajeti hii ni nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza kuchangia, naomba nianze na suala zima la ubadhirifu wa mali. Naipongeza Bajeti hii ni nzuri sana na imemlenga kabisa mwananchi kwa kumletea maendeleo lakini tabu inakuja kupatikana kwa watendaji wetu walioko huko Mikoani kwenye maeneo tulikotoka. Fedha zinapelekwa kwa malengo maalum ya kuleta maendeleo ya Mikoa yetu na Wilaya zetu lakini tatizo linakuja kutokea kwa hao watendaji ambao wanakiuka miiko ya fedha hizo zilikuwa zimelenga nini. Wengi wa watendaji wanashahau majukumu waliyopewa na Serikali hii, matokeo yake fedha wanazopata wanajaza safari za kikazi, hivi naomba Serikali leo iniambie hao watendaji wa ngazi za juu huwa mnawapangia safari nyingi kiasi gani mbona kila wiki Dar es Salaam, huko Dar es Salaam wanafuata nini kila wiki?

Mheshimiwa Spika, nadhani Serikali ingefika mahali ione umuhimu wa kuwapunguzia safari hawa watendaji ili fedha hizi ziweze kufanya kazi waliyoilenga. Siyo safari tu kuna tabia ya ujanja wa kalamu, ujanja wa kalamu umezidi kwa watendaji wetu. Watu sasa hivi wanacheza na kalamu kuainisha matumizi mbalimbali kinyume na matumizi halisi. Naomba Serikali ilione hili kwa karibu. Kwa kweli viongozi wenye dhamana ya wananchi tunapata shida ya kuhojiwa maswali na wananchi wetu kwa sababu wana macho wanaona na siyo hivyo tu unakuta mtendaji ameletewa fedha kwa ajili ya Akaunti A, anahamisha yeye mwenyewe kwa hiari yake kupeleka Akaunti B, bila hata kibali cha Serikali na Serikali inaona, hivi jamani ni halali? Halafu mtendaji huyo huyo mbadhirifu wa mali na fedha za umma anapobainika kwa viongozi wenye dhamana za watu anaondolewa kituo A anapelekwa kituo B, hivi hawa wa kituo B ndio wanamhitaji kiongozi wa aina hiyo? Naomba tuijilize. Naomba ifike mahali hawa watendaji wanaoonekana waziwazi kwamba hawawezi kutimiza majukumu ya Serikali wakae pemberi watupishe mbona tuna wasomi wengi tu shida iko wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani hilo Serikali itakuwa imelisikia na sasa naomba niongelee jambo lingine. Ambalo ni suala la mishahara, naipongeza sana Serikali inavyowathamini watendaji wanaofanya kazi kwenye idara za fedha wakiwemo *TRA*, *TANROADS* na maeneo mengine mengi wameamua kwa makusudi kuwatunishia mishahara yao ili kuwapunguzia kiu ya kuanza kuiibia Serikali. Huo ni uamuzi mzuri na imesaidia kwa kiasi kikubwa lakini Serikali imesahau kwamba *TRA* zipo nyingi. Hata Wakurugenzi wetu wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji wana-deal na fedha. Sasa hivi kuna miradi mbalimbali, utakuta Halmashauri moja ina miradi zaidi ya kumi yenye kuletewa mamilioni ya pesa lakini unakuta Wakurugenzi hawa mishahara yao ni midogo, waweka hazina mishahara yao ni midogo na watumishi wote wa idara hiyo ya fedha mishahara yao ni midogo, je, hawa watumishi hawana nyongo? Hata wao wana vishawishi kama wengine

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa hivi tumeshaona na wenyewe wanashika shika fedha nyingi, ili kuwapunguzia tamaa naiomba Serikali nao iwajali, ifike mahali basi iwaongezee mishahara yao ili waweze kutawala nafsi zao. Kwa kweli Halmashauri nyingi sasa hivi zinakuwa na ubadhirifu wa mali mimi niko kwenye Kamati ya *LAAC*, nimeona. Lakini nimekaa na kufikiria nimeona inatokana na mishahara yao midogo. Ninaamini na wenyewe wakipata mishahara minono kama maeneo mengine niliyoyataja watafika mahali watatunza mifuko hii vizuri kama wanavyofanya watendaji wengine wanaofanya kazi kwenye maeneo ya fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea hilo, naomba sasa nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuongelea suala zima la kupanda kwa sementi, bati na umeme. Mimi kabla sijaja Bungeni nimetokea kwenye ziara Mkoani kwangu. Nimefanya ziara Wilaya zote, nimekutana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Mheshimiwa Chiligati hapa nilikuwa kwake, nimepita Majimbo yote ya wenzangu na wote wameniunga mkono katika ziara yangu.

Swali nzito ambalo nilikuwa naulizwa kila mahali ni suala la ujenzi wa nyumba, wananchi wanasema pamoja na juhudini kubwa za kuwasaidia katika masuala ya kilimo hata wakalima wakapata fedha lakini lengo lao wakipata fedha vilevile wajenge nyumba bora. Sasa mkulima huyu hata akipata fedha nyingi, leo anauziwa mfuko mmoja wa sementi kwa shilingi 20,000 na bado inaendelea kupanda na bei za mabati ziko juu na umeme ndiyo mahitaji ya mwananchi wa kawaida umepanda bei, je, watanufaika nini hawa wananchi katika Serikali yao? Naiomba Serikali ifikirie upya katika suala nzima la bei hizi za sementi, mabati na suala la umeme ili wananchi hawa waweze kunufaika na Serikali yao. Wanapenda pia waishi katika nyumba bora. Kwa mtindo huu wa shilingi 20,000 kwa mfuko wa sementi watakaojenga ni akina Diana waliopewa heshima na wananchi hao, wenyewe hawatanufaika na Serikali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hilo. Sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la walimu. Hapo nyuma walimu walikuwa wanapata *Teaching Allowance* yaani Posho ya kufundishia. Lakini ilifika mahali posho hiyo ikafutwa, naomba Serikali itambue kwamba walimu hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu, wanafundisha wanafunzi wenyewe matatizo mbalimbali. Wapo wanafunzi wana upele, ugonjwa wa Kifua Kikuu na wana maradhi ya kuambukiza mengine lakini walimu yote hayo wanakabiliana nayo. Lakini bado walimu hawa hawajapewa chochote cha kuwasaidia katika hali waliyokuwa nayo ya mazingira magumu. Naomba posho ya kufundishia ya walimu irudishwe ili walimu waweze kunufaika na Serikali yao na waweze kufanya kazi ya kufundisha kwa moyo mmoja. Walimu sasa hivi ni wanyonge kwa sababu fedha wanayoipata haitoshi kulingana na kazi nyingi ama ugumu wa kazi wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba nizungumzie kuhusu suala hili la kufuta kodi kwa wafanyabiashara wadogo wadogo. Kwa hili naipongeza sana Serikali kwa sababu imemlenga kabisa yule mfanyabiashara mdogo anayehangaika, sasa tumtazame Afisa Biashara. Afisa Biashara kazi yake ilikuwa ni kudhibiti kodi za hawa wafanyabiashara wadogo wadogo ambao ndiyo hao wamefutiwa kodi. Hapa naiomba

Serikali iangalie hawa Maafisa Biashara sasa watakuwa na majukumu gani? Wawatazame upya kama majukumu yatakuwa yameisha basi wapewe haki zao wakae pembedi kuliko tukae na watu ambao wanapata mishahara bila kufanya kazi, kwa sababu kazi yao kubwa ilikuwa ni hii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala zima la hawa Maafisa Mipango. Maafisa Mipango ndiyo hawa wanaotegemewa na Halmashauri zetu katika kubuni vyanzo vya mapato. Sasa hivi Halmashauri zetu toka zimefutiwa kodi mbalimbali zimekuwa na mapato kidogo kwa sababu Maafisa Mipango wameshindwa kubuni vyanzo vingine vya mapato. Naiomba Serikali iwatazame hawa Maafisa Mipango iwape semina, wengi wao wameishapitwa na wakati, lazima Serikali iwabrashi. Wapate semina mbalimbali ili waweze kupata uwezo tena wa kubuni vyanzo vya mapato vingine ili Halmashauri zetu ziweze kuinua mapato vyake kuliko kutegemea Serikali Kuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu suala nzima la pensheni. Suala la pensheni wastaa fu wote wanazifuata fedha zao Hazina Dar es Salaam, watoke Songea, watoke Singida, watoke Bukoba hivi Serikali haioni kwamba hawa wastaa fu wanatoka mbali na ni gharama kubwa. Malipo ya pensheni yapelekeni Mikoani watu wakachukulie fedha zao huko, watagongwa na magari Dar es Salaam hawajui matumizi ya taa za barabarani. Siyo hivyo tu watakufa kwa *Pressure* kwa kushinda Hazina kutwa nzima wanafuutilia malipo yao ya pensheni. Wanakaa miezi sita hata mwaka hawajapata malipo yao, pelekeni huduma hii Mikoani ili wastaa fu wapunguze gharama na wapate fedha zao kiurahisi ama mpaka Wilayani huduma zifike ili wapate haki zao kiurahisi. Hii habari ya kusafiri kwenda Dar es Salaam watakufa kabla hawajapata fedha zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kusema suala la wastaa fu kurudishwa kwenye malipo ni nzuri sana, lakini wapo wastaa fu walio ko vijijini kabisa hata habari hizi hawana. Tumieni mbinu zenu kupeleka taarifa hizi na msije mkafunga mlango kwa watu kuleta majina yao waliostaafu wakapata fedha zao za mkupuo mapema ili na wengine wapate haki zao.

Mheshimiwa Spika, napenda nirudie tena naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

MHE. BERNARD K. MEMBE: Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Mramba iliyowasilishwa kwenye Bunge hili pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapa pole wote waliofiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze rafiki yangu Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kurejeshwa tena Bungeni kwa tiketi ya CCM. Nimeishaongea naye

nimemualika aje katika Jimbo la Mtama azungumze na watu wachache wa *UDP* ambao wala Chama chenyewe hawakijui vizuri nadhani atakuja kuwasaidia kuwaelewesha *UDP* ni nini?

Mheshimiwa Spika, na mimi naomba nichangie katika hotuba hii lakini niseme kwamba naiunga mkono kwa asilimia mia moja kuondoa suspension. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninayo maeneo manne tu ya kugusia na mimi katika uchangiaji wangu. La kwanza kabisa na wananchi wangu huwa nawaambia siku zote kuwa bajeti ni namna Serikali inavyopata fedha zake, halafu ni namna Serikali inavyozitumia fedha zake. Sasa nina jambo moja tu la kupendekeza kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha la wapi apate tena fedha za kuendesha Serikali. Amezungumzia suala la mfumo wa ushuru na pale kwenye ukurasa wa 54 amezungumzia suala la pombe ambazo zitatozwa ushuru. Sina kipingamizi na suala hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nilikuwa nataka nipendekeze kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atapenda kujipa muda na kufanya utafiti kwenye eneo hili la pombe. Mimi pombe za Mji na pombe zilizoko kwenye chupa hazinisumbui kwa ushuru wake. Lakini zipo pombe za kienyeji zilizoenea kote nchini kwenye sekta isiyo rasmi na sehemu hii ni nzuri kuiwekea kodi kwa sababu mbili.

Kwanza, ni pombe nyingi sana na wanywaji ni wengi mno. Lakini pili, wanywaji wengi ni nguvu kazi na wanatumia muda wao mwangi tangu asubuhi, mchana hadi jioni kunywa pombe, kutowasomesha watoto wao shule, kutokuzihudumia familia zao vizuri kwa sababu baada ya mavuno fedha nyingi hizi hutumika kwa kunywea pombe na mimi natoka kijijini naeleta kwamba pombe zinaathiri zake kiuchumi.

Badala ya kufanya kazi baadhi ya watu kweli wanatumia muda ule kunywa pombe zile. Kwa hiyo, ningomba eneo hili ingawa siyo rasmi la kisekta lifanyiwe utafiti ili kesho na kesho kutwa iwe pia ni sehemu ya kuchukulia fedha za kuendesha Serikali kwa kupunguza kasi ya unywaji wa pombe kwenye vijiji hasa wakati wa masaa ya kazi, lakini pia kuwawezesha watu wanaokunywa pombe hizo kutumia hizo fedha watakapoona vilabu vinafungwa vingine kuzitumia hizo fedha kwa maendeleo ya nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi nina maeneo kama matatu, manne. Lakini kabla sijaenda huko niipongeze pia Wizara kwa kazi nzuri na wenzangu wamezungumzia kuhusu pensheni. Kote ninakopita katika Jimbo langu wamefurahia kurudishwa kwanza kwa watu wale wastaafu ambao walikuwa wamepata pensheni zao kwa mkupuo wa miaka 12 kurudishwa tena katika orodha ya watu wa kulipwa pensheni lakini pia hata wale watu wa pensheni waliokuwa wanalipwa kiasi kisichozidi shilingi 10,000 kwa mwezi wamefurahia sana Serikali kuwalipa sasa kiwango cha shilingi 20,000 na kuendelea.

Lakini nadhani ni mapendekezo ya wengi kwamba ni vizuri hufanywe utaratibu kwa wastaafu hawa ambao ukiwaona wanatia huruma hakuna sababu tena ya

kuwaadhibu, kuwaacha miezi sita bila kuwalipa kiinua mgongo chao hatujawasaidia sana. Ningependekeza Wizara ya Fedha ichukue hatua madhubuti ya kuhakikisha kwamba kiasi hicho kidogo cha fedha kinachoweza kupatikana kwa wastaafu hao kwa mwezi basi wapewe walau kila miezi miwili, tunajua urasimu uliopo na matatizo yaliyopo, lakini kuwalipa kila baada ya miezi sita kwa kweli tunawazungusha kwenye madeni na hali zao bado zitaendelea kuwa mbaya na hawataweza kumudu maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, lipo eneo lingine ambalo siku zote tunalitilia mkazo na sisi Waheshimiwa Wabunge ndiyo tunahusika, nalo ni taarifa za Auditor General, nazungumzia matumizi ya fedha za Serikali. Tufike mahali sasa pa kusema *Auditor Generals Report* yaani taarifa za Wakaguzi wa Fedha zinazotolewa kila mwaka siyo tu kwamba zije Bungeni halafu zinatoka *PAC* zinarudi tena kwenye Mawizara na Serikali halafu inabakia kazi ya kuandikiana barua kati ya *Accounting Officers* na watu wengine. Mimi naona lazima twende hatua moja mbele ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na matumizi bora ya fedha za umma au fedha za Serikali. Vinatolewa vyeti kwa Wizara zote au Idara za Serikali na Mikoa wanaofanya vizuri, wanaofanya vibaya na wanaofanya vibaya zaidi.

Mheshimiwa Spika, nataka niishauri Serikali kwamba pale inapotokea kwamba *Accounting Officer* mara tatu anapata *No Opinion Certificate* yaani vyeti vya kuonyesha kuwa hawezi kueleza fedha zimetumikaje ni kwamba fedha zimetumika kiholela miaka mitatu mfululizo kwa nini asifukuzwe kazi. Mara tatu anafeli kutoa mahesabu sahihi ya namna fedha za umma zilivyotumika anakwenda kwenye *PAC* anarudishwa akafanye tena lakini bado Maafisa Wahasibu wanaendelea kufanya kazi katika nyadhifa hizo. Sana sana jambo labda mtu anabadilishwa kutoka kwenye kituo kimoja kwenda kwenye kituo kingine.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependekeza kwamba ufile wakati wa kutowaacha hawa watu kwa kutosimamia fedha za umma vizuri wana vyeti vya kuanguka kutokufanya kazi. Hawa napendekeza kwa kweli wafukuzwe kazi ili liwe somo kwa watu wengine na siku za mbele kwamba unapopewa dhamana ya kusimamia fedha za umma uvumilivu una kikomo chake. Haiwezekani uwe unaanguka kila mwaka kuna fedha ambazo unashindwa *kuzi-account for* na wewe unapata vile vyeti vyote na bado unashiba kitambi tu unakunywa pombe zako na unajihakikishia kazi katika Serikali tukomeshe hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nchi yetu ni changa, nchi yetu ni maskini takwimu zote tutakazozisoma za *Human Development Report* na Takwimu zote za Ulimwengu nchi yetu ni maskini ingawa isingetakiwa kuwa maskini. Mimi nasema sehemu moja inayotufanya tuwe maskini kwanza kabisa ni kwa sababu *growth* au ukuaji wa uchumi tunaousema ni *jobless growth* yaani ni ukuaji wa uchumi ambaa hauleti ajira kwa vijana wetu. Uchumi unakua kwa kigezo kimoja cha ukuaji wa uchumi ni *job creation* upatikanaji wa ajira kwa watu wetu. Huko vijijini hawajui suala la *4.9 percent increase*. Vijijini wanaposema uchumi unaongezeka ni pale wanapoona ajira inaongezeka. Tulipotaifisha Makampuni na Mashirika Binafsi lengo lilikuwa kwa kweli kwa imani

kwamba Sekta binafsi zitaleta ajira kwa vijana wetu lakini ziko sekta binafsi ambazo zilinunua Mashirika ya Umma kwa muda wa miaka minne mpaka sasa Mashirika hayo na viwanda hivyo havijafanya kazi na maana yake hawajaleta ajira, na maana yake uchumi wetu huwezi kukua, na maana yake uchumi katika kiwango cha asilimia 8 hakiwezi kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kutilia msisitizo na nitapata nafasi ya kuzungumza wakati wa Wizara zinazohusika kwamba kigezo kimoja cha ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote ile ni *job creation*. Ukuaji wa uchumi wowote ule ambaa hauleti ajira au *job growth* hatusaidii sana.

La mwisho, Mheshimiwa Spika, ningependa kwa dakika hizi za mwisho, niseme kwamba tunapopata hizi fedha na tukizitumia nyingi sana kwa ajili ya makongamano, kwa ajili ya semina, kwa ajili ya warsha, kwa ajili ya safari za ndani, semina nyingi sana zinazowafanya watendaji wetu wasiwepo maofisini na zinazofanya posho zitumike zaidi kila siku ningependa kuishauri Serikali angalau tufanye mikutano, warsha, semina na kongamano michache ambayo inafanyika katika nchi hii na fedha hizi badala yake zitumike katika kuelekezwa kwenye sekta ya uchumi kumbukeni wananchi kwamba katika trilioni moja iliyopangwa kwa ajili ya kifungu cha maendeleo bilioni 857 zinategemewa kutoka nje na bilioni 250 ndiyo zitatoka humu ndani ya nchi, tuna uhakika gani kwamba wenzetu wa nje watatusaidia hizo bilioni 857 za maendeleo. Kwa hiyo, Bajeti ya maendeleo ni ndogo na lazima tutumie hiki kidogo tulichonacho. Namna moja ya kutumia hiki kidogo tulichonacho ni kwa kupunguza mikutano, warsha, semina na hasa pale inapotokea kwamba tunafanya mikutano zaidi badala ya kufuatilia athari zake. Tunahitaji mikutano ya kazi siyo kazi ya mikutano.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie hilo kwamba tunahitaji mikutano ya kazi siyo kazi ya mikutano, tutaumiza wananchi wetu na tunahitaji kutumia hicho kidogo tulichonacho kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba tena nirudie kuunga mkono hoja hii na kusositiza kwamba mapato ya Serikali lazima yatumike vizuri wasiofanya kazi vizuri wawajibishwe, wanaopata vyeti visivyo kuwa *qualified* au *adverse or no opinion* wafukuzwe kazi hasa pale wanaporudia rudia kupata hivyo vyeti. La pili, ni kwamba tunapotenga fedha za maendeleo tutumie kidogo tulichonacho badala ya kutumia kiasi kikubwa cha nje kwa sababu Wahisani nao ni *un predictable* na fedha zao wanazitoa wakati ule tu ambapo Bajeti zao zinapita, na kwa taarifa yenu bajeti nyingi za Ulaya zinapitishwa mwezi Machi na mwezi Aprili ndiyo mwaka wa Fedha. Kwa hiyo maana yake kwa kasma hizi tulizozionomba sasa hivi za bilioni 857 kutoka nje za Wahisani lazima zitatoka kuanzia mwezi Aprili, Mei na Juni, mwakani haziwezi kutoka mwaka huu ndiyo wenzetu wanavyofanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningeomba nimalizie tena kwa kutoa nasaha zangu hizo na ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninajua nitapata nafasi tena ya kuchangia kwenye Wizara moja moja. Ahsante. (*Makofî*)

MHE. WILLIAM J. KUSILA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie mawazo kidogo kwenye hoja hizi mbili zilizopo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kabla ya kuanza mchango wangu niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole nyingi sana kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa msiba waliouupata. Lakini vilevile natoa pole zangu nyingi sana kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata matatizo mbalimbali katika kipindi hiki wakati Bunge hili linaendelea.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja zote mbili na nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wote wanaohusika na hoja hizi pamoja na watendaji wote wa Wizara husika kwa kutuletea hoja nzuri zilizoandaliwa vizuri. Nawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali na Waheshimiwa Wabunge wote nafikiri tunakubaliana katika jambo moja la msingi sana kwa ajili ya uchumi wa Taifa letu. Suala la kilimo ambalo wote tunakubaliana kwamba ndiyo mhimili wa uchumi wa Taifa letu na vilevile ndiyo mhimili wa maisha ya Watanzania walio wengi. Wote kwa kauli moja tunakubaliana. Lakini tatizo tu ni katika utekelezaji. Inapokuja kwenye utekelezaji basi kwa kweli azma, mipango yetu na hata utengaji wa rasilimali haviendani au havifanani na kauli ambazo wote tunazitoa na hili Waheshimiwa Wabunge wote wamelielezea na mimi napenda tu nisisitiza hilo kwamba kwa vile wote tunakubaliana katika suala hili nafikiri wakati umefika ambapo mipango yetu na ugawaji wa rasilimali zifanane na kauli tunazozitoa kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, wote tunasisitiza umuhimu wa kilimo lakini inapokuja kwenye utekelezaji, kwa mfano, tazama kwenye hiki kitabu cha dondo za bajeti unaona waziwazi kwamba katika sekta nyeti au sekta ambazo ni muhimu katika kupambana na umaskini ikiwemo Sekta ya kilimo unaona wazi kabisa kwamba sekta nyingine zote mgao wa fedha umeongezeka kati ya mwaka 2003/2004 na 2004/2005 isipokuwa Wizara ya Kilimo na Chakula peke yake ndiyo mgao wa fedha umepungua. Sasa hii haifanani na hayo tunayoyasema. Ingelikuwa vizuri basi angalau hata tukagawa sawasawa kwa baadhi ya Sekta lakini Wizara nyingine zote tumeziongezea fedha lakini Wizara ya Kilimo peke yake ndiyo fedha yake imepungua. Sasa hali kama hii haionyeshi basi kwamba tunafanya yale ambayo tunaamini, tunatenda kulingana na imani yetu. Kama kweli tunaamini na ndiyo ukweli wenyewe kwamba kilimo ndiyo kitakachotuwezesha kusonga mbele na kilimo ndiyo kitakachoondoa umaskini kwa wananchi wetu basi tuzingatie hilo katika mipango yetu na katika ugawaji wa rasilimali ndogo tuliyonayo ili kweli tuweze kusonga mbele. Kwa hiyo, mimi ningelipenda basi kuanzia hapa na kwenda mbele hili lijionyeshe katika mipango yetu yote na katika bajeti zetu zote zinazokuja ili tuweze kufanikiwa katika suala hili la kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha amezungumzia juu ya ongezeko la mauzo yetu ya nje ambayo yamesababishwa kwa kiasi kikubwa na bidhaa zisizo asilia. Ni kweli kwamba hivi sasa bidhaa ambazo si

asilia, mazao ya kilimo na bidhaa nyingine zimeanza kuwa na mchango mkubwa kabisa katika pato letu nchi za nje, na tumekuwa tunapata *frustrations* nyingi hasa kwa mazao yetu ya asilia kutokana na bei zake kushuka katika soko la dunia. Hivyo kuna umuhimu sasa tuelekeze nguvu zetu katika kuongeza uzalishaji wa mazao ambayo si asilia na vilevile uzalishaji wa bidhaa nyingine zote tunaziita siyo za asilia.

Mheshimiwa Spika, hapa Mkoani Dodoma na Mkoa jirani wa Singida na nafikiri na sehemu nyingine tu za kanda ya kati ya nchi hivi sasa naweza kusema kwamba tumepata mkombozi wa zao ambalo halikuwa muhimu sana huko nyuma, lakini sasa hivi linawapatia wananchi fedha nyingi sana nalo ni zao la ufuta. Sasa hivi zao hili kwa kweli limekuwa ni muhimu sana na lina bei nzuri tu katika soko na soko si tatizo. Hivi sasa ninavyozungumza kilo moja ya ufuta hapa Dodoma ni shilingi 1,000/=. Kwa hiyo gunia la kilo 100 ni laki moja na bei hii mpaka tutakapofika mwezi Desemba mwaka huu itapanda hadi kufikia shilingi 1,600/ kwa kilo au zaidi, ukilinganisha bei hii na mazao mengine ambayo tunayaenzi sana yale ya asilia inawezekana bei ya ufuta iko juu.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha zao la ufuta ni rahisi sana, na kwa sababu hiyo kilimo cha zao hili kimekuwa ni kivutio kikubwa sana kwa vijana, kwanza zao hili la ufuta linachukua muda mfupi sana kukomaa haizidi miezi minne tangu unapolipanda na kuvuna. Kwa hiyo, wananchi wanapata fedha haraka haraka tu. Kilimo chake si aghali na kila mtu anaweza kukimudu. Zao la ufuta halihitaji mbolea na halishambuliwi na wadudu kwa mfano ndege wala wanyama. Kwa hiyo, hakuna matumizi ya dawa na ukilipanda kitaalamu hata palizi halihitajiki. Kwa hiyo, sifa zote hizi zinafanya zao hili kuwa ni zao ambalo linahitaji mtaji kidogo sana kuweza kulilima na kwa sababu hiyo ndiyo nasema limekuwa ni kivutio sana kwa vijana wengi wamejiingiza katika kilimo cha zao hili. Bei yake kama nilivyosema katika soko bado ni nzuri sana kwa sababu wanalihitaji huko Ulaya ambapo watu wameanza kuogopa matumizi ya mafuta yanatokana na wanyama, kutokana na madhara yake na wanakimbilia matumizi ya mafuta ya mbegu, kwa hiyo linatakiwa sana.

Mheshimiwa Spika, nadhani ni wakati muafaka kukubaliana na Serikali kwamba tuelekeze raslimali nyingi katika kilimo cha zao hili na nina hakika linaweza kustawi katika maeneo mengi tu siyo Dodoma peke yake au Singida peke yake lakini nadhani linaweza kustawi katika maeneo mengi. Tulizalishe kwa wingi ili liweze kutoa mchango wake katika uchumi wetu. Tuchukue nafasi hii ya sasa ambapo bado linatakiwa sana katika soko la dunia, tuna *experience* ya mazao mengine kwamba kuna wakati bei ilikuwa nzuri sana na sasa bei siyo nzuri sana. Inawezekana na wengine wataingia katika kilimo cha ufuta baada ya muda na kwa hiyo bei itashuka kwenye soko la dunia. Kwa hiyo, mimi ninaomba sana tutumie nafasi hii ya sasa hivi ambapo soko bado ni nzuri na bei bado ni nzuri ili tuimarishe kilimo cha zao hili ambacho ni jepesi sana ili lichangie kama inavyofaa katika uchumi wa Taifa letu kabla ya mambo hayajabadilika. (*Makofi*)

Nadhani kama Serikali itaelewa na katika utaratibu huu ambao imeupanga wa zao moja la biashara na zao lingine la chakula sisi tunaomba hizi raslimali au fedha zilizotengwa kwa makusudi hayo basi ziletwe kwetu kwa ajili ya kilimo cha ufuta ili kila

inapowezekana tuwasaidie vijana kwa kuwakopesha ili waweze kupanua mashamba yao na kuzalisha zaidi. Nina mfano wa mkulima mmoja wa kawaida kabisa katika Jimbo langu ambaye msimu huu wa sasa hivi amepata milioni 21 kutokana na kilimo cha ufuta. Kwa kweli zao la ufuta linaweza kutukomboa watuletee hizo fedha ambazo wamezitenga kwa ajili ya kilimo cha zao la biashara ili tuimarishe kilimo cha zao la ufuta. Nina hakika linaweza kuleta mafanikio makubwa na mafanikio ya muda mfupi sana kwa sababu kama nilivyosema ni zao la muda mfupi sana linaweza kutusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, mimi yangu yalikuwa ni hayo, labda nimalizie tu kwa kuomba kwamba Mkoa wa Dodoma kama wote mnavyofahamu ardhi yetu ni nzuri haina tatizo ina rutuba katika sehemu nyingi hatuhitaji hata mbolea, lakini tatizo letu ni maji.

Sasa kama Serikali inaweza kutusaidia tukaweka mkakati wa kuchimba malambo madogo madogo katika maeneo mengi inaweza kutusaidia sana na nina hakika tunaweza kuzalisha chakula kingi tu tukaweza kusaidia sana hata tatizo la chakula katika Taifa. Nyote mnaona mahindi yanayotoka katika mkoa huu tukipata mvua nzuri na tutapata mazao mengine. Tunaweza kuzalisha mboga mboga kwa wingi sana, lakini tatizo letu ni maji. Ningiomba sana Serikali na hili tumekuwa tukilizungumzia sehemu nyingi tu. Naomba sana mtusaidie suala la malambo madogo madogo. Vijana waweze kulima mboga mboga wakati wa kiangazi na tuweze kuyatumia vile vile kwa ajili ya mifugo na matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, wakati mwagine tunawalaumu vijana kwamba hawafanyi kazi wanashinda vijiweni na kadhalika, lakini kwa kweli wakati mwagine hawana cha kufanya. Dodoma wakati wa kiangazi utafanya nini kijijini. Lakini mahali ambapo kuna maji utakuta vijana wanajishughulisha na kilimo cha mboga mboga mwaka mzima. Mifano mnaiona kwenye sehemu walizochimba watengenezaji wa barabara, maji yanajaa na vijana wanayatumia hayo maji vizuri tu kwa kilimo cha mbogamboga. Kwa hiyo, nina hakika kama tunaweza kuwa na malambo maeneo mengi basi tunaweza kuongeza sana uzalishaji wetu wa mazao ya chakula na vile vile hata kilimo cha mboga mboga.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kama nilivyoanza kwa kuunga mkono hoja zote mbili, nikiwa na matumaini kwamba mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasema hasa suala la kuwekeza katika kilimo litazingatiwa ili tuweze kwenda kwa kasi ambayo tunaitegemea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Bajeti ya mwaka 2004/2005.

Kabla sijatoa mchango wangu ningependa nami pia nishiriki katika kuwapa pole familia ya akina Kigoda kwa msiba wa kufiwa na baba yao na pia kumwombea Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, ambaye kwa sasa amelazwa hospitalini,

apate nafuu kwa ajali aliyoipata Kwa ufupi niseme kwamba naunga mkono sana Bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuipongeza Serikali kwa kufanya vizuri katika kukusanya mapato yake hasa katika kipindi hiki cha utawala wa awamu ya tatu. Nasema hivi kwa sababu sote tunajua kwamba makusanyo yaliyokuwa yanakusanywa na Serikali katika kipindi cha mwaka 1995 yalikuwa hayazidi shilingi bilioni 300. Lakini kwa sasa Serikali inakadiria kukusanya shilingi bilioni 1,700 hii ikiwa na maana kwamba ni ongezeko la karibu mara sita katika kipindi cha miaka minane iliyopita. Sasa mtu usiporidhika kwa kweli utakuwa hutendi haki kwa Serikali. *I mean* mtu yoyote anayependa kusema mambo ya kweli na anapenda haki ataipongeza sana Serikali kwa juhudhi ya kukusanya mapato ya nchi. (*Makofi*)

Lakini si kwamba Serikali inakusanya tu. Lakini pia inatumia vizuri. Wananchi wetu sasa wanaridhika sana katika mambo mengi yanayofanywa na Serikali. Tumeona programu nzuri kabisa ya MMEM ilivyoendeshwa katika nchi. Tumeona barabara zinavyotengenezwa vizuri katika nchi na huduma za afya wananchi wanaridhika nazo sana. Kwa hivi mambo haya ni lazima tuipongeze Serikali ili nayo ipate moyo kwamba inafanya vizuri.

Tunakoendelea kwamba tunayo hii programu ya *SEDEP* ambayo itakuwa ni kuboresha Elimu ya Sekondari katika nchi. Nilikuwa nashauri kwamba fedha za programu ya *SEDEP* zipelekwe pia katika Halmashauri ya Wilaya ili zikasimamiwe huko badala ya kusimamiwa na Wizara moja kwa moja. Nasema hivi kwa sababu mradi wa MMEM ambao kwa kiasi kikubwa ulisimamiwa na Halmashauri umefanya vizuri sana. Nadhani hata hii programu ya *SEDEP* ni vizuri ikasimamiwa na Halmashauri katika maeneo ambayo zinajengwa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, pia nimefurahi sana na Bajeti hii kwamba Serikali imefuta kodi ya *VAT* ya zao la chai. Zao hili naamini kabisa litatoa nafuu kubwa sana kwa wazalishaji wa zao hili kwa sababu ilikuwa ni mzigo mkubwa. Sisi Mufindi tunazalisha asilimia 67 ya chai yote ya Tanzania na wawekezaji wakubwa wamewekeza ulimaji wa zao la chai karibu hekta 40,000 kule Mufindi.

Lakini Serikali kupitia kodi ya *VAT* wakulima hawa wakubwa kwa mwaka walikuwa wanailipa Serikali karibu shilingi bilioni 3. Kwa hivi mchango kwa wakulima wa chai Mufindi wakulima wakubwa ni mchango mkubwa sana katika hii Serikali.

Lakini jambo ambalo tunapenda sisi kama wananchi wa Mufindi kutoa masikitiko yetu ni kwamba wakati Serikali inavuna pale shilingi bilioni 3 sisi Halmashauri ya Mufindi pale tunapewa shilingi milioni 30 kama *cess*. Sasa hii ni asilimia ngapi. Maana yake ukipiga hesabu unashindwa hata kupata jibu, maana yake hii wataalamu wa hesabu wanasema *is insignificant figure*. Yaani *is nearly negligible what we get* sisi kama Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na kile kinachopatikana kwa kodi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu gani. Sisi kwa sheria iliyopo sasa hivi kwamba kila chai inayotengenezwa tunalipwa *cess* ya chai iliyotengenezwa, *black tea*, shilingi 1.80 kwa kilo wakati bei ya chai iliyotengenezwa ni shilingi 1,250/=. Katika hizo Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi inalipwa shilingi 1.80. Serikali hii hii inasema Halmashauri mnaweza kupandisha *cess* mpaka 5%. Lakini sisi tumehangaika na hili kwa miaka minane (8). Hii *cess* ambayo tunalipwa kutokana na zao la chai ni 0.15. Yaani hata *1 percent* haifiki. Ukienda kwa TAMISEMI unaambiwa unajua hili zao la chai wanalima wakubwa. Sasa mwende taratibu, yaani twende taratibu.

Kwa miaka minane (8) huu utaratibu utakwenda mpaka lini? Naiomba Serikali *through this budget* ituidhinishie *cess* ya zao la chai Mufindi ili na sisi tuweze kupata angalau asilimia 2. Unajua hivi wanaangalia takwimu mbalimbali. Sasa Mufindi *per capita income* yao ni kubwa sana, kwa hivyo sio watu maskini. Nikiongelea Halmashauri moja iko Kusini kule. *Income* yao kwa mwaka *through* ushuru wa korosho ni bilion 1. Sisi *income* yetu ni Shilingi milioni 30, wanasema ile inayokusanya 1 bilioni ni maskini, sisi tunaopata 30 milioni ni matajiri wala hatutakiwi kusaidiwa sana. Hivi *logic* hii inapatikana wapi?

Mimi nashindwa kuelewa, yaani najaribu kufikiria haiingii hata kidogo akilini mwangu. Nasema ninyi mnajua hata huu mradi wa *TASAF* hamuwezi kuwemo kwa sababu hali yenu nzuri. Tunakusanya 30 milioni hao wanaokusanya 1 bilioni hawa lazima wasaidiwe tuwasaidie madarasa, sisi tuna madarasa mengi tu ya msingi wananchi wamejenga hatuwezi kuezeka kwa sababu Halmashauri haina fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi naamini si hilo tu ukienda kule Mufindi kuzuri sana. *Estate* zile zinapendeza kweli. Lakini nataka nikuthibitishie kwamba vijiji vyote vivilyo ndani ya kzile hakuna hata Kijiji kimoja chenye maji. Pamoja na vijiji vile wafanyakazi wake wanachangia Serikalini 3 bilioni kila mwaka, hakuna hata kijiji kimoja kina maji. Nadhani suala la kwamba *cess* ya chai haiwezi kupandishwa iwe shilingi 1/80 toka miaka ya 1980 mpaka leo nadhani ni makosa na kwanza sio utaratibu. Mimi nafikiri sasa hivi sheria zote za kodi zinaandikwa kwa *percent* kwa sababu thamani ya fedha inabadilika mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumze pia. Kwanza niishukuru Serikali kwamba imefanikiwa kubinafsisha Kiwanda cha *SPM Mgololo*. Kiwanda hiki kimetusumbua miaka mingi. Kwa kweli tuishukuru Serikali kwa juhudu kubwa. Lakini pia tumshukuru hata mwekezaji aliyeewekeza katika kiwanda kile. Lakini kiwanda kile sote tunajua bado kina matatizo makubwa sana ya kimazingira, bado ni tishio kwa uhai wa Taifa letu. Kwa hiyo, pamoja na kwamba mwekezaji amepewa kiwanda kile katika suala la mazingira ningependa Serikali iwe jirani na mwekezaji yule ili kweli tujiridhishe kwamba tishio la kimazingira, kemikali za sumu na hewa ambazo zilikuwepo hapo awali kwa sasa zinaondoka na jambo hili pia linahitaji msaada wa Serikali kwa sababu athari zitakapopatikana pale hazitakuwa za mwekezaji, zitakuwa ni athari za nchi. Kwa hiyo, ni vizuri nchi ikaona kwamba bado ina wajibu mkubwa juu ya hali iliyopo pale *SPM* sasa. Lakini Kiwanda kile kinahitaji ukarabati mkubwa na kinahitaji fedha nyingi ili kiweze kufanya kazi. Juhudi kubwa mwekezaji anafanya ya

kununua vifaa duniani kote kuhakikisha kwamba kiwanda kile kinafanya kazi. Kiwanda kile kilianza mwaka 1984 na sasa ni mwaka 2004 ni miaka 20.

Kwa takwimu ambazo Serikali inatuambia ni kwamba katika miaka yote 20 *SPM* haikutengeneza faida. Ndiyo maelezo ambayo tunaambiwa na Serikali. Sasa jambo ambalo mimi siko *comfortable* nalo ni kwamba Serikali inasema kwa miaka hiyo 20 mafao yao walipwe na huyu mwekezaji atakapowasha kiwanda. Sasa mimi napata shida, Serikali yenyewe iliendesha kile kiwanda kwa miaka 20 na haikupata faida sasa anayenunua mwekezaji, huyu mwekezaji atakarabati kiwanda, atakiwasha, atafanya biashara, atapata faida na atawalipa mafao hawa watumishi. Inanipa shida kidogo kuamini kwamba *statement* hii ya ukweli. (*Makofî*)

Watumishi hawa wamefanya kazi kwa uadilifu mkubwa sana katika kipindi cha karibu miaka 9 kwa kuitunza kiwanda kile. Sasa ni vizuri tukawa wakweli na tukawatendea haki.

Mimi nadhani ni namna fulani ya kuwatelekeza watumishi wale. Maana yake mtu kwanza unaona kile kiwanda hakijawashwa, unasema aah hiki kitakarabatiwa, kitawashwa, kitatengeneza karatasi na faida ya mwekezaji na halafu baadaye mtakuja kulipwa mafao. Sijui mimi naona hii, lakini kwa ustaarabu tu tuiambie Serikali lipeni mafao ya watumishi wa *SPM Mgololo*. Inabaki hii lugha.

Mimi nafikiri hakuna mtu atakayeaminu katika mazingira hayo kwamba mwekezaji yule kweli atajenga uwezo wa kuwalipa watumishi wale mafao. Kwa Serikali hata kama haina uwezo basi afadhali iseme tunatafuta uwezo lakini jukumu la kuwalipa watumishi wale ningependa kwa dhati kabisa na kwa hakika iendelee kubewa na Serikali yenyewe. (*Makofî*)

Maana *logic* inakwambia hivyo *no way*. Huna namna kwa sababu unawenza ukamwambia mtu kitu akawa anakuangalia tu, kwanza anakushanga Kwamba *are you serious* na unachokisema. Mwekezaji yule tunamwombea tu Mwenyezi Mungu kwanza apate kuwasha kiwanda kipate kuwaka kwa sababu kimekaa muda mrefu bila ya kufanya kazi.

Tunaomba Mwenyezi Mungu angalau karatasi ya awamu ya kwanza hii iweze kupatikana. Tunamwingiza mwekezaji huyu katika migogoro na wafanyakazi bila sababu. Hawezi kuwalipa kwa sababu uwezo hana. Kwa hivi atajikuta na migogoro mingi sana na wafanyakazi. Watu wamekaa miaka 20 na karibu muda wao wa kustaafu unafikia sasa.

Sasa kweli atawasha kiwanda *ata-operate* na *at the same time* atalipa wafanyakazi? Hata yale mafao ya lazima yaliyokuwepo *NSSF, PPF* Serikali ilikuwa hailipi pale.

Kwa hivi mimi nashauri kwamba ni vizuri mafao ya wafanyakazi wa *SPM* ilipe Serikali yenyewe. Hili ni vizuri kabisa Serikali ikachukua jukumu la kwenda pale *SPM Mgololo* ikazungumza na wafanyakazi wale ikatengeneza nao makubaliano ya namna nzuri ya kuwalipa watumishi wale mafao yao. Tunajua matatizo ya viwanda katika nchi. Matatizo makubwa ya gharama za umeme. Tumelizungumza jambo hili miaka mingi. Mimi sitegemei kama mwekezaji yule katika kipindi cha miaka 6, 7 ijayo itatengeneza faida. Siamini kabisa. Kwa hiyo bado nashauri Serikali ilipe watumishi wa *SPM Mgololo*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine dogo ambalo ningependa kulizungumzia nalo ni kuhusu kilimo. Kilimo ni maji. Sasa mimi sielewi kama nchi ina ukame hivi Waziri wa Kilimo anafanya nini. Suala hili mimi nalionka kwa wale ambao wamepata bahati ya kusafiri katika anga la Tanzania nchi yetu inageuka jangwa.

Sasa kama hatu-*address* ujangwa wa Tanzania haya matatizo ya kilimo tutapambana nayo miaka mingi sana. Kwa sababu mimi naamini Watanzania wanafanya kazi wanalima sana. Lakini kwa sababu ya matatizo ya mvua tunashindwa kuvuna, na matatizo ya mvua hatuwezi kuondokana nayo kama tunakata misitu kama tunavyofanya sasa. Mimi nadhani nchi inatakiwa sheria kubwa sasa juu ya uhifadhi wa misitu *that's the only way*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maana yake mimi nilikuwa nafikiria huyu Ndugu yangu Mheshimiwa Charles Keenja, hivi afanye nini sasa nchi yote jangwa. Mimi nasema kwa hali tuliyonayo ya mvua sasa hata ungetoa Bajeti yote ya Serikali ukiingiza katika kilimo hatuwezi kulipa. Tunapozungumzia umwagiliaji hakuna maana yake mabwawa yanataka mvua, mito inataka mvua hata kisima kinataka mvua. Kwa hivyo ukisema tuachane na mvua za kubahatisha twende kwenye mabwawa kama mvua hainyeshi mabwawa yanapata wapi maji.

Kwa hiyo, kwa namna yoyote hata tungesema tunaendelea hatutahitaji mvua tunajidanganya. Mvua ndiyo *key* maana maji ya mabwawa yanatoka katika mvua, maji ya mito yanatoka katika mvua, maji ya visima yanatoka katika mvua. Kwa hivyo kwanza lazima tujihakikishie kwamba nchi yetu ina-*create* mvua. Na tuweze ku-*create* mvua kama tunafyeka misitu. Hawa wakulima wetu ukielekea kule Kiteto unakuta mtu ana heka 1,000 katika eka 1,000 hakuna mti.

Tungekuwa na utaratibu kwamba ukilima eka 100 hakikisha kwamba eka zako 100 zote umezungushia miti ili kwamba hata kama mashamba yatakuwa makubwa mashamba yale yanakuwa *covered* na miti ili kukaribisha mvua. Nadhani tunayo kazi kubwa bado ya kufanya katika suala zima la kilimo. Lakini mimi nasema hakuna kilimo kitakachofanikiwa bila maji na maji ni mvua. Hivi vingine ni *shortcut* tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, pamoja na ile ya Waziri Abdallah Kigoda, Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji.

Kabla ya yote ningetaka nami kutoa pole sana kwa Mheshimiwa Kigoda, Waziri pamoja na Mheshimiwa Aisha Kigoda kwa kufiwa na mzazi wao. Pia napenda kutoa pole sana kwa Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na binti yake ambaye pia ni rafiki wa binti yangu. Pia natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge ambao walipata ajali wakati wakija Bungeni, Mheshimiwa Mama Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Estherine Kilasi na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuirudishia heshima CCM katika jimbo la Bariadi, baada ya kushinda kwa kishindo uchaguzi mdogo wa hivi karibuni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia ningetaka kusema kwamba mimi naunga hoja zote mbili mkono kwa asilimia mia moja. Pia natoa pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri wahusika na Bajeti hizi mbili pia kwa wataalamu wao wote kwa hotuba nzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tatizo haliko kwenye utengenezaji wa hotuba na haliko kwenye Bajeti. Kwa mtazamo wangu mimi tatizo kubwa liko hasa baada ya kupitisha Bajeti panapita muda mrefu kabla fedha hazijapatikana kwa ajili ya maendeleo mbalimbali. Matokeo ni kwamba kuna miradi mingi Wilayani pamoja na miradi ya kitaifa ambayo huchelewa kuanza, hasa miradi ya ujenzi wa barabara.

Kwa mfano barabara mojawapo ya kutoka Nangurukuru kwenda Liwale mwaka jana fedha zimepelekwa wakati mvua inanyesha. Matokeo Makandarasi ameshindwa kukamilisha kazi hiyo na hatujui nini kilichotendeka kwa fedha hizo ambazo zilikuwa zimekusudiwa kufanya kazi hizo. Hivyo ndivyo ilivyo nchini kote. Ninashauri Bajeti inapopitishwa basi mara moja fedha zipelekwe katika maeneo husika ili ziweze kufanya kazi zilizokusudiwa. (*Makofî*)

Mwaka jana 2003 tulifuta kodi au vyanzo vya kodi katika Halmashauri zetu. Matokeo yake ni kwamba Halmashauri hizi zimeshindwa kufanya kazi zake vizuri kwa vile fedha ambazo zilitarajiwa kutoka Serikalini zilichukua muda mrefu kufika katika Halmashauri zetu. Hii ilikwamisha sana baadhi ya miradi ya maendeleo katika Wilaya zetu.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa kuwapunguzia wafanyabiashara wadogo wadogo kodi au kuwafutia kabisa kodi ya leseni.

Lakini jambo muhimu hapo sio kufuta tu, jambo muhimu kwa Serikali ni kufuatilia baada ya matamko yake. Imewahi kutokea na inaendelea kutokea sehemu zingine kwamba baada ya kufuta kodi unakuta watekelezaji wanakuwa na kigugumizi sana kiasi cha kwamba hata wafanyabiashara huwa wanashangaa kodi iliyofutwa ni ipi.

Kwa hiyo naomba baada ya kutoa tamko la Serikali kwamba kodi zimefutwa au kodi ya leseni imepunguzwa vitu kama hivi naomba Serikali ifuatilie kwa watendaji wake tafsiri iwe ile ile ili wafanyabiashara hawa waweze kunufaika na hatimaye wananchi husika watanufaika. Vinginevyo wafanyabiashara hawa wadogo wadogo kama tutazidi kuwabughudhi matokeo yake watakwenda kuuza bhangi ambayo haina kodi. Sasa kwa nini tulete mwanya wa aina hiyo.

Naomba Mheshimiwa Waziri ufuatilie hili kikamilifu kwa watekelezaji wako wanaohusu utozaji wa kodi ili watekeleze kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Serikali isitishe kwa muda ukataji wa magogo. Kwa upande wa magogo kwanza mazingira yanaharibika, pili barabara zetu zinaharibika, madaraja yanaharibika kwa kuwa hawa wanaokata magogo wanapeleka magari makubwa sana huko Vijijini kwetu. Wanaharibu madaraja na barabara. Fedha za kutengeneza barabara hakuna. Naomba hili lizingatiwe.

Pia naomba isitishwe kwa muda ununuzi wa chuma chakavu au vyuma chakavu. Hii imeleta athari sehemu nyingi tu. Kuna watu wanavunja madaraja na kubeba hivyo vyuma na kwenda kuviuza. Kuna watu wanatoa vyuma ambavyo vimetengwa kwa ajili ya mifereji kiasi cha kwamba wengine wanapata ajali kuwa anakuta lipo shimo ghafla hata hapa Dodoma nimeona. Dar es Salaam mashimo ya aina hii yako mengi. (*Makofii*)

Naomba biashara hii sidhani kama ina manufaa ya kutosha kwetu isitishwe kwa muda pia mpaka hapo utaratibu utakavyofanywa wa kufanya biashara hii ifuatiliwe kikamilifu, kwa kweli chuma chakavu ndiyo inayopatikana na ndiyo inauzwa. Sio kutuharibia majengo ambayo yamejengwa kwa kutumia chuma au madaraja yaliyojengwa kwa kutumia chuma.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kuhimiza mikopo ya Benki ipelekwe kwenye sehemu husika hasa Vijijini. Kwa hivi sasa mikopo hii kusema kweli ipo sana mijini ambako ni wachache tu wananaufaika wengi wao tupo Vijijini. Walimu wa Vijijini mpaka sasa wengi wao hawajapata mikopo hasa kutoka *Bank* ya *Microfinance*.

Kwa kuwa *facilities* zilizoko katika Wilaya sasa hivi ni *Microfinance*. Lakini utaratibu wake sio mzuri bado haujakamilika kikamilifu kiasi ya kwamba wote waweze kufaidika. Tuna Madaktari, wauguzi wengi katika vijiji, Mabwana shamba na hata wafanyakazi wa Halmashauri zetu nao wanetaka kunufaika na wao ndio wanaoweka Serikali hapa tulipo kuliko wale walioko Mjini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali suala la simu kupeleka kila Wilaya lizingatiwe na lifanyiwe haraka iwezekanavyo. Sisi Wana-Liwale bado tuna kilio kikubwa kuhusu simu pamoja na hatua nzuri ambazo zinachukuliwa lakini bado hatujakamilishiwa na hatujajua hatma ya upatikanaji wa simu.

Leo hii nimepewa kikabrasha ambacho kinaonyesha kwamba simu imefika Wilayani kwangu au itafika hivi karibuni lakini hajatueleza hasa lini hiyo simu itafika.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake Wilaya yangu inatumia fedha nyingi sana kufuatilia au kwenda kuhudhuria mikutano hewa wakati wanajiandaa kwenda kwenye mkutano wanafika Makao Makuu ya Mkoa wanakuta ule mkutano umeahirishwa matokeo ni kwamba wamepoteza gharama za kusafiri mpaka kufika kule nadhani hivyo ndivyo ilivyo katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ihmize wawekezaji hawa waweleka simu mahali husika, kila Wilaya haraka iwezekanavyo kusudi kuondoa matatizo kama haya ambayo yanatugharimu bila sababu yoyote.

Mheshimwia Spika, hivi juzi wafanyabiashara wangu walikuwa wanafuatilia mbolea, walilazimika kwenda Mtwara wakakuta bado hajafika. Hizi gharama baadaye zinakwenda kwa mlaji, hili jambo ni bayu sana kwa mlaji kwa kuwa kama pangekuwa na simu wangkuwa wameshaelewa kwamba kuna mbolea au hakuna. Mtu angeweza kufunga safari yake kutokana na taratibu zitakazomwezesha yeye kujua anachokwenda kuchukua atakipata ama vipi.

Mheshimiwa Spika, katika hii Bajeti nimejaribu kufuatilia nimekuta kwamba haikuzungumzia chochote kuhusu ndege ya Mheshimiwa Rais. Nataka kujua ni lini ndege hii itapatikana hasa kwa vile mwakani ni uchaguzi? Ni vyema ndege hii tukajulishwa kwamba itapatikana awamu hii kabla awamu nyingine haijaanza. Itatuletea heshima wana CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukienda kwa upande wa uwekezaji, pamoja na mtandao wa simu tunaotumia, lakini ningependa kujua Serikali inajua vipi kuhusu hizi kadi tunazotumia kwenye simu kama *value* iliyowekwa pale kwa mfano Dola 5 au shilingi 5,000/= kweli zina thamani hizo? Naona katika eneo hilo hatuna *TBS*, ni nani anayetuhakikishia kwamba kadi ya shilingi 5,000/= ni kweli ina thamani ya shilingi 5,000/=? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema tena kwamba naunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami leo niweze kuchangia katika hotuba hizi mbili za Waheshimiwa Mawaziri wa Fedha na Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, pamoja na Profesa Anna Tibaijuka, kwa kuteuliwa na Serikali ya Uingereza kuwa Makamishna wa Tume ya Afrika. Naomba pia kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, ambaye amerudi Bungeni kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, naomba kuchukua nafasi hii kutoa pole sana kwa kaka yangu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na dada yangu Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba mkubwa uliowapata na pia kutoa pole kwa ndugu zangu Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere pamoja na Mheshimiwa Mama Anne Malecela, kwa matatizo waliyoyapata barabarani. Lakini pia, naomba kumpa pole na kumtakia afya njema, Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Bujiku Sakila, ambaye tunapata faraja sana tunapomwona akiwepo Bungeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ningeanza kwa kuonyesha viashiria fulani vichache tu ambavyo vinaonyesha kwamba kwa kweli kutokana na hivyo uchumi wa nchi yetu unakua. Katika mambo ambayo ni *indicators* nzuri, moja ni utekelezaji wa Mpango wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya matumizi ya wananchi wa eneo lile ambapo tunaamini kabisa pia baadaye utasaidia katika *irrigation*. Nasema hili ni muhimu kwa sababu ya vitisho vilivyokuwepo na jinsi Serikali ya kikoloni ilipolishikilia jambo hili la matumizi ya maji na kukabidhi matumizi yote kwa nchi ambayo iko mbali zaidi ya kilometra 400 kutoka kwenye Ziwa lenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mradi huo wa Ziwa Victoria, vile vile ninapongeza huu mradi wa Chalinze ambao ukiutazama umepita katika eneo zaidi ya kilometra 150 kuwashudumia wananchi. Katika Wilaya yangu nijivunie nini baada ya kusema kwa wenzangu?

Naomba niishukuru pia Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kuingiza Wilaya ya Muheza katika huu Mpango wa Maji na Mazingira unaodhaminiwa na Benki ya Dunia. Mradi huu kwa kweli utasaidia sana kuhakikisha Wilaya ya Muheza inapata maji ya kutosha katika mji wenye kwenye pamoja na kata zaidi ya nane.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni eneo la barabara ambalo wote tunafahamu limeshazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge. Suala la kuwa na uhakika wa baadaye wa kuwa na barabara ya lami kutoka Bukoba hadi Mtwara pamoja na kukamilika kwa daraja la Mkapa, hayo ni mambo ambayo yanaashiria kwamba sasa tunafungua milango ya kukua kwa uchumi. Lakini katika Wilaya yangu ya Muheza tutajivunia ahadi ya Serikali ya kusaidia kuweka lami barabara yetu ya kutoka Muheza kwenda Amani ambayo hapa Bungeni Mheshimiwa Waziri alisisitiza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, ninapongeza mradi wa *TASAF* ambao umefanya kazi kubwa ya kufungua barabara iliyokuwa na matatizo makubwa ya kutoka Magila kwenda Magoroto pamoja na barabara nyingine ambazo ndani ya Wilaya ya Muheza zimekwishafunguliwa na naomba wananchi wangu waendelee kuzitunza vizuri kwa sababu bado Serikali inaendelea na jitihada ya kufungua barabara nyingine zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ni Mpango wa Elimu ambao sihitaji kuuzungumzia sana kwani umefanya kazi nzuri. Lakini napenda niseme tu kwamba, dalili zimeanza kuonekana kwamba kazi hiyo nzuri katika kipindi kilichopita cha mwaka

2003 tunasikitika kwamba vijana wetu wengine ambao wamefanya vizuri katika mitihani yao wamekosa nafasi ya kwenda Shule za Sekondari. Hii inaashiria kwamba upo umuhimu wa utekelezaji wa Mpango huu wa Ujenzi wa Shule za Sekondari Kitaifa na hilo pia linaonekana.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni wiki mbili, tatu, zilizopita uchaguzi wa wanafunzi watakaoingia Chuo Kikuu katika msimu unaokuja umeonyesha vile vile dalili hizo hizo kwamba wapo wanafunzi wengi ambao wamefanya vizuri, lakini nafasi zitakuwa chache hawatakuwa na mahali pa kwenda. Kwa kweli hili linasikitisha, lakini inaonyesha kwamba tumechelewa kuchukua hatua za haraka na lazima sasa tujifunge kibwebwe tuweze kuhakikisha kwamba nafasi zinatosha. Wengine wamepata *first class*, lakini katika michepuo ambayo walikusudia kwenda nafasi hazikupatikana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nimshukuru tena Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwanza kwa kukubali baadhi ya mapendekezo ambayo nimeyatoa na kuyatumia vizuri katika Bajeti hii. Mapendekezo hayo ni pamoja na pendekezo la kufuta kodi ya stempu ambalo nililitoa hapa Bungeni na sasa limekamilika na ninashukuru sana. Hilo ndiyo pia limenisaidia sana katika kuweka wazo la kufuta hizi leseni za biashara. Nashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme wazi kwamba mawazo hayo yote yanatoka kwa wananchi wangu wa Muheza na nachukua nafasi hii kuwapongeza sana na naomba niwapongeze sana Waheshimiwa Madiwani watatu ambao waliandika barua ya kuonyesha jinsi wafanyabiashara wa Wilaya ya Muheza wanavyonyonyaswa katika mpango wao wa leseni. Waheshimiwa hao ni Diwani wa Majengo, Mheshimiwa Mkufya, Diwani wa Masuguru, Mheshimiwa Bosi na Diwani wa Mbaramo, Mheshimiwa Mussa. Nawashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa ningeomba vile vile wananchi wangu waelewe kwamba Mheshimiwa Waziri amefanya marekebisho kidogo katika ile *tax band* ambayo tulifanyia majadiliano kama miezi miwili iliyopita. Wananchi wengi wanajua kiwango cha chini pale ni shilingi 20,000/=, lakini katika mpango huu mpya wa marekebisho kiwango hicho sasa ni shilingi 35,000/=.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie wananchi wangu kwamba hakuna lililoharibika hapa kwa sababu katika kodi ya ushuru wa stempu walikuwa wakilipa kwa kiwango cha chini cha shilingi 3,000/= kwa mwezi walikuwa wanalipa zaidi ya shilingi 36,000/= kwa mwaka. Kwa hiyo, pamoja na shilingi 20,000/= za *income tax* maana yake walikuwa wanatakiwa kulipa kiwango cha zaidi ya shilingi 56,000/= kwa mwaka.

Sasa, kwa mpango huu mpya wa kufuta kiwango cha *stamp duty* na kubakiza kiwango cha shilingi 35,000/= tu kwenye kodi ya mapato, maana yake ni kwamba bado wana *advantage* kubwa kwamba wamepunguziwa zaidi ya shilingi 21,000/= kwa mwaka. Kwa hiyo, nilitaka hili niliweke sawa ili waweze kulielewa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuweka jambo hili sawa, sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kitu kimoja. Kwa taarifa naelewa kwamba *stamp duty* sasa mwisho wake itakuwa ni mwezi Juni, 2004 kwa sababu sheria mpya hii itaanza Julai, 2004. Basi tuambiane vema ili wataalam wetu huko katika Wilaya zetu wasiendelee kuanza kuwabana watu kwamba aah, hii itakuja mwakani. Wamekwishalipa *stamp duty* kwa miezi sita, mwisho ni mwezi Juni, 2004. Bila shaka hivyo ndivyo ninavyoolewa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama watakuwa wamelipa kwa miezi sita na kwa sababu wamekwishafanyiwa *assessment* ya kodi ya mapato katika kipindi kilichopita, watakuwa wanalipa shilingi 20,000/= mpaka kipindi kinachokuja. Kwa hiyo, ukizijumlisha hizi kwa pamoja unafikia pale pale Mheshimiwa Basil Mramba alipopiga mahesabu ya karibu shilingi 35,000/= au shilingi 36,000/=. Hivyo, hakutakuwa na tofauti na tuwaambie kabisa kwamba *stamp duty* mwisho mwezi Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, vile vile, ningeomba sasa suala la *TIN* mliweke vizuri kwa sababu kuna wafanyabiashara wale wa vijijini kule nao pia wanatakiwa waende *TRA* wakajiandikishe *TIN* kwa kiwango kidogo cha biashara wanachofanya.

Sasa tuliweke hili sawa kwa sababu nalo lisije likaanza kuwageukia wafanyabiashara wadogo wadogo tukidhani kwamba tumewasaidia wakaendelea kubughudhiwa. Nitashukuru sana kama Mheshimiwa Waziri atayaangalia hayo na kuyafanyi kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nije katika eneo lingine, eneo ambalo kwa kweli ni la kupungua kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. Inaonekana kwamba kupungua huko kumechangiwa sana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni, lakini njia pekee ambayo tumeambiwa inaweza ikasaidia ni kuongeza kasi ya mauzo ya nje.

Naomba kuchukua nafasi hii kwanza kupongeza mpango wa *EPZ* katika eneo lile la Dar es Salaam hasa viwanda hivi vya *NIDA Textile Mills, Millennium Business Park* pamoja na *Quality Industrial Park*, ambao kwa kweli wamefanya kazi nzuri ya kutuongezea mapato ya fedha za kigeni. Lakini naamini kabisa kwamba wao wamefanikiwa kwa sababu miundombinu Dar es Salaam imekaa vizuri.

Sasa ni nini tunachofanya kuhakikisha kwamba *EPZ* katika maeneo mengine zina *takeoff*? Tunafanya maandalizi gani Tanga? Tumefanya maandalizi gani Mtwara, kwa *Mtwara Corridor*? Tumefanya maandalizi gani kwa *Central Corridor*? Fedha ambazo zimetengwa kwa *NDC* ni kidogo sana na haziwezi kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni mambo ya *Crude Oil exploration*. *Shell* wanashindwa kutekeleza mkataba wao kule Kaskazini mwa Pemba na sababu kubwa ni mgogoro tu uliopo au kutolewana kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwamba suala la mafuta siyo suala la Muungano na kwa hiyo *Shell* wako kijiweni. Ni lazima tuelewe

kitu kimoja kwamba, *Shell* ni moja kati ya *big brothers* wa mambo haya ya utafutaji wa mafuta duniani na ndiyo wanaotegemewa sana.

Leo anapowakwamishwa, maana yake dunia nzima inajua kwamba *Shell* amekwamishwa Tanzania na si rahisi kumpata mtu mwingine atakayekuja kufanya *exploration* pale.

Kwanza kazi yenye *exploration* katika *deep seas* inahitaji aina fulani za *rig* ambazo ni maalum sana na ninavyofahamu mimi katika dunia ziko kama tano tu. *Rigs* hizo zikichukuliwa kukodishwa kupelekwa mahali pengine maana yake ni kwamba, sisi Tanzania hata tukimruhusu *Shell* kesho *rig* haitakuja, haitakuwepo imekwenda mahali pengine. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie tufanye maamuzi ya haraka.

Mheshimiwa Spika, nafahamu Oman kuna mafuta na kuna *refinery* pale, lakini jambo lingine ambalo ni lazima tulielewe ni kwamba, nchi nyingi za Kiarabu hazijihuishi sana katika mambo ya *exploration*. Kwa hiyo, tusitegemee kwamba zitakuja zitusaidie katika mambo hayo ya *exploration*. Wao wanajihuisha sana katika mambo ya *supply* na *distribution*. Nafahamu Makampuni ya *KPC*, *AMOCO* yote hayo, lakini hawaendi katika uchimbaji na utafutaji.

Kwa hiyo, *Shell* anataka kutumia shilingi zake bilioni 15 sisi tunasema hapana, hapana, tunavutana vutana! Hakuna mikataba mizuri kama ile ya utafutaji wa mafuta ambayo inasikitisha kwamba hata *proposal* za *amendments* kuletwa Bungeni zinacheleweshwa kwa sababu hiyo. Tuchukue hatua kwa jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la *LPG* kwa kifupi sana, kwamba tumefanya kazi nzuri ya kupunguza ushuru na kweli *supply* imeongezeka, hapa *figures* zinaonyesha kwa kiasi cha asilimia 52. Lakini ni lazima tutazame kwa upande wa pili. *Projected demand* yetu ni tani 50,000, katika kipindi hiki imeongezeka kwa tani 2,500 tu. Kwa sababu *stimuli's* nyingine zile za *promotion* hatujazifanya kazi na ni nini hizo? Ni kupunguza au kuondoa kabisa ushuru kwa hizi *cylinders* ili watu waweze kununua na waweze kutumia gesi.

Sasa kuna *cylinders* ambazo zinahitajiwa na magari yanayohitajiwa kusambaza gesi hayazidi matano kwa nchi nzima, tutakuwa tumepeoteza nini hapa kwa kufuta hizo? Wala siyo fedha nyingi. Kwa hiyo, tujaribu kuangalia hilo na nadhani ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, angalieni jinsi matumizi ya mkaa yalivyoongezeka. Ukitaka kujua mkaa unatumika Dar es Salaam hebu pita saa moja jioni angalia maghorofa yote unayoyafahamu, kaangalie maghorofa ya Urafiki, ya Keko, angalia maghorofa ya *Kilwa Road*, kaangalie maghorofa ya *TAZARA*, cheche za moto zinatoka ni mkaa mtupu unatumika kule. Lakini pamoja na hayo, hata *Oysterbay* nako cheche za moto wa mkaa zinaonekana. Kwa hiyo, matumizi ya mkaa na kuni kwa kweli ni makubwa sana na ni lazima tuchukue hatua ya kujaribu kupunguza.

Sasa ningeomba vile vile nizungumzie suala la mwisho ambalo ni la *Mafuta House*. Jengo lile ni kubwa na limesimama kwa muda sasa wa zaidi ya miaka minne, kile ni kipusa. Ni kipusa ambacho watu wengi wanakitamani na kimekaa pale kwa muda mrefu. Hivyo, ninaamini kuna watu wanakitamani sana. Lakini kama kuna watu wanakitamani na tunawenza kufikiria kufanya maamuzi yoyote tukumbuke kitu kimoja cha msingi sana kwamba, jengo lile ni la ubia kati ya *TPDC* na *National Housing*. *TPDC* walipolijenga jengo lile *basement* yake walijenga maalum kabisa kwa ajili ya kuhifadhi *data za exploration* na kama tutawapa watu wengine tukawanyima *TPDC*, basi tujue kwa uhakika hizi *data za exploration* ambazo zina *very high value* kwa nchi hii zitaendelea kuharibika.

Sasa hivi *data* zote hizo za *exploration* ziko pale Upanga katika ofisi zao na ziko katika *container*, sijui lilikuwa limeleta mizigo ya nani. Kwenye *container* unaweka *International data!*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vyovyyote vile akitokea mwekezaji awekeze, lakini *basement* ile maalum kwa ajili ya *preservation* ya *data* wabakiziwe *TPDC*. Tusiwaue *TPDC*. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante, kabla hatujuahirisha kikao, nikumbushe vikao viwili vinavyotuhusu Waheshimiwa Wabunge wote. Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani wana kikao kule kwenye sehemu walijotengewa na Waheshimiwa Wabunge wa Chama Tawala wana kikao hapa hapa ndani.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 06.48 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja zote mbili zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwanza kabisa kuwatokia heri na mema kwa wale wote waliofanikiwa. Lakini vile vile naomba nitumie nafasi hii kutoa pole na rambirambi zangu rasmi kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba uliowapata.

Mheshimiwa Naibu Spika na mimi nianze kwa kuchangia katika Bajeti ya mwaka huu, kwanza kwa kuiangalia Bajeti nzima ilivyotayarishwa. Bajeti ina ngazi nne kwa

kawaida, kwanza malengo ya Bajeti yenyewe, raslimali zikiwepo fedha na watu, halafu utekelezaji wake na hatimaye udhibiti na usimamizi.

Sasa ni lazima tuangalie kama tunataka kuisifia Bajeti hii tunaangalia katika ngazi zote hizo nne, je, malengo yaliyowekwa na Bajeti hii ni malengo yanayoweza kufikiwa? Kwa upande wa malengo naisifu sana Bajeti hii kwa sababu yanaenda sambamba na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Imelenga watu wa kima cha chini, kuwakomboa na kuwapatia fursa watu wa kima cha chini. Lakini raslimali sasa, je, tunazo raslimali za kuweza kutekeleza yale ambayo tumeyaweka katika Bajeti hii? Kazi nzuri inafanywa na *TRA* kama kuna mtu ambaye hajui *TRA* inafanya nini basi huyo atakuwa na kasoro zake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili wanasema mkia wa mbuzi unajifagilia pale alipo mbuzi mwenyewe na mimi ningependa kukisifia sana kitengo cha *TRA* pale Mbeya, wamefanya kazi nzuri kwa sababu wameongeza makusanyo. Nafikiri Ndugu Sisya amejitahidi sana, hata nafasi ya Mbunge wanaitambua. Ile hali ya kuwepo na elimu kwa walipa kodi kumesababisha angalau sasa Serikali iheshimike badala ya kukimbizana na walipa kodi. Ninawapongeza *TRA* Mbeya kwa kazi yao nzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningeomba katika upande wa *TRA* nisisitize jambo moja na lifanyiwe kazi, hawa wafanyakazi wa *TRA* ni binadamu, wanawenza wakawa na kasoro ndogo ndogo kama binadamu wengine tulivyo na kasoro ndogo ndogo. Hawa wafanyakazi wa *TRA* wanahitaji kupendwa, wanahitaji kuishi katika jamii kama wanavyoishi watu wengine. Wasingependa kuishi katika *isolation*, ni sehemu ya jamii wafanyakazi hawa.

Sasa Mheshimiwa Waziri Basil Mramba lipo tatizo kwa upande wa sukari. Bahati nzuri wewe mwenyewe ulitokea Mbeya na unajua jinsi soko la sukari lilivyoajiri vijana wengi pale kwangu Mwanjelwa. Maisha ya Mwanjelwa, Uyole, Mbalizi yanategemea sana soko la sukari. Tunaipongeza Serikali kwamba tulipozungumza hapa mlizingatia na mkatoa vibali. Lakini vibali vile vimetolewa kwa watu wawili tu, kinyume na sera za sasa hivi za soko huria. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukishawapa watu wawili hawa vibali watafanya *monopoly*, watahadhi. Sasa matatizo tunayoyapata ni haya na matatizo haya ndiyo yanayowakabili wafanyakazi wa *TRA* Mbeya. Hakuna mwongozo thabiti unaowaelekeza hawa wafanyabiashara ndogo ndogo watakusanya vipi hii kodi ili na wenyewe wachangie katika Pato la Taifa. Sasa matokeo yake ni *TRA* kufukuzana na watu kubeba sukari inakuwa ni kama vita wakitumia *FFU*. Lakini siyo kosa lao hawa watu wa *TRA* mwongozo gani umewekwa kuwasaidia kwamba hata hawa wafanyabiashara wadogo na wenyewe wachangie katika Pato la Taifa wasikimbie kimbie bali wafanye biashara iliyo halali na wazi na ndiyo tatizo tulilonalo. Hawa *TRA* wako wangapi? Watu ni wengi. Sasa wataishi katika hali ya uhasama mpaka lini?

Naomba muwatatalie hili na ni maombi yao wenyewe kwamba wanaona sheria ya kuwapa vibali wale watu wawili bado wao haiwapi unafuu wa namna ya kutekeleza

majukumu wanapokuwa wameikamata sukari au waelimishwe wale wafanyabiashara ndogo ndogo namna gani wafanye biashara zao, la sivyo tusipotatua tatizo hili tutakuwa tunazalisha majambazi. Watafanya kazi gani? Hii ni biashara yao iliyo halali. Lakini tunataka tuhalalishe wafanye ili na wenyewe wachangie katika Pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nimeliona na ninafikiri kwamba Mheshimiwa Basil Mramba, atalifanya kazi. Unaweza ukapata hata taarifa kutoka kwa wao wenyewe imekuwa ni tatizo kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba sasa nizungumze kwa uchungu kabisa na kutamani kulia lakini siyo mahali pake hapa. Nimetumwa na watu milioni 2 wa kutoka Mkoa wa Mbeya, wanasema kuna mambo manne ambayo Serikali na Bajeti hii inapaswa kuzingatia. (*Makofi/Kicheko*)

La kwanza ni utayari wa wananchi, wananchi wa Mbeya amba mara nyingi tunaonekana ni wabishi lakini kwa hiari yao na moyo wao wote wametoa ardhi yao ili itumike kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Songwe, pale wametoa ardhi yao. Nakumbuka ardhi hii ndiyo iliyokuwa inawalisha katika kupigana na janga la umaskini, sasa wameamua kwa hiari yao watoe ardhi hii iweze kutumiwa na Serikali kwa ajili ya maendeleo na nini matarajio ya wananchi hawa, wanajua kama Kiwanja cha Ndege cha Songwe kitajengwa na kitatoa fursa kubwa zaidi za kuibua uchumi wa Mbeya kuliko wao kuwa na vishamba hivi vyta kulima. Sasa Serikali itawasaidia vipi?

Juzi tulikuwa na semina hapa juu ya mikakati ya kuondoa umaskini, moja kati ya lengo kuu ni kuimarisha mawasiliano pamoja na miundombinu vikiwemo viwanja. Bahati nzuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000, imezungumzia juu ya kuimarisha viwanja vya ndege kama sehemu ya kuibua uchumi wa wananchi siyo kitu ambacho kinatoka hewani kipo pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ipo ahadi ya Rais, nataka nimkumbushe Mheshimiwa Basil Mramba, wakati Rais, anaweka jiwe la msingi la barabara ya Songwe kwenda Tunduma wakati anapokea ripoti ya Mkoa wananchi walimwuliza na alieleza na alisema ingekuwa ni furaha yake na angependa aone ndege ya kwanza inatua kwenye Kiwanja cha Songwe yeye akiwa bado madarakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ndiyo ahadi na ilikuwa ni mazungumzo na wananchi wamekamatia hapo na wanajua Rais wao ni mtu wa hekima na busara na mtekelezaji siyo mbabaishaji. (*Makofi*)

Sasa sidhani kama Serikali itakuwa tayari kumtosa Rais wetu ambaye amejijengea heshima kubwa katika nchi hii, aliahidi na kutoa kauli kwamba nitatimiza nione ndege ya kwanza inatua nikiwa bado madarakani. Rais mwenye maono, Mheshimiwa Basil Mramba una *challenge* kubwa kwa sababu wewe ndiye mtekelezaji. Lakini si utekelezaji tu naomba nitumie fursa hii vile vile kukupongeza sana, wewe ulipokuwa Mbeya ndiyo mtu wa kwanza kugundua kwamba Mbeya *is a strategic town* kwa maana ya biashara ya Kusini mwa Afrika hasa kipindi hiki cha utandawazi tunapojaribu kuimarisha *regional*

cooperation. Mbeya inatakiwa ifungue *the southern corridor* kwenda DRC, Zambia, South Africa, Zimbabwe, Lesotho na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilieleze hili fika *feasibility study* ilifanyika toka mwaka 1985 na waka-*revise* kuiweka iwe ya kileo mwaka 1987. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, sidhani kama ulikuwa Waziri wakati huo, lakini mipango ya Serikali ilikuwa pale pale. Sasa kama Serikali imeamua kutekeleza basi na tufanye kweli na nakumbuka siku ile Rais alizungumza kwa uchungu sana ni mwaka jana tu akasema ningependa sana Serikali iwe na miradi michache inayoweza kutekelezeka kwa wakati, kuliko kuwa na miradi mingi kila mradi ukatekelezwa nusu nusu *at the end of the day* unakuwa huna mradi uliokamilika. Hii ndiyo kauli ya Rais tulipokuwa tunajadiliana naye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Basil Mramba, wewe ndiye Waziri wa Fedha, umepewa Rais amekukabidhi jukumu hili ni changamoto (*challenge*) kwako. Kwanza naomba niishukuru Serikali usiposhukuru kwa kidogo hata kikubwa hutashukuru, Serikali imefanya kazi nzuri imetupatia shilingi bilioni 1.88 ambazo ndizo zilizofanya kazi ya kulipa fidia wananchi na vile vile kwa ajili ya kufanya clearance na kulisafisha lile eneo.

Naipongeza Serikali kwa sababu tayari mmetangaza *tender*, *tender* imefungulia na tumetiliana mikataba na wale wazabuni waliopewa *tender* hizi, lakini cha kushangaza Wizara iliomba bilioni tano, kwenye Bajeti yetu tumepewa bilioni moja, wakati wale wazabuni watatu kwa ajili ya kujenga *runway* jengo na sehemu zingine wanahitaji asilimia 40 kwa mujibu wa *tender* na asilimia 40 inawapeleka kwenye bilioni tatu na hawa tayari kisheria wameshasaini *documents*. Sasa itakuwa vipi katika utekelezaji wa mradi huu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mzima gharama yake ni shilingi bilioni 7.42, wananchi wa Mbeya wanajuliza kulikoni? Kama sisi maskini tumeji-sacrifice tumeachia eka zetu, mashamba yetu tufe sisi na watoto wetu lakini Serikali ipate nafasi ya kujenga uwanja kama ilivyoahidi, kigugumizi kinatoka wapi? Bahati mbaya nakumbuka ule wimbo wa *Atomic Jazz* kwamba tulikuwa mimi, baba na mama na mtoto baharini, kimbunga kikatukuta lakini uwezo wangu ni wa kuokoa mtu mmoja, nimwokoe nani? Mimi namuuliza Mheshimiwa Basil Mramba, unataka kumtosa nani, mtoto, baba au mama? Nani unayetaka kumtosa katika janga hili? Watu walijitahidi wakajibu, wakasema kama ni mtoto utazaa mwingine kilichobaki mwokoe mke wako, lakini ni kweli? (*Makofi/Kicheko*)

Sasa katika hili tunataka kumtosa nani? Chama? Mnataka kunitosa mimi Mbunge au mnataka kuwatosa akina Mheshimiwa Edson Halinga, wazee? Mimi sitakubali maana bado ndiyo kwanza nimeonja na hata mzee anahitaji chakula kizuri zaidi ili aweze kusogezza siku zake na sisi tuendelee kupata hekima kutoka wazee hawa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua mimi ni *product* yako ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba za Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafshaji ilioletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Awali ya yote na mimi naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Waziri Dr. Abdallah Kigoda pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kupotelewa na mzazi wao mpendwa. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niwape pole Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliopata misukosuko pamoja na ajali walipokuwa safarini kuja Bungeni. Lakini vile kwa dhati kabisa naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kurudi tena Bungeni kwa kishindo kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Hongera sana, unakaribishwa. Tumekupokea na tunaamini hutarudi tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hotuba zote mbili moja kwa moja kwa sababu lazima nikiri kwamba kwa kipindi cha sasa miaka minne iliyopita kuna mambo mengi sana yamefanyika katika awamu hii ya Serikali.

Kwanza nikitoa mfano kule kwangu Mbinga au Mkoa wa Ruvuma ilikuwa inachukua saa tano kutoka Songea hadi Mbinga kwa gari, sasa barabara imeboreshwa inachukua saa moja na nusu. Kwa muda mrefu magari yalikuwa hayaendi Lituhi, sasa gari hata ndogo zinaweza kwenda Lituhi kwenda na kurudi kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa sana. (*Makofi*)

Pamoja na mafanikio hayo bado kuna tatizo huku nyuma palikuwa na mipango ya kujenga barabara kutoka Songea mpaka Mbinga kwenye kiwanda cha kahawa kwa lengo la kuboresha zao la kahawa. Kama mnavyofahamu kahawa kama inapita kwenye vumbi ina tabia ya kushika vumbi na hiyo kupunguza ubora wake. Jitihada hizo zilifanyika madaraja yakajengwa, barabara ikajengwa kilometra 20, ikakomea hapo. Sasa leo nilipokuwa nauliza swali la nyongeza ilielekea Mheshimiwa Naibu Waziri, hakunielewa lakini baadaye ameelekea kunielewa, ameliona kwamba ni jambo la msingi kwa sababu kwa kweli hii miundombinu inataka kwanza ielekezwe kule ambako uzalishaji ni mkubwa kama Wilaya ya Mbinga. Tukumbuke kwamba Wilaya ya Mbinga inazalisha kahawa nyingi kuliko sehemu yoyote katika nchi hii. Asilimia 20 ya kahawa inatoka Mbinga. Kwa hiyo, ni muhimu Serikali nayo ikalionna hilo. (*Makofi*)

La pili ningependa tuzungumzie suala la uboreshaji wa miundombinu mingine muhimu. Wilaya ya Mbinga, ni moja kati ya Wilaya ambazo ziliahidhiwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba itakapofika mwaka 2005 Wilaya zote zimepata umeme. Ni matumaini yangu kwamba umeme huu utapatikana, kama hautapatikana nategemea kwamba Serikali ijieleze vizuri. Nilishasema hapa kwamba Bunge hili litawaka moto na nasema wazi kwamba suala la umeme si kitu cha mchezo kwa sababu hakuna nchi hata moja hapa dunia ambayo imeendelea bila umeme. (*Makofi*)

Hivi sasa Mheshimiwa Rais ni Mwenyekiti Mwenza wa Tume ya Utandawazi na amekwishesasema kwamba hatuwezi tukakwepa utandawazi lazima tuijandae. Sasa mimi nashangaa tutajiandaaje ikiwa kama maeneo mengine hayana umeme? Hivi hata huko kuboresha shule ambako mimi nakiri kwamba Serikali imefanya kazi kubwa sana. Lakini tunaboresha idadi ya watu au tunaboresha elimu hivi kuna mtu hapa atatuambia ni tofauti gani kati ya elimu uliyokuwa unafundisha miaka 20 na elimu inayofundisha leo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni kweli elimu hii itapambana na utandawazi? Haiwezekani. Sana sana kama ni suala la kufundisha *computer* litafanyika kwenye miji na yale maeneo ambayo tayari yamepata umeme. Kwa hiyo, mimi ni ombi langu na hili ninaelekeza upande wa mipango kwamba umefika wakati Serikali, sasa ibadilishe mtizamo umeme uwe ndiyo kipaumbele, mambo mengine yatafuata, watu watajiendeleza wao wenywewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la umeme lisiletewe mchezo. Mchezo wa kutegemea umeme wa maji, nadhani hautatusaidia popote kwa sababu maji haya kwanza yanatakiwa kwenye kilimo. Sasa sisi tunalegalega, tunashindwa kuchukua maamuzi ya haraka ya kuhakikisha kwamba tunatafuta umeme kutoka kwenye mkaa lakini badala yake tunaona kwamba hili ni tatizo. Mimi nadhani tatizo la kutokuamua tena kwa haraka litatufikisha mahali pabaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa niseme kwamba Serikali imefanya vizuri sana ni la mawasiliano hasa ya simu. Mimi nilimwandikia *kinote* siku moja Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi nikamuuliza kuna uwekezano wa kupata simu ya mkononi? Akasema ngoja tuangalie, simu imepatikana wananchi wa Mbanga wanashukuru sana. Lakini wanaomba yale maeneo mengine ambayo waliahidiwa kama sehemu ya Maguu ambaa inazalisha kahawa nyingi sana nayo ile ahadi itimizwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka nizungumze ni hili suala la Benki ya Wakulima. Mimi nakuwa na wasiwasi kidogo kwa sababu kuanzisha leo Benki ya Wakulima itakuwa ni kuturudisha nyuma. Labda mtuambie hii Benki ya Wakulima itachukua jukumu gani? Lakini kama ni mfumo wa *National Micro Finance Bank* mimi sikubaliani nayo kwa sababu inapingana yenyewe huwezi ukawa na kitu kinaitwa *National* halafu kikawa *Micro*, is a contradiction, haiwezi ikafanyakazi hata kidogo.

Mimi nadhani maadamu wananchi sasa wameitikia kuwa na Benki zao wananchi zinazotilia maanani mazingira ya maeneo yale ni wakati muafaka sasa wa kuhakikisha kwamba hizi fedha ziende zikaimarishe juhudzi za wananchi. Fedha hizi pale ambapo bado hawajaanzishwa basi ziende *SACCOS*. Sisi tumejifunza mambo mengi sana kwamba ilikuwepo na mifuko ya pembejeo, lakini matumizi hayajamsaidia mtu yeoyote.

Kwa hiyo, pamoja na mifuko mingine ya mikopo kama kwa vijana, akinamama hii mifuko yote imetumika vibaya, badala yake iende benki wakachukue huko,

naisisitizwe kwamba anayechukua mkopo alipe lakini vile vile, liwe ni jukumu la Serikali kuwapa elimu hawa watu namna ya kusimamia mikopo hiyo ili iwe na maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba niseme kero moja ya mwisho na ningeomba nipatiwe maelezo mwaka jana tulijulishwa katika Bunge hili kwamba Halmashauri zetu zitakuwa zinatoza asilimia tano ya mapato kama *crop sales*. Lakini mimi napenda nipate maelezo sahihi, kuna Wilaya nyingine zinatoza asilimia tano bei ya shambani, lakini kuna Wilaya kama yangu kuna ushindani. Tozo hili linakwenda kutozwa kwenye mnada, matokeo yake ukilinganisha inaonekana kwamba wanatozwa zaidi ya asilimia kumi na hizi fedha zinakwenda kuchukuliwa kwenye mnada. Sasa wananchi wamenituma itolewe taarifa rasmi na pawe na utaratibu mmoja kwa nchi nzima wa kutoza tozo hilo kwa sababu jinsi wakulima wa kahawa wa Mbeya wanavyotozwa yaani, Mbozi ni tofauti kabisa na wakulima wa Mbinga wanavyotozwa. Kwa hiyo, hili ni ombi ningeomba tupate majibu ili mambo yaweze kwenda sawa sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba nishukuru tena kwa jinsi Serikali, ilivyofanya vizuri sana katika mpango wa MMEM na hasa kule Mbinga, watu waliweza kujenga madarasa mengi sana zaidi ya mara tatu ya yale ambayo yalikuwa yamepangwa.

Kwa hiyo, sina budi kuwapongeza na kwa kweli walimu wamekuwa wakifanya vizuri lakini naomba kama Wabunge wenzangu walivyosema kero la malipo ya walimu tafadhari lishughulikiwe vinginevyo tutawakatisha tamaa walimu wetu. Wale waliohusika basi wachukuliwe hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tatizo lingine ambalo ningependa, najua halitawapendeza lakini lazima niliseme ni kwamba suala la mzunguko wa fedha Mheshimiwa Waziri Basil Mramba, niliwahi kuzungumza na wewe, suala la mzunguko wa fedha ni matatizo makubwa sana. Noti ya shilingi 10,000/= inamnufaisha nani, inawanufaisha watu wa mjini na mjini ndiyo kwenye mabenki, kule vijijini ukienda na noti ya shilingi 10,000/= hupati chenji. Noti hii ndiyo inayogusiwa, inayosababisha mzunguko haramu wa fedha. Hivi ikitolewa kutakuwa na matatizo gani katika mzunguko badala yake tukaongeza noti za shilingi 5,000/= na 2,000/=ambazo zitawasaidia wanavijiji kuendesha biashara ya fedha. Nakwambia huku vijijini hakuna fedha, watu wanaendesha biashara sasa hivi ya ujima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema wazi kabisa ya kwamba kuna watu wanafanya biashara hiyo haramu ya noti ya shilingi 10,000/= pamoja na kwamba noti hii inawafanya wafanyabiashara wahodhi fedha badala ya kuzipeleka benki. Hivi kweli Watanzania sasa hivi tuko katika hali ile ile ya kutembea na mamilioni ya fedha kwa nini tuisitumie mbinu za kisasa, lazima tuweze kutumia *negotiable instruments*. Mimi natoa rai kwamba na ninaamini kabisa kwamba tukiondoa hiyo noti wale amba wanataka kutembea na mapesa mengi basi wawe wanaweka kwenye magunia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. FRANK M. MUSSATI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hizi mbili. Na mimi naomba nitoe rambirambi kwa Waheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kumpoteza baba yao. Ama nimpe pole Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan kwa kumpoteza mwanaae.

Nawapa pole Wabunge wenzetu waliopata majanga na matatizo mbalimbali wakati wakija kwenye Kikao hiki cha Bunge. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuingia Bungeni, kwa kutumia mlango mkubwa wa uhakika. Karibu Mheshimiwa Danhi Makanga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kutoa pongezi kwa Serikali hasa Serikali Kuu kwa kutufanyia mambo mengi mazuri tu Mkoani Kigoma. Kwanza mradi wa MMEM nadhani hakuna Mkoani uliotekeleza vizuri kama Mkoani wa Kigoma, tumefaidika sana na mradi wa MMEM. (*Makofî*)

Tumefaidika vile vile kwa mwaka huu kwa mara ya kwanza kabisa tangu tupate Uhuru, Mkoani wa Kigoma tumeweza kufungua Sekondari 9 kwa mara moja. Tunaishukuru sana Serikali na tunawapongeza, nawapongeza wananchi wa Mkoani wa Kigoma wote, Wilaya ya Kigoma, Wilaya ya Kasulu na Wilaya ya Kibondo, chini ya uongozi wa Mkoani akiongoza Kanali Mahawa, Mkuu wa Mkoani, Kanali Makunenge Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Henry Clemence, Mkuu wa Wilaya ya Kigoma na Luteni Kanali Mzurikwao, Mkuu wa Wilaya ya Kibondo. Nawaambia hongera sana. (*Makofî*)

Sasa sisi Mkoani wa Kigoma, tumepeata Sekondari, tumepeata shule za msingi nzuri sana. Lakini naomba niseme kwamba pamoja na hayo umaskini uliopo Kigoma ni wa ajabu sana, unatisha. Sisi ni matajiri wa umaskini. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna mahali ambapo umaskini umekithiri ule Waingereza wanaita *object poverty* utaupata Mkoani wa Kigoma. Sasa tumepeata shule, tumepeata zahanati nyingi tu, kwa bahati mbaya tunazo zahanati kadhaa hazina wafanyakazi wala vifaa. Kwa hiyo, tunazo tu kama *white elephants*. Hatuna barabara, hatuna umeme na kama mnavyo jua bei za mafuta, petroli na dizeli na mafuta ya taa zimekuwa zikipanda kila siku. Mwezi wa tatu wakati bei ya petroli Dar es Salaam lita moja ilikuwa shilingi 700 na kidogo, Kasulu tayari tulikuwa tunanunua lita ya petroli shilingi 1,200/=. Lita ya dizeli ilishafikia shilingi 900/=.

Sasa hilo ongezeko la juzi nina uhakika kabisa kwamba lita ya petroli Kasulu sasa hivi itakuwa inakaribia 1,500/= na lita ya dizeli nina uhakika iko kwenye shilingi 1,000 na kidogo. Sasa mimi sijui kwa mwendo huo tutakosa kutajirika kwa umaskini kweli? Huo mwendo unatisha sana na vyombo vile ambavyo tulitegemea vingetusaidia katika kuangalia bei za mafuta kama *EWURA* mpaka leo hiki chombo hakijaanza.

Chombo ambacho kingetusaidia labda kuangalia *Surface and Marine Transport (SUMATRA)* mpaka leo hakijaanza. Kwa hiyo, sisi Tanzania nzima tutaumia lakini sisi Mkoani wa Kigoma tunaumia zaidi kwa hivi vyombo kutoanza kazi. Kwa hiyo,

namwomba Mheshimiwa Waziri, atueleze *EWURA* na *SUMATRA* vinaanza lini ili viweze kutusaidia hasa sisi tunaotoka hii Mikoa ya pembezoni na sisi tuweze kufurahia matunda ya Uhuru. (*Makofi*)

Vile vile ningependa kujua ni lini Mkao wa Kigoma utaunganishwa na gridi ya Taifa ya umeme. Mkao wa Kigoma ni Mkao ambao una Wilaya za zamani sana. Wilaya ya Kasulu imeanza mwaka 1919. Kibondo mwaka 1946. Kigoma labda mwaka 1919 lakini Wilaya ya Kasulu hasa ninakotoka mimi, umeme hatujuui, mpaka inabidi upande gari uende Kigoma kama siku hiyo kutakuwa na umeme Kigoma kwenyewe mjini ndiyo unaweza ukaambiwa kwamba hicho ndicho kitu kinaitwa umeme, vinginevyo tunasikia tu umeme hatujuui ni kitu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sisi tunaomba umeme jamani. Mheshimiwa Rais alipokuja mara ya mwisho mwezi Septemba, 2000 akinadi Chama Cha Mapinduzi na kuomba kura, alituahidi sisi wakazi wa mji wa Kasulu kwamba haitafika mwaka 2003 kabla hamjapata umeme mji wa Kasulu. Lakini leo hii tarehe 17 Juni, 2004 bado tuko gizani. Bado tuko gizani na hakuna hata matumaini.

Sasa sijui sisi tufanyeje? Sasa huu umaskini uliokithiri na nchi inatangaza kwamba tunapiga hatua kupambana na umaskini na umaskini unaisha. Umaskini unapungua, mimi sijui unapungua namna gani. Labda Wabunge wenzangu, mimi kila kukicha mimi kama Mbunge naona umaskini unaongezeka tu wangu mimi mwenyewe binafsi. Sasa sijui mwananchi wa kawaida, umaskini wake unapungua. Ni kweli umaskini unapungua?

Mheshimiwa Naibu Spika, unapungua? Sisi kwa viwango hivyo na umaskini huo uliozidi mimi naona unazidi kuongezeka tu. Sasa unaongezekaje? Ukiangalia dondoo ya Bajeti hii 2004/2005 dondoo ya 12 ambayo inasema Sekta za kipaumbele chini ya mkakati wa Taifa wa kupunguza umaskini. Sekta iliyoongezeka kidogo elimu, afya kidogo, maji kidogo, barabara kidogo, sheria kidogo, ukimwi kidogo, kilimo kimepungua yaani mwaka 2003 na mwaka 2004 afadhali hata mwaka 2003. Mwaka 2004 imepungua kidogo.

Sasa lakini imepungua kwa ajili gani? Nadhani *we are not serious about it*. Kwa sababu kilimo tunatumia bado zana za kizamani za Adam na Eva. Hakuna zana za kisasa na zana za kisasa siyo kwamba hatutaki zana za kisasa ni kwamba zana za kisasa hazinunuliki. Trekta milioni 30 na kitu. Sijui hapa kati yetu Wabunge nani ana trekta sijui kama yupo. Sasa kama Mbunge hawezি kupata trekta Muha wa kawaida anaweza akapata trekta? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusichukue hatua za makusudi, Serikali ikaamua kutoa ruzuku kwa bei za zana za kilimo. Kwani kuna shida gani kwa mfano Serikali ikalipia kila ikileta shangingi moja inaleta na trekta moja. Haya mashangingi tunaweza kuyanunua mengi tu, tukachukua hatua za makusudi kwamba ukileta shangingi moja ulete na trekta mbili na trekta liuzwe milioni tano kwani kuna shida gani. (*Makofi*)

Jembe la mkono kama ninavyosema sisi wa Kasulu, Kigoma tuna matatizo kweli. Jembe la kawaida shilingi 2,000 mwananchi wa kawaida kupata shilingi 2,000 atapata wapi jamani. Kwa nini jembe lisiuzwe kwa shilingi 500/=? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zana za uvuvi, mashine ya boti, *HP 48*, milioni tatu na nusu nani atapata hiyo hela. Nyavu, wavu mmoja unahitaji vipande 10 na kila kipande ni shilingi laki moja na elfu tisini na moja. Kwa hiyo, unahitaji milioni mbili kupata wavu wa kutosha kuvulia, utazipata wapi? Hiyo inaitwa Kipe, utapata wapi Kipe. Huwezi ukapata milioni 2, milioni tatu na nusu ya mashine na milioni kama tano ya kujengea mtumbwi wenye. Kwa kweli mimi nashauri kwamba ni vyema Serikali ikachukua hatua kuhakikisha kwamba zana za kilimo, zana za uvuvi, zana za ufugaji, zinapata ruzuku kutoka Serikalini. Hakuna namna nyingine. (*Makofi*)

Sisi wana Kasulu tunaitika mwito wa kuongeza kilimo. Kuna vijiji vitatu vya jimboni kwangu tumelima tangawizi. Mwaka huu tutalima tena tangawizi ni mwaka wa nne mfululizo tunalima tangawizi lakini hatuna mnunuzi. Vijiji vya Kalela, Kigogwe na Mzeze. Tuna zaidi ya tani laki moja ya tangawizi ambayo imelimwa bila kutumia mbolea. Hatuna mnunuzi. (*Makofi*)

Mara ya mwisho tulipata mnunuzi mwaka 2000 alikuwa akinunua kilo moja ya tangawizi shilingi 50/=, hebu niambie umaskini utaisha kweli kwenye nchi hii? Kilo moja ya tangawizi shilingi 50/=. Baada ya hapo *DC* aliyekuwepo akamfukuza huyo Mjerumani kwamba alikuwa mwizi. Kumbe alikuwa walau anatusaidia kwa hiyo shilingi 50/=. (*Kicheko*)

Sasa hata hiyo shilingi 50/= hatuipati tena kwa hiyo, tangawizi inalimwa imokusanya tu, haina mnunuzi. Sasa kweli ndiyo tunapambana na umaskini hivyo? Mwananchi ameambiwa alime, analima. Lakini anachokilima hakinunuliwi. Sasa tufanyeje?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitamwomba Mheshimiwa Waziri anayehusika kwa kweli anipe jibu na anihakikishie ni lini hiyo tangawizi yetu itanunuliwa. Vinginevyo kwa kweli atakuwa ananikaanga mimi mwaka 2005 nitakaangika hasa na itakuwa vigumu hasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi naona uchungu sana na nirudie tena kusema kwamba kama kuna Mkao ambaa una utajiri wa umaskini, Mkao wa Kigoma umepiga hatua kubwa kabisa na sisi tunapata kitu ambacho ni kibaya tu, wakimbizi tunaletewa sisi. Sasa hivi tuna wakimbizi zaidi ya laki nne. Hatuna barabara, hatuna umeme, hatuna kila kitu. Ila tuna kila kitu kibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ingawa kwa shingo upande. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami niwe mmoja wa wachangiaji katika hotuba hii. Lakini kwanza

naomba nitoe mkono wa rambirambi au mkono kwa wafiwa, kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao na pia Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kufiwa na mtoto wake. Hiyo ni safari ya kila mmoja wetu na sisi tunasema *Inalilahi Wa Inailahi Rajuu* na *inshallah* Mwenyezi Mungu aziweke maiti zao mahala pema.

Pili niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa katika Taasisi za Kimataifa, *AU* pamoja na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa katika ile Taasisi ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa. Lakini pongezi zangu hasa zimwendee Mheshimiwa Getrude Mongella kwa kuchaguliwa kama Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika. Kuchaguliwa kwake haikuwa ni sifa kwa yeye peke yake lakini ilikuwa ni fahari kubwa kwa Tanzania na hasa kwa Bunge hili lililokuwa limemchagua kutuwakilisha kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi zangu kwa Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji kwa hotuba safi ambazo wametuletea. Hizi ni hotuba za ukombozi na kwa kweli imejibu masuala yote yale ambayo watani wetu upande ule wa Kambi ya Upinzani walikuwa wameweka kama ndiyo Sera yao ya kupigia debe mwaka 2005. (*Makofi*)

Tumeshaiweka sawa hiyo na sasa labda tutafute lingine. Lakini vile vile naomba kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kuja kuiwakilisha tena na kuitia nguvu CCM katika Bunge hili kutoka katika Jimbo la Bariadi Mashariki na nawasihi ndugu zetu upande wa upinzani kwamba kosa walilolifanya wasilifanye tena. Ndiyo kwa sababu tunawataka wapinzani tuwe nao Bungeni. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Na mwanzo nimesema kwamba nimeipongeza hotuba hizo hasa kwa vile hatua muhimu walizozichukua kama vile kutuelekeza katika mustakabali mzuri na kuwasaidia kuondoa umaskini ndugu zetu wafanyabiashara na wakulima wadogo wadogo. Kuondosha kodi ndogo ndogo za biashara, Serikali kuongeza pato la *TRA* kuanzia miaka ya 90 bilioni 21 kukusanya mpaka miaka ya 2004 kukusanya bilioni 108 hiyo ilikuwa sifa kubwa sana na tunawapongeza kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa hotuba zote za Wabunge wote tulikuwa tunazungumzia suala la kilimo na ni mbinu ya kuondoa umaskini. Kwetu sisi maana yake kuondoa umaskini ni kuimarisha kilimo. Na katika hotuba na taarifa mbalimbali zilizotolewa hapa tumeona kwamba wakulima Watanzania au kilimo kinachangia zaidi ya asilimia 50 ya Pato la Taifa, siyo hivyo tu lakini vile vile ajira inapatikana zaidi kati ya asilimia 75 mpaka 80 ya wakulima katika Tanzania.

Bajeti iliyokuwa imetengewa Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2003/2004 ilikuwa kama bilioni 45.7 na wakati huu tunapozungumzia kilimo ni uti wa mgongo au sekta kongozi kwa kuondoa umaskini Tanzania safari hii Bajeti imetengewa 47.8 bilioni. Lakini ukilinganisha kuna baadhi ya Wizara zingine kama *Defence* imetengewa laki moja na thelathini na sita bilioni tena hiyo ni *OC* peke yake.

Sasa tunapozungumza Tanzania ni maskini na tunapozungumza kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo au kilimo ndiyo ajira peke yake kwa Watanzania na kilimo kwamba ndiyo mategemeo ya kuinua nusu ya pato la nchi hii na tunaitengea pesa kidogo kiasi hicho. Tunaelekea wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii kwa kweli Watanzania, kama watu wazima na sisi kama viongozi kama tulioletwa hapa, tunaowakilisha zaidi ya watu milioni 34 tuko hapa tunazungumzia, tunasemea. Sisi bado tunashindwa kusimama na kusema kwamba kama hii ndiyo sekta kiongozi kwa nini isitengewe pesa za kutosha ikaweza kutuongoza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inaonekana kwamba sisi bado hatujawa *serious* katika suala hili na kama tuko *serious* basi tungejielekeza wote tukaona kwamba kilimo tunakipa *first priority* tukaacha mambo mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kuna mwenzangu hapa alisimama na akasema kwamba ingekuwa sisi tungejipanga sote tukasema tunafunga mkanda, kama tulivyofunga katika mwaka wa 1978/1979 na tukasema kwamba jamani mengine yote tunasahau lakini tuondokane na fedheha hii ya kutegemea chakula cha omnia omba, kumbe tujifunze nini. Tunategemea chakula cha misaada kumbe tujifunze nini, mwaka uliopita tumekutana na janga la njaa, kumbe tujifunze nini.

Kenya leo kuna watu wanakufa na kuna matatizo ya njaa. Katika Afrika kuna tatizo la njaa. Sisi bado tumekaa tunasema kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo. Kilimo ndiyo sekta kiongozi. Lakini hatukichukulii kilimo *seriously* kama vile ambavyo tunasema. (*Makofi*)

Kama watu wazima na kama viongozi hili kweli linahitaji kulisimamia katika hali hiyo. Sasa najua kwamba bajeti hii tumemaliza. Lakini kwa kuongezea, nakumbuka wakati fulani alipokuwa anazungumza Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, alisema kwamba kwa nini tusingefanya semina Wabunge, tukakaa tukalizungumzia suala la kilimo peke yake halafu baada ya hapo tukaelekeza nguvu zetu zote na tunakubaliana vipi na tutazipeleka vipi.

Hilo halikufanyika na leo Bajeti inaonyesha kwamba tumepewa bilioni 47 katika Wizara ya Kilimo na kilimo chenyewe tunachozungumza kwamba ndicho kinachotuongoza kwa kila kitu halafu sisi tunapiga blaa blaa. Sasa hii itatifikisha wapi? Naomba mwaka unaokuja tuache yote, kama mkanda basi tujifunge mkanda kujiekeleza katika kilimo. Tupunguze matumizi katika Wizara na Taasisi nyingine kuona kwamba tunajiekeleza zaidi katika suala la kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nataka kulizungumzia lilikuwa ni suala la wastaifu ambalo wenzangu vile vile wamelizungumzia. Lakini mimi nataka nielekee upande wa wastaifu wale wa *East African Community* iliyovunjika mwaka 1977. Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa nataka atuelezee suala lile, wastaifu wale wamefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha inasemekana zimelipwa na Uingereza ili walipwe pesa zao wale Wastaafu wa *East Africa Community*. Kenya na Uganda wamelipwa sisi Tanzania pesa zimelipwa. Kwa nini hawa wastaafu hawajalipwa? Mheshimiwa Waziri naomba utakapokuja uweze kutujibu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania Bara wanazungumzia suala linaitwa MMEM. Sisi Tanzania Visiwani hatuna MMEM, lakini tuna kitu kinaitwa *TASAF*, najua kwamba *TASAF* na MMEM ni vitu tofauti lakini inawezekana kwamba vinafanya kazi moja wakati fulani au zinakubaliana wakati fulani. Tunatoa pongezi kwa Serikali na tunaomba kwa nguvu zetu zote sisi *TASAF* ndiyo inayotusaidia. Tunapongeza sana Serikali kwa hatua zote walizochukua na kutusaidia. Na kwa kweli katika kila mradi wa *TASAF* ulioletwa Zanzibar umeleta sura ambayo ni ya ukombozi kwa upande wa elimu, kwa upande wa afya, upande wa maji na katika sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. RAYNALD A. MROPE: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa maoni yangu. Lakini kabla sijafanya hivyo, naomba nami nitoe pole nyingi kw wenzetu waliopatwa na misiba hasa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda. Pia ndugu yetu Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan naye kwa kumpoteza binti yake.

Kwa namna ya pekee kwa kupitia Bunge lako Tukufu naomba kupeleka salaam zangu za rambirambi kwa wananchi wa Jimbo langu la Massasi, ambao hivi majuzi tarehe 13 Juni, 2004 waliwapoteza watu 12 katika ajali mbaya iliyotokea katika Mto wa Nangoo wakati basi la TAWFIQ lilipoingia kwenye mto huu na kuua watu pamoja na kupelekea majeruhi wengi. Kwa hiyo, naomba sana kwa kupitia Bunge lako, kupeleka salaam zangu za rambirambi.

Baada ya hapo, nami pia nataka kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa maajabu makubwa aliyoyafanya kwa kupita kwa nguvu zote na kuonyesha kwamba CCM ni kiboko yao. (*Makofi*)

Baada ya haya, nilitaka kuzungumza kwamba mengi yamezungumzwa na sekta nyingi zimeguswa katika maoni ya Wabunge. Ninalotaka kusema ni kwamba mimi nakubaliana karibu na yote yaliyozungumzwa na Wabunge na nawaomba wenzetu katika Wizara mbalimbali kama wameyasikia wayachukue kama ni *constructive criticism* itakayowasaidia kufanya vizuri zaidi siku za usoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu nilitaka kuchangia katika eneo moja ambalo nimeona halijazingumziwa sana, nalo ni eneo la utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii ni sekta inayokua kwa kasi kubwa sana duniani na hivi sasa ndio inayoajiri watu wengi zaidi, karibu mtu mmoja katika kila kumi. Kwa

hiyo, ni sekta ambayo si ya kupuuzwa. Hasa wenzangu upande wa mipango nilitegemea kuona utekelezaji wa sera ya utalii iliyotolewa siku nyingi kidogo, Utekelezaji wa miaka kumi wa Sera ya Utalii lakini haikujionyesha sana katika hotuba ya Mipango.

Nataka kukumbusha kwamba utalii unatoa mchango mkubwa kwa Pato la Taifa. Hivi sasa ndio kilimo kinaongoza kwa asilimia 45.4 ya *GDP* lakini utalii ni ya pili kwa kutoa asilimia 16 halafu inafuatwa na madini ambayo inatoa asilimia 10 au chini ya hapo. Mapato kwa mwaka, mwaka jana katika biashara ya utalii tulipata dola za Marekani milioni 731 au 25% ya Pato la Taifa. Kwa hiyo, hiki ni kitu kikubwa na haki yake kizungumzwe na kipewe uzito unaostahili katika Bunge letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuangalia ni kiasi gani katika Bajeti yetu kitakwenda kusaidia shughuli za utalii. Nimeona Bodi ya Utalii imetengewa shilingi bilioni moja na milioni minne ambapo mwaka 2003 walitengewa bilioni moja na milioni mia saba. Sasa nashangaa kwa nini kumekuwa na punguzo la namna hii.

Nataka kuishauri Wizara ya Fedha kwamba hapa tuangalie kwa sababu dunia nzima biashara ya utalii ni ya mashindano. Ukitulinganisha sisi na Kenya, mwaka 2003 peke yake wenzetu wa Kenya walitumia shilingi bilioni 10 kwa ajili ya shughuli za utalii, Afrika ya Kusini walitumia shilingi bilioni 30 na mwaka huu wametenga shilingi bilioni 40, sasa sisi sekta yetu inayoendesha shughuli za utalii tunaitengea shilingi bilioni moja na milioni nne, hii ni haki kweli, kweli tunataka kupambana katika shughuli hizi?

Matokeo ya ufinyu huu wa bajeti itatufanya sisi tusionekane katika masoko, tutashindwa *ku-promote* mauzo ya utalii wetu na tutashindwa kutengeneza vipeperushi vya utalii vitakavyoweza kuonyesha vivutio vyetu katika Tanzania na tutashindwa kabisa kuitangaza nchi yetu kwani matangazo ya television za Kimataifa kama *CNN* kwa dakika tatu kwa mwezi unalipa shilingi milioni 250, sisi kweli tutaweza kujitokeza katika maeneo hayo na kushindana na wenzetu? Mwaka jana ndio tulileta watalii 576,000 na mwaka huu tulikuwa na nia ya kuleta 600,000 lakini kwa mpango huu wa Bajeti finyu itakuwa vigumu kutoa huduma sahihi kwa watalii wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara ya Fedha na Mipango iangalie tena jinsi walivyotoa fedha katika bajeti hii ili kuendeleza utalii. Kwa kutengewa shilingi bilioni moja kuendesha shughuli za utalii ni kichekesho na ambapo Bodi ya Utalii wanahitaji kiwango cha chini kabisa kiwe walau shilingi bilioni tano. Naomba katika bajeti hii hebu muangalie tena tunaweza kufanya namna gani ili kuhakikisha kwamba utalii katika nchi yetu unakua kwa kuwapatia Bodi ya Utalii amba wanaiwakilisha Serikali, fedha za kuhimili ushindani na nchi jirani. Hili litekelezwe katika Bajeti hii.

Sasa hivi tunataka utalii huu uenee sehemu zote hasa maeneo yale ambayo yamesahauliwa kwa muda mrefu, maeneo ya Kusini kuna vivutio vingi, Kilwa kuna fukwe safi sana, kuna mambo ya kale, unakuja mpaka Mtwara fukwe za ajabu, moja kwa moja mpaka Ruvuma kuna mambo mengi makubwa, njoo mpaka Udzungwa, Ruaha, sehemu hizi zote hazijafunguliwa, Magharibi kwa wenzetu Kigoma huko kuna Sokwe na mambo chungu mbovu sasa tutawezeje kuyatangaza mambo haya kama fedha ni finyu

kiasi hiki? Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana suala hili lipewe umuhimu unaostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu udhibiti wa fedha za kigeni. Naona sisi ni peke yetu ambao tunaikumbatia na kuithamini sana dola. Angalia majengo ya kisasa yote yanayojengwa sasa hivi Dar es Salaam, ukienda kuuliza bei utaambiwa *square meter* fulani ni dola 140, *square meter* fulani ni dola fulani, hawaitambui shilingi hao, ukienda kukata tiketi ya ndege utaambiwa dola fulani, ukienda kuomba chumba hotelini, hoteli hizi za kitalii nazo zote zinatumia dola. Hivi kwa nini Wizara hii, kwa nini Benki Kuu isichukue sarafu yetu ikaipa umuhimu kwamba mtu yejote anayekuja atumie shilingi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbona *Vodacom* sasa hivi wameshaanza utaratibu wa kutumia shilingi, *voucher* zao tunalipia kwa shilingi? Sasa kwa nini haya majumba yapimwe kwa *square meter* kwa dola? Huu sio utaratibu mzuri hata kidogo. Wenzetu Kenya wanakwambia kama unataka kitu nunua kwa *Kenya Shilling*, ukienda Afrika ya Kusini nunua kwa *Rand*, hata wenzetu wa Uganda unanunua kwa shilingi sasa kwa nini sisi hatuithamini sana shilingi yetu? Tuwaambie wafanyabiashara wote waende kubadili pesa zao ziwe katika shilingi ya Tanzania ndipo ziweze kutumika. Kwa njia hii tutapata faida kubwa katika kubadilisha pesa hizo. Jukumu hili ni la Wizara ya Fedha wala halihitaji kufika tena Bungeni, toeni amri tu kwamba kuanzia tarehe fulani kama ukienda hotelini ulipie kwa *Tanzania Shilling* sio kwa dola. (*Makofi*)

La mwisho ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu *Mtwara Development Corridor* (Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara). Mpaka hivi sasa naona kwa upande wetu wa Tanzania tunachezacheza, tunaona kitu hili kama sio *serious*. *Mtwara Development Corridor* wenzetu wote waliokaribu nasi wa Malawi, Msumbiji, wanatuambia mbona ninyi mnakwenda taratibu mno kwa sababu watu wa Malawi wanataka sana njia hii Mtwara lakini mpaka leo tunalegalega, kwa nini? Siku zote tumesema ukitaka *Mtwara Development Corridor* iende kwa haraka tuanzishe taasisi itakayokuwa inasukuma maendeleo hayo ya *Mtwara Development Corridor*. Hivi kuna ubaya gani kuanzisha taasisi hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukitoka Mtwara kwenda Songea unakuta alama X tu zimechorwa katika nyumba za watu kwamba humu baadaye kutapita barabara lakini wananchi wanalamika jamani hizi X hizi ni za nini na hiyo barabara itakuja lini?

Kwa hiyo, naomba sana tuwe *serious* katika jambo hili tuweke ofisi itakayoshughulikia *Mtwara Development Corridor*. Marais wetu hawa ndio wanang'atuka, Bakili Muluzi ameondoka, Joachim Chissano anaondoka Desemba, Benjamin Mkapa anaondoka mwakani sasa tutabaki na nini? Ni lazima tukazane wakati huu tuhakikishe kwamba *Mtwara Development Corridor* unafanya kazi wakati Marais hawa wawili bado wapo, tukizidi kuchelewa sana itakuwa *Mtwara Development Corridor* iko katika vitabu vyetu tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa kuna jitihada zinafanywa lakini hata ile ofisi ya NDC basi ihamie Mtwara walau watu wa Mtwara wasikie kwamba jina hilo walilotoa kwa ajili ya ukanda huu mkubwa kumbe sasa inakuwa kweli lakini kama tutaendelea namna hii wananchi wengi wataanza kukosa imani kwamba *Mtwara Development Corridor* itakuwepo.

Baada ya kusema haya, ingawa nilikuwa na mengi kuhusu kilimo cha umwagiliaji, nataka kusisitiza kwamba umwagiliaji ni lazima uwe katika mito na mabwawa ambayo yapo siyo katika mifereji na vijito vidogo vidogo. Bila kuwa na *master plan* itakayoanzia Mto Rufiji, Malagarasi na kadhalika, sio vijito vidogo vidogo. Hicho kilimo cha umwagiliaji kichukue maji na kutumia wakati wa kiangazi sio kungoja kifuku ndio unamwagilia, hapana. Nafikiri Waziri wa Kilimo ananisikia bila shaka katika programu yake atatueleza ana mpango gani kamambe katika maeneo haya yenyе uhakika wa maji kuliko kule anakopeleka kwenye vijito vidogo vidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, kwa dhati kabisa naomba kuunga mkono hoja hizi mbili zilizoletwa na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge wale ambao walikuwa kwenye orodha ya leo, wale ambao walikuwa humu ndani wote wamepata nafasi. Baada ya kufika hapo naona ni vizuri tukaahirisha ili tuendelee kesho. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 12.12 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,
tarehe 18 Juni, 2004 Saa Tatu Asubuhi*)